

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Tatu – Tarehe 30 Oktoba, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama kawaida yetu siku ya Alhamisi kazi zetu zinaanza kwa maswali kwa Waziri Mkuu kwa muda wa dakika 30. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu mwulizaji wa swali la kwanza leo ni Mheshimiwa Mzee John Samwel Malecela.

MHE. JOHN S. MALECELÀ: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la kwanza.

Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi sasa kuna tatizo la uandikishaji wa vijiji vipyta, vijiji ambavyo zamani vilikuwa kama vitongoji lakini sasa vimekuwa vijiji vingi na vikubwa na pia kuna tatizo la ugawaji wa kata. Sasa mambo yote haya yanashughulikiwa na TAMISEMI.

Je, Serikali haingeona uwezekano wa kukasimu madaraka ya uandikishaji wa vijiji yaende kwene Halmashauri za Wilaya na suala la uandikishaji wa ugawaji wa kata liende kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, kwa hiyo kuondoa msongamano ambao sasa hivi uko TAMISEMI kiasi kwamba viko vijiji ambavyo vimependekezwa na Halmashauri zaidi ya miaka 10 iliyopita lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mzee Malecela swali lake zuri sana kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kuendeleza utaratibu huu wa kutaka jambo hili liwe linaamuliwa katika ngazi hii ni kwamba kuna masuala ya kifedha ambayo yanaendana sambamba na uanzishwaji wa vijiji, kata na maeneo mengine mapya. Kwa hiyo, kwa msingi huo Serikali bado inaona ni vizuri uamuzi kama huo ukaendelea kubaki

mikononi mwetu ili hilo liweze kuwa ni jambo ambalo linatu-*guide* katika kuamua vijiji vingapi safari hii turuhusu itakuwa na *component* ya Watendaji na kata ngapi kwa sababu utaongeza mambo mengine ndani ya kata. Kwa hiyo, hiyo ndiyo sababu moja kubwa sana. Vinginevyo tungeweza tukakasimu mikoani huko na Halmashauri zetu lakini uwezekano kwamba vingezalishwa vingi wakati mwingine bila ya kujali jambo hili lingeweza kuleta matatizo baadaye kidogo.

Lakini kwa utaratibu wa sasa bado hakuna tatizo kubwa hata kidogo. Nadhani Mzee Malecela unaliuliza hilo kwa sababu una baadhi ya maeneo ambayo umeshaomba na zoezi hili kusema kweli limeshakamilika kilichobakia ni kutangaza. Lakini kutangaza kule nako kunategemea mambo fulani fulani. Kwa mfano masuala ya kata hatuwezi kuyatangaza kwa sababu yanaingiliana na Majimbo. Kwa hiyo tunachofanya hapa ni kuianisha wakati muafaka karibu na Uchaguzi Mkuu ujao ndipo matokeo haya yatangazwe kama maandalizi ya wakati huo. Nikijaribu kurekebisha kitu chochote sasa hivi maana yake lazima na Majimbo mengine yatakuwa yameingiliana mipaka na yenyeewe utalazimu yaweze kufanyiwa marekebisho.

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kweli kwamba suala la Watendaji wa Vijiji linakuja kama ni mojawapo ya kufikiria. Sasa jimbo la Mtera linalo tatizo ambalo baada ya bwawa lile kuanza kutumika na wavuvi kuja tunavyo vijiji zaidi ya 20 ambavyo viko kandokando ya bwawa lile na tumepeleka maombi sasa karibu nasema kweli karibu miaka 10 lakini hayajaweza wala kufikiriwa hata kujibiwa tu barua kwamba jamani maombi yenu yanafikiriwa. Kama ni hili suala la fedha bado kuajiri kwa Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata bado inafanyika katika ngazi ya Halmashauri.

Kwa hiyo nina hakika Halmashauri ingeweza ikashauriana na Serikali. Bado nafikiri kwamba mengine ingekuwa vizuri Serikali ifikirie tena jambo hili upya tuone namna tutakavyoweza kulitekeleza vizuri zaidi kuliko hali ya sasa.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mzee Malecela rai yake bado naona anayoisisitiza ni ile ile, lakini niseme jambo ambalo sikuwa nimelisema. Mheshimiwa Mzee Malecela katika maombi tuliyoyapokea kwa ajili ya vijiji tumepokea maombi 225. Katika maombi 225 ni maombi 42 tu ndio yaliweza kukidhi vigezo. Kwa hiyo liko tatizo vile vile la Halmashauri kutokuzingatia vigezo ambavyo ni muhimu sana katika kuanzisha vijiji. Kwa hiyo tunaling'ang'ania hili kwa sababu ni suala la Utawala Bora, ni suala la uwezo wa kijiji katika kuamua kama kiwe ni Serikali ya Kijiji au hapana.

Lakini bado nasema Mheshimiwa Mzee Malecela hata hilo ambalo nasema bado suala la fedha linaamuliwa na Halmashauri ni kwa sababu wanaolipa bado ni Serikali Kuu. Watendaji wote wanalipiwa na Serikali Kuu. Kwa hiyo ni lazima tujue kwa kweli *implications* za zoezi lolote ambalo litajitokeza. Lakini aah!!! Mzee ukiuliza swali gumu namna hii basi tuseme wacha tutaliangalia *as time goes on. (Makof)*

MHE. MOHAMED H. J. MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkoo kwa kuwa tuna utamaduni ambao tumeuzoea umekuwa kama sheria kikawaida kujadili hotuba zote za Mheshimiwa Rais anazozitoa hapa Bungeni. Na kwa kuwa mara hii katika Mkutano wa 13 hatutojadili hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyotoa katika Mkutano wa 12 kwa sababu kuu 2 ambazo ni muda na kwamba *hansard* hazijakamilika. Je, utatuhakikishia kwamba Mkutano wa 14 tutaweza kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkoo suala hilo sio la kwako. Kwa sababu tulipokaa Kamati ya Uongozi ambayo inamhusisha Spika, Mwenyekiti na Wenyeviti wote ndio Wajumbe ndio inayopanga ratiba ya nini tufanye katika Bunge hili. Kwa hiyo, ye ye hakushiriki na wala hajui. Kwa hiyo, naomba sana ikubalike kwamba ni Kamati ya Uongozi.

Unaniuliza mimi?

MHE. MOHAMED H. J. MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, lagine dogo la nyongeza ambalo litamhusu ye ye.

NAIBU SPIKA: Lakini sio hili?

MHE. MOHAMED H. J. MNYAA: Halihusiani na hili, ni swali lagine.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkoo wewe ndio Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni na kwa kuwa suala la kujadili hotuba ya Rais halimo katika kanuni zetu. Je, sasa hivi Serikali iko tayari kuliweka katika kanuni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge unabishana na mimi sasa, basi naomba ukae. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkoo, kuhusiana na suala la Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkoo aliyejiuzulu Mheshimiwa Edward Lowassa, katika kipindi chake chote cha Uwaziri Mkoo hakuwahi hata siku moja kutumia ziara ya Kiserikali kufanya kazi za chama chake. Katika kipindi chako cha muda mfupi cha Uwaziri Mkoo mara mbili umefanya ziara za Serikali na umegawa kadi za chama chako na kupokea wanachama wa chama chako. Je, unatumia fedha za umma kufanya kazi za chama chako au chama chako kinashiriki katika ruzuku inayopata kukuchangia unapokwenda kufanya kazi za chama wakati unafanya ziara ya Uwaziri Mkoo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Zitto Kabwe swal i lake kama ifuatavyo. Kabla sijasema hivyo nataka tu niseme kwa Mheshimiwa Mnyaa akija baadaye nitamnong'oneza alichokuwa ametaka kujua maadam Mheshimiwa Naibu Spika ameshalirekebisha.

Mheshimiwa Kabwe unalolisema linawezekana lina ukweli mimi sikufutilia sana kama aliyahidi kufanya au hakuwahi kufanya. Lakini haya ni mambo ambayo wakati mwingine yanatokea tunapokuwa kwenye ziara. Ratiba imepangwa, lakini unafika kwenye kituo unakuta kuna ratiba nyingine ndogo ndani ya Wilaya inayohusika. Wakati mwingine inakuwa vigumu sana kusema hapana kwa sababu ya mazingira halisi yalivyo. Lakini niongeze kusema tu kwamba kwa nafasi hizi tulizonazo Mheshimiwa Kabwe hata ungekuwa wewe ungepata taabu. Mimi ni mjumbe wa Kamati Kuu, ni mjumbe wa Halmashauri Kuu, ninapokwenda mikoani kufanya ziara ni kweli nakwenda kufanya ziara nikiwa Waziri Mkuu lakini ni vigumu sana kuziondoa hizo kofia nyingine.

Lakini kubwa ninapokwenda kule kusema kweli nakwenda kukagua shughuli za maendeleo ambazo ni matokeo ya Ilani ya Chama kinachotawala. Kwa hiyo wakati naelewa unachosema ni nini lakini nataka vile vile unielewe na mimi *position* yangu ndiyo maana nimesema katika mazingira haya wakati mwingine sio rahisi kulikwepa hata kidogo.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya ziara na kushirikisha shughuli za chama ilikuwa ni mwaka 2007 mwezi Aprili, baada ya kelele za wananchi hajawahi kufanya hivyo tena. Vile vile nimekupa mfano wa Waziri Mkuu aliyekutangulia ambaye hakuwahi kushirikisha licha ya kwamba naye alikuwa mjumbe wa Kamati Kuu, licha ya kwamba alikuwa mjumbe wa Halmashauri hakuwahi kushirikisha shughuli za chama na shughuli za Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wabunge wa CCM wajue hili kwamba unapofanya ziara za Kiserikali unatumia fedha zetu wanaolipa kodi ni wana-CCM, ni wana-CHADEMA, ni wana-CUF na wasio na vyama, je, utaacha sasa kufanya shughuli za chama? (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilinde.

NAIBU SPIKA: Umeshauliza swal?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ataacha sasa kutofautisha.....

NAIBU SPIKA: Mwachieni nafasi amalize. Eee!!! maliza sasa.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Waziri Mkuu utaanza sasa kutofautisha shughuli za Serikali na za chama chako?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kwa nini Mheshimiwa Kabwe unaona nalo hili kama kikwazo kikubwa sana.

NAIBU SPIKA: Agenda ya siri

WAZIRI MKUU: Mimi sijaona kwamba ni tatizo kubwa sana. Ni kweli ninapokwenda pale nimekwenda Kiserikali natumia gari ya Serikali nakwenda kufanya kazi. Unaacha kuona kazi kubwa niliyokwenda kuifanya ya kuangalia shughuli za wananchi kwa upana wake, unaona tatizo kubwa ni kupokea kadi za wana-CCM 10 katika kazi yote niliyoifanya, kidogo na mimi napata taabu sana kuelewa *problem* hasa ni kitu gani?

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Kwa kuwa kuna madai mbalimbali ya walimu na kwa kuwa madai haya mengine ni ya muda mrefu na ndio chanzo cha walimu kutaka kugoma. Je, Serikali itatekeleza lini au itashughulikia lini madai hayo ambayo yameshahakikiwa?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mzee Lubeleje kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili ambalo limekuwa likiendelea hivi karibuni kwa sehemu kubwa limeshakamilika. Halmashauri 133 zimeshahakikiwa isipokuwa Halmashauri 14 ambazo zoezi linaendelea. Katika Halmashauri hizo ambazo zimeshahakikiwa tayari kiwango cha fedha zinazohitajika ni bilioni 9 na pointi kidogo hivi. Katika hizi shilingi bilioni 6.5 madai yake tayari yamekwishaanza kushughulikiwa na Wizara ya Fedha, kiasi kilichobaki tunaendelea kukamilisha tuwasilishe Hazina ili na zenyewe ziweze kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kusema hili, labda nitoe maelezo kidogo ya ziada. Jambo hili la malimbikizo ya madai ya walimu kwanza si jambo zuri hata mimi sipendi sana kwa sababu linakera sana. Lakini ni matatizo ya taratibu ambazo tunadhani nazo ni ndefu mno. Kwa hiyo nimewaambia wenzangu Serikalini humu pengine tutazame huu utaratibu wa masuala kutoka Halmashauri kwenda Idara Kuu ya Utumishi, toka Idara Kuu ya Utumishi iende Hazina halafu itoke Hazina irudi TAMISEMI kwa lengo la kurejesha *feedback* nadhani ni mlolongo mrefu sana kwa watumishi amba ni zaidi ya asilimia 52. Pengine tungeweza tukakasimu madaraka haya kwenye mikoa kwa maana ya kuthibitisha, baada ya pale ziende moja kwa moja Hazina, Hazina watalia na Idara Kuu ya Utumishi. Kwa hiyo tunaliangalia kwa maana ya kujaribu kupunguza mlolongo lakini vile vile tunaomba na walimu nao kwa kweli watekeleze wajibu wao vizuri. Baadhi ya madai tuliyoyagundua wamedanganya tena kwa kiasi kikubwa tu sasa nalo hili si zuri sana ndio linafanya Serikali tung'ang'anie kutaka kuhakiki kwa sababu baadhi ya walimu kutokuwa waaminifu sana.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimwulize Waziri Mkuu suala moja.

Kwa kuwa wakati inavunjika ile iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kulikuwa na nchi 4 tu wanachama nazo ni Uganda, Kenya, Tanzania na Zanzibar. Lakini baadaye mwaka 2000 kwa busara za viongozi wa nchi hizo walifufua Jumuiya ya Afrika Mashariki na hata kuwakaribisha nchi jirani za Rwanda na Burundi.

Suala langu lipo hapa, je, ni hasara gani iliyoipata Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondoa uanachama wa Zanzibar katika Jumuiya wakati nchi waanzilishi kama Kenya na Uganda hazikuwa na pingamizi yoyote kwa Zanzibar kuwa mwanachama kamili wa Jumuiya hiyo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Salim Khamis maswali yake siku zote lazima uyasikilize vizuri sana, kwa sababu kila likiulizwa lazima ujue linaelekea wapi. Naomba tu niseme kwamba ni kweli kabisa wakati Jumuiya ya Afrika Mashariki inavunjika uanachama ulikuwa ni *inclusive* pamoja na Zanzibar na walikuwa na *shares* zake. Sasa kulitokea nini baada ya pale, kilichokuja kutokea baada ya pale wakati tunarejea ilishakuwa tena sura ni tofauti kwa maana ya kwamba ni Jamhuri sasa ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo kilichofanyika ilikuwa kwa kweli ni kujaribu kuingia katika mfumo mpya na ndiyo maana hata wakati ule kilichofanyika ilikuwa ni kujaribu kuanzisha jambo ambalo tunadhani litaendeleza dhana sasa ya uelewa wa nchi moja kama vile Tanzania badala ya kuendelea kuwa na vipande *inclusive* labda upande wa Zanzibar. Kwa hiyo kwa kweli hakukuwa na mantiki nyingine tukiondoa suala tu la Muungano kwamba lazima twende nalo kama ndio mtazamo mpya wa Taifa letu.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kwa kuwa nchi wanachama hasa waanzilishi hawakuwa na pingamizi yoyote kwa Zanzibar kujiunga na Jumuiya hiyo. Je, Serikali ya Muungano itakuwa tayari kukubali ombi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pindi likiletwa rasmi kwa Serikali ya Muungano kujiunga au litawakatalia kama ilivyowakatalia kujiunga na Shirikisho la Soka la Dunia (*FIFA*) au kujiunga na *OIC*?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, si jukumu kwa kweli la nchi hizi nyingine wanachama kutuamulia sisi juu ya mfumo wa kujiunga na Jumuiya hiyo hata kidogo. Hili ni jukumu letu kama Taifa la Tanzania. Ili mradi tumekubali kwamba Taifa hili ni moja la Tanzania sasa kurudi nyuma tunakwenda kutafuta nini? (*Makofii*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali dogo. Swali langu kimsingi linahusiana na wastaifu na nitajikita zaidi kwa wastaifu wa Jeshi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwa kuna malalamiko kuhusiana na kutokulipwa kwa wastaifu wa Jeshi na malalamiko hayo yawezekana yametokana na mchanganyiko fulani sasa nitahitaji wewe unisaidie kama msimamizi wa Serikali.

Kuna makundi matatu ya tuzo ambayo hawa wastaa fu wanatakiwa walipwe. Kuna kundi la kwanza ambao wanatakiwa wachukue malipo yao ndani ya mwezi mmoja hii imekuwa *introduced* mwezi Julai, 2008 hapa karibuni. Kuna kundi la 2 waliandikiwa wachukue chini ya miezi 6 na kuna kundi la 3 liliandikiwa baada ya miezi 6.

Sasa kumetokea tatizo kundi la kwanza ambalo ni ndani ya mwezi mmoja wao wanlipwa kama kawaida. Kundi la 2 ambalo ni chini ya miezi 6 nao wamejikuta kwamba wanlipwa kama kawaida. Sasa limetokea hili kundi la 3 ambalo hawa walipewa tuzo kihalali ambao waliandikwa baada ya miezi 6 ndio wao wanakwenda kuchukua fedha zao.

Sasa kutokana na mkanganyiko huu hawa watu wakienda Hazina wanaambiwa kwamba tumeshalipwa, lakini ukweli ni kwamba wanaolipwa ni yale makundi mawili tu. Lalamiko hili linaanzia mwezi Januari mpaka Juni, 2008 ambayo kuna rekodi kabisa *NMB* kwamba fedha zimebekwa lakini wao wanapewa usumbufu.

Sasa nilikuwa naomba unipe msimamo wa Serikali hasa kuhusiana na kundi hili la tatu ambalo ni tuzo iliandikwa miezi 6 baada ya miezi 6 wanakwenda wanasumbuliwa hawalipwi. Serikali inasemaje?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mdee swali lake kama ifuatavyo:-

Kwa bahati nzuri ameanza vizuri tu kwamba ni tatizo. Sasa kwa sababu ni tatizo basi na mimi nikuombe dada yangu nipe muda kidogo nilifanyie kazi halafu baadaye nitakupa jibu ambalo ni la uhakika zaidi.

MHE. DR. ALI TAARAB ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu ukiondoka leo kwenda Morogoro hadi Iringa utakuta maeneo makubwa ya misitu na milima imechomwa kabisa na hiyo inatokezea kila mwaka wakati wa kiangazi. Ni uharibifu mkubwa wa bioanuwai (*biodiversity*) labda niseme. Aina ya miti na wanyama inaharibiwa kila mwaka.

Je, inatosha tu Serikali kuzungumza hili kuchukua hatua au kuna njia gani sahihi na thabiti za kuweza kuzuia uchomaji huu wa moto. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Yaani kuanzia Morogoro?

MHE. DR. ALI TAARAB ALI: Kuna uchomaji wa moto kuanzia Morogoro, milima ya Kitonga sasa hivi inawaka.

NAIBU SPIKA: Kitonga haiko Morogoro.

MHE. DR. ALI TAARAB ALI: Ehee!!!! ndio inawaka sasa kwa hivyo uharibifu huu unatokezea.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema Mheshimiwa pale kwa sehemu kubwa ni kweli na wala sio eneo hilo tu uchomaji moto Tanzania ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata jana tu *actually* naweza nikasema pengine mpaka leo, moto umewaka Mlima Kilimanjaro na tumelazimika sasa kuingilia kati kujaribu kufanya kila litakalowezekana kuuzima. Ni tatizo kwa nchi nzima.

Sasa Mheshimiwa anauliza hivi Serikali inachukua hatua gani au tufanye nini ili kukabili ana na tatizo hili? Namna moja ni kuendelea kulisemea kama tunavyolisema. Wananchi wanakusikia na wanansikia kwamba ni vizuri Mtanzania akajua kwamba uchomaji moto tunaoita moto kichaa ni jambo la ovyo halina tija na kusema kweli lina athari kubwa sana.

Lakini tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali, tumejaribu kutengeneza sheria ndogo tumewabana baadhi yao, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro ye ye akaamua kutumia Uanajeshi wake moto ulipowaka akaamua kuchukua *fire brigade* zote pandisha mlimani kwenda kuzima ule moto na wanavijiji wote, lakini bado ukipita Morogoro utaona watu wanachoma misitu. *So issue* ni kubwa sasa inawezekana kwa sababu utamaduni huu bado umejikita mno katika fikra za watu kutokujali, kutokuchoma moto sasa lazima tuendelee kulisema na kulisema na kulisema.

NAIBU SPIKA: Mmm!!! Mheshimiwa Ali Taarab Ali umeridhika? Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kujua tatizo ni mwanzo wa kutafuta njia ya usuluhishi. Nasema kujua tatizo ni mwanzo wa kutafuta njia ya utatuzi. Kwa kuwa Tanzania ni nchi maskini sana na ambapo

haipaswi kuwa maskini na kwa kuwa nchi yetu ilipokuwa inapata uhuru nchi nyingi za Afrika kama vile Nigeria zilikuwa sawa kimaendeleo pamoja na sisi.

Lakini leo hii nchi hizo zimekuwa na maendeleo makubwa ikiwa ni pamoja na zile nchi za Asia. Lakini leo hii Tanzania bado tuko chini sana. Je, wewe unadhani ni sababu gani hasa ambazo zimetufanya Tanzania tuendelee kubakia nyuma na sasa Serikali yetu itafanya nini ili nchi yetu iweze kusonga mbele?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Nyami kwa swalii zuri lakini anauliza kitu ambacho wote tunatakiwa tukijibu tu. Huyu Waziri Mkuu wa miezi 9, 7, au 8 ni kama alivyo tu Ponsiano katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tatizo la umaskini si jambo ambalo nalionia leo, ni tatizo ambalo tumekuwa nalo kwa kipindi kirefu. Sasa tulikosea wapi huko siku za nyuma, hilo pengine sasa itakuwa ni kwa lengo la kujiuliza tufanye nini ili tuweze kuondoka hapa tulipo.

Mimi nadhani jambo la msingi sasa maadam tumetambua kwamba tatizo letu la umaskini likoje na sasa hivi Bunge hili wote mmekuwa mkijielekeza sana katika kusema tufanyeje tutoke hapa tulipo tuweze kwenda hatua moja mbele. Mimi nadhani huo ndiyo mtazamo sahihi, tushirikiane tuweke nguvu zetu pamoja, tuwe na Sera, Sheria na tuwe na maelekezo ambayo yatatuwezesha kutoka hapa tulipo ili tuweze kupiga hatua ambayo ni ya kasi kubwa zaidi. Juhudi zilizoanza si mbaya kwa sababu imetuondo angalau katika hali ya *inflation* ambayo ilikuwa mbaya sana, *GDP* kidogo tumeiongeza lakini bado wanasesma ni lazima tuongeze jitihada zaidi hasa katika sekta za uzalishaji. Kwa hiyo, mimi nadhani inawezekana ilimradi tujumuike na tufanye kazi kwa pamoja.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa vile mambo mengi tumeyaainisha katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi yanayotoa muongozo mzuri sana kuelekea kwenye maendeleo yetu. Lakini tatizo kubwa tunalokumbana nalo pia ni pamoja na uzembe mkubwa uliopo maofisini watu wengi hawataki kuwajibika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nyami unaingia kwenye *debate* sio maswali.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Je, Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba watumishi wale ambao ni wazembe sasa wanaachishwa kazi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za nidhamu kwa watumishi zimekuwa zikichukuliwa kila ilipobainika kwamba amekosea, ndani ya Halmashauri hata ndani ya Serikali Kuu. Lakini naomba niseme tu kwamba hilo peke yake bado halitoshi.

Mimi nadhani kubwa ni jitihada za kila mtumishi mmoja mmoja kwanza kujua anatakiwa kutekeleza wajibu wake kwa uadilifu mkubwa, kwa bidii kubwa na kwa maarifa makubwa. Tukiamua tukadhamiria wote kila mmoja kwa nafasi yake baadhi ya matatizo mengi tunayoyaona sasa yatapungua yenyewe. Lakini nadhani kasoro kubwa bado iko katika uadilifu wetu sisi wenyewe.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wa kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkoo maswali ya moja kwa moja umekwisha na bahati nzuri wote walioomba wamefikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri tena tunaomba tukushukuru, isipokuwa Waheshimiwa Wabunge leo hamkufanya vizuri sana. Hamkufanya vizuri sana *in the sense* kwamba tunapouliza maswali tusiende nje. Nilipomwuliza Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali kwamba unataka kusema ni Morogoro tu? Mimi nilifikiri alikuwa anazungumza kitaifa uharibifu wa mazingira. Sasa ukisema Morogoro tu inaonekana unaenda Morogoro. Kwa hiyo ni vitu kama hivyo tunatakiwa tuulize maswali ya kisera ambayo Waziri Mkoo yeye kama yeye hana tatizo. Lakini mengine yapo kama yakiwizara wizara. Tulanza vizuri na nadhani turudi kwenye utaratibu ule ambaa tulikuwa tunafanya vizuri. Sasa tunaendelea, Katibu.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 30

Wananchi Waliobomolewa Nyumba Tabata

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI aliuliza:-

- (a) Je, ni wananchi wangapi waliobomolewa nyumba zao pale Tabata Dampo?
- (b) Je, wananchi hao walilipwa kiasi gani cha fedha kama fidia yao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki Mbunge wa Ole kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kubomoa nyumba za wananchi katika kiwanja Na. 52 kilichopo eneo la Tabata Dampo, ambacho kinamilikiwa na *Allied Cargo Freighters Ltd* kwa miaka 18 lilifanyika kati ya tarehe 27 -28/2/2008. Ubomoaji huo ulifanyika kwa kufuatia amri ya Mahakama baada ya Wananchi kuvamia na kujenga nyumba za kuishi kutokana na mmiliki kushindwa kukiendeleza kiwanja hicho kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi waliobomolewa nyumba walizokuwa wamejenga katika Kiwanja Na. 52 kilichopo eneo la Tabata Dampo jumla yao ni 88.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukiukwa kwa taratibu katika uendeshaji wa zoezi la ubomoaji Serikali iligharamia kiasi cha jumla ya shilingi 1,760,000,000/- kwa wananchi 88 walioathirika na zoezi hilo. Kila mwananchi ambaye nyumba yake ilibomolewa alilipwa kiasi cha shilingi milioni 20,000,000 kama fidia.

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI: Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri katika jibu lake la msingi kwamba Serikali ilitumia shilingi bilioni 1.76 kama fidia ya wananchi waliovunjiwa nyumba zao pale Tabata Dampo. Je, fedha hizi zilizotumika katika malipo hayo zilitokana na mfuko upi?

Pili, Je, ni nani au ni chombo gani kilichoidhinisha matumizi ya pesa hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili lilipojitokeza hapa Serikali ilibidi iingilie kati kwa maana ya kuhakikisha kwamba kuhakikisha kwamba wananchi wale waliopata bugudha ile wanatendewa haki. Kilichofanyika hapa ni busara kutumika kuona kwamba hawa wananchi wanalipwa hizo milioni 20 ambazo zilikuwa zimekuja katika utaratibu wa dharura.

Kuhusu kibali kwamba kilitoka wapi? kilitoka Serikalini.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuulizwa swalii moja ya nyongeza. Katika hali ya kawaida mahali popote wanapoishi watu nyumba zao huwa hazilingani ama kwa ukubwa ama kwa *quality* ya nyumba zenye. Hivi ni sababu gani ambayo Serikali kila inapowalipa watu ikawa ina *flat rate* ya kuwalipa watu bila ya kuangalia wengine walitumia gharama kubwa kujenga nyumba hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoleza hakuna kigezo chochote kilichotumika katika kuziangalia zile nyumba. Kilichotokea ni kwamba kulikuwepo na kero imetokea pale na ilipotokea pale Serikali iliona itumie busara yake walau kuiondoa kero hiyo kwa maana ya kulipa milioni 20 kwa kila nyumba. Kwa maana hii anayoizungumzia Mheshimiwa Khalifa kama tukeenda tukapima na kuangalia hali halisi na kigezo tukasema kwamba ni thamani ya nyumba pale ni kweli kabisa kwamba wananchi wengi wangepata kiasi kidogo sana kitu ambacho kwa kweli kisingelingana na aina ya kero ambayo ilijitokeza pale.

Na. 31

Mpaka Halisi wa Wilaya za Korogwe na Lushoto

MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA aliuliza:-

Je, mpaka wa uhakika kati ya Wilaya ya Korogwe na Wilaya ya Lushoto katika eneo la Mombo ni upi na unabainishwa na alama zipi za asili au *beacons* zipi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kati ya Wilaya za Korogwe na Lushoto katika eneo la Mombo unabainishwa katika Tangazo la Serikali Na. 34 la tarehe 13. 2. 1948 ambalo lilitangaza mgawanyo wa Wilaya ya Handeni kuwa na Wilaya za Handeni na Korogwe. Pia lilitangaza mgawanyo wa Wilaya ya Korogwe kuwa na Wilaya ya Korogwe na Lushoto. Serikali imekuwa ikitumia tangazo la Serikali ambalo limekuwa likitumika kueleza mpaka huo kwa kutumia Mlima wa Mitanga, mpaka wa Hifadhi ya Msitu wa Shume- Magamba, Mlima Vumba, Ncha ya Kaskazini ya mpaka wa shamba lenye Namba *L.O. 12141*, makutano ya kijito kinachopita eneo hilo na Mto Mzimui, *Survey Beacon*, Kilima kilichopo nusu maili Mashariki mwa Kiwanja cha Korona (*Sisal Factory*) kilichopo maili mbili na robo tatu kusini mwa Mombo na Mlima Kilanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, tangazo namba 34 la tarehe 13/2/1948 limekuwa likitumika kuelekeza mpaka wa Wilaya za Korogwe na Lushoto. Sababu za kufanya hivyo ni kwanza tangazo hili linakidhi mahitaji ya sasa ya kutoa maelezo ya mpaka wa Wilaya hizo. Hata hivyo mchakato wa kuandaa maelezo rasmi ya mpaka wa Wilaya za Korogwe na Lushoto hivi sasa unaendelea. Namwomba Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama avute subira, kwani Serikali imedhamiria kukamilisha kazi hii mapema iwezekanavyo.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza je, Serikali inawahkikisha wakazi wa Lushoto kwamba mpaka huo wa mwaka 1948 haujafanyiwa marekebisho yoyote hadi leo?

Je, Serikali ipo tayari kuweka nguzo za zege katika maeneo ya utata kama vile eneo lile la Mombo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama nilivyoeleza katika jibu hili napenda nikiri kwamba *concern* yake ni kubwa sana kwa sababu unapozungumza kijito kinachopita kinaweza kikakauka kesho asubihi ukaamka ukakuta hakipo pale. Kwa hiyo mpaka huu si mpaka ambao unaweza ukasema ni reliable. Majibu haya yalitokana na swali la msingi kwa sababu alitaka kujua ile mipaka ya asili ambayo iko pale. Lakini hata hivyo nakubaliana naye kwamba sasa kazi hii inafanyika na

tunawasiliana na Wizara ya Ardhi kwa maana ya kuweka *beacons* ambazo ni za kudumu ambazo hazitakuwa hizi tunazozizungumzaia *GN* na Serikali.

Na. 32

Mpango wa Kuboresha Mazingira Nchini

MHE. ELIETTA N. SWITI aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekwisha amua kupambana na hali mbaya ya mazingira nchini:-

- (a) Je, ni fedha kiasi gani zimepelekwa Mkoani Rukwa kwa madhumuni ya kuboresha mazingira tangu wito huo ulipotolewa?
- (b) Je, Serikali inaweza kutoa taarifa ya ubora wa mazingira hususan upandaji wa miti katika Wilaya za Nkasi, Manispaa ya Sumbawanga na Sumbawanga Vijijini?
- (c) Je, Serikali haioni kuwa ipo sababu ya kuongeza motisha ya upandaji miti na udhibiti uchomajji moto ili kuboresha na kuepuka athari zinazotokana na nyumba kuezuliwa na upepo?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Elietta Namdumpe Switi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Tangu Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji uliopitishwa Aprili 2006 miradi kadhaa imeanza kutekelezwa. Miradi mitatu inatekelezwa katika Mkoa wa Rukwa chini ya ufadhili wa Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (*UNDP*). Miradi hiyo ni:-

Hifadhi ya Mazingira kuititia Ufugaji wa Nyuki (*Conservation Through Beekeeping*) unaotekelawa katika Wilaya ya Mpanda kwa gharama ya shilingi 39,544,000/-. Mradi huu unatekelezwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali linaloitwa Mimaki.

Hifadhi ya Msitu wa Mbizi unaotekelawa na Shirika la Rukwa *Environmental Youth Organisation* kwa gharama ya shilingi 29,000,000/-.

Skimu ya Usambazaji wa Maji, Mbizi (*Mbizi Water Supply Scheme*). Mradi huu unatekelezwa na Manispaa ya Sumbawanga kwa gharama ya shilingi 38,200,000/-.

Katika mwaka huu wa fedha 2008/2009 Miradi ifuatayo imetengewa fedha:-

Shilingi 198,000,000/- za mradi wa usimamizi Shirikishi wa Misitu (*Participatory Forestry Management*). Shilingi 110,510,000/- za Programu ya Maendeleo na Usimamizi wa Mazingira Mijini. (*Urban Development and Environment Management*).

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia Novemba 2007 hadi Mei 2008 Wilaya ya Nkasi ilipanga miti 632,500 na Wilaya ya Sumbawanga miti 731,100. Katika kipindi hicho Manispaa ya Sumbawanga ilipanda miti 532,100 Hata hivyo idadi ya miti iliyopandwa ni ndogo ukilinganisha na lengo la miti milioni 1.5 kwa Wilaya kwa mwaka lililowekwa katika Mkakati.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza hamasa kwa jamii katika utunzaji wa mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais imekamilisha maandalizi ya Tuzo ya Rais ya kutunza Vyano vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti. Tuzo itaongeza ufahamu wa wananchi kuhusu hifadhi na utunzaji wa mazingira. Tuzo itatolewa kwa mara ya kwanza tarehe 5 Juni, 2009 na itakuwa inatolewa kila baada ya miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Ofisi yangu iliomba na kukubvaliwa kupatiwa namba ya kifungu maalum kwa ajili ya masuala ya mazingira kuanzia mwaka huu wa fedha 2008/2009. Kifungu kinahusu Bajeti za Wizara zote na Serikali za Mitaa. Pamoja na hili masuala ya mazingira na gharama zake yamehuishwa katika programu na miradi mbalimbali ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa tathmini ya athari kwa mazingira. Hivyo basi fedha za kuboresha mazingira katika Mkoa wa Rukwa ni nyingi zaidi ya zile nilizozitaja.

MHE. ELIETTA N. SWITI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Rukwa ni Mkubwa na mahali pengi panahitaji kupandwa miti. Je Serikali haioni kwamba iko sababu ya kuongeza kasi ya upandaji miti; kwa mfano kwa Mheshimiwa Dr. Mzindakaya?

Swali la pili, kwa kuwa uchomaji wa moto na ukataji miti katika Mkoa wa Rukwa unatisha ingawaje umekwisha jibowi vizuri sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je, Serikali haioni kwamba ipo sababu ya kutafuta namna nyingine au kutunga Sheria ambayo itawakaba kabisa hawa wachomaji miti na wakataji?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana naye kwamba kuna haja ya kuongeza nguvu katika suala zima la hifadhi ya mazingira hasa upandaji miti na nashukuru kwamba kwa kweli Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa ni mashahidi lakini vile vile ni wasimamizi wakubwa kwa sababu ni wao waliochochea hata kuwa na mwaka wa mazingira katika Mkoa wa Rukwa. Kwa hiyo, naomba tuendelee kushirikiana Halmashauri pamoja na Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla katika kuongeza kasi katika utunzaji wa mazingira.

Kuhusu uchomaji moto, swali hili limejibowi vizuri sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa kama Mheshimiwa Waziri Mkuu amejibu, Waziri hawezi akaongezea.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika Mkoa wa Rukwa Halmashauri zetu huwa wanauza ile miche ya miti kwa bei kubwa. Je, Serikali isingeona ni vizuri miche ile ikatolewa au kwa bei ya chini sana kwa maana kwamba wananchi wengi wameshahamasika kupanda lakini wanashindwa kununua kwa sababu bei yake ni kubwa?

NAIBU SPIKA: Serikali Halmashauri au ipi?

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Serikali inayotoa fedha kuitia Halmashauri. (*Kicheko*)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kitu chochote bure kinaonekana kama hakina thamani. Kwa hiyo nakubaliana naye kwamba angalau bei ingepungua lakini si kutoa bure kwa sababu hakitathaminiwa na suala kubwa ambalo ningependa kusisitiza si kupanda miti tu lakini vile vile kutunza miti. Kuhusu ipunguke bei kiasi gani basi angeweza kutusaidia katika Halmashauri yake wapunguze bei ili wananchi waweze kupata miche kwa urahisi ili kuendelea kutunza mazingira.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, kama sikusahau nakumbuka kabisa wewe uliongoza Kamati ya Wabunge kuja kule Mpanda na mlipata bahati ya kutembelea makazi ya wakimbizi ya Katumba. Uharibifu uliofanywa na wakimbizi katika makazi ya Katumba ni wa kutisha. Jumuiya ya Kimataifa haionyeshi dalili zozote za kusaidia kurekebisha uhalibifu uliofanywa na wakimbizi katika makazi hayo. Sasa Serikali inasema nini kuhusu kurekebisha dosari zilizotokana na athari ya kuwepo wakimbizi kule Mpanda?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uharibifu wa mazingira kutohana na kuwepo na wakimbizi nchini si suala la Mpanda tu lakini ni maeneo mengi hasa maeneo ya Magharibi mwa nchi yetu. Tumepata misaada mbalimbali kutoka kwa wahisani kuweza kurekebisha mazingira au kushughulikia hili suala.

Lakini ufumbuzi wa suala hili kwa kweli ni kutokuwa na wakimbizi na suala hili linashughulikiwa na wenzetu wa Mambo ya Ndani basi matumaini yetu ni kwamba Kambi ya Katumba haitakuwa kambi ya kudumu milele na uoto wa asili utarudi pale ambapo hawa hawataendelea kuwa wakimbizi watarudi makwao na wale ambao watabakia nchini basi watakuwa ni raia wa kawaida kwa taratibu na sheria za nchi yetu.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Musa Azzan Zungu, kwa swali linalofuata.

MHE. MUSA AZZAN ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili Namba 33 lilipata majibu Bunge lililopita naomba lifutwe.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 34

Kurekebisha Sheria ya Umiliki wa Ardhi

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA aliuliza:-

Kwa kwa Sheria ya sasa ya umilikaji wa ardhi inatoa nafasi kwa mwekezaji wa nje kumiliki ardhi kwa miaka 99.

- (a) Je, Serikali haioni kuwa Sheria hiyo ina kasoro kwa sababu inawanyima haki wananchi ambao wanakosa nafasi ya kulima kwani wanatakiwa kupisha ardhi husika kwa wawekezaji?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kubadilisha Sheria hiyo ili mwekezaji wa nje alazimike kushirikiana na wananchi katika kupata na kutumia ardhi hiyo?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria yetu ya ardhi inakata wageni wasimilikishwe ardhi isipokuwa wawekezaji wenyewe Hati ya Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (*TIC*). Mwekezajia anapohitaji ardhi ya kijiji Sheria ya Ardhi ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 inataka apeleke ombi kwenye Serikali ya Kijiji husika. Ombi hilo kwa mujibu wa Sheria linajadiliwa na Mkutano Mkuu wa Wanakiji wote, iwapo wana ardhi ya ziada kutokana na mpango wa matumizi ya ardhi wanaweza kupendekeza apewe ardhi.

Pendekezo hili hupitia katika vikao vya Halmashauri, Ofisi ya Waziri na hatimaye Mheshimiwa Rais ndiye mwenye madaraka ya mwisho ya kuruhusu ardhi ya kijiji imegwe na kupewa mwekezaji kwa utaratibu wa kumpangisha kwa muda yaani *lease* na siyo inakuwa mali yake ya kudumu.

Hivyo siyo kweli kwamba Sheria ya kuwamilikisha ardhi wawekezaji wa kutoka nje ya nchi kwa miaka 99 inawanyima haki wanavijiji kwa kukosa nafasi ya kulima. Kama kijiji kina tatizo la uhaba wa ardhi hawawezi kupendekeza mwekezaji apewe ardhi.

- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kufanya marekebisheshi Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 kwa kuwa haki za wananchi kumiliki ardhi zimezingatiwa kwenye Sheria hiyo. Pia, haki za wananchi kumiliki ardhi zimezingatiwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999, ambayo umiliki

wa ardhi kwa Wanavijiji hauna ukomo. Kwa ujumla Sheria za Ardhi hazizuii ushirikiano kati ya wananchi na wawekezaji katika kuomba na kupatiwa ardhi.

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na kwamba Mwekezaji anapitia TIC na ombi lake kujadiliwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji, lakini bado ukweli upo pale pale kwamba mwekezaji huyu anaweza akamilikishwa miaka 99. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kupunguza miaka ya umilikaji wa ardhi hii kuanzia kati ya miaka 20 hadi 30 na wasiozidi kupewa hekta 500 ili kupunguza hatari ya ardhi hapo baadae kumilikiwa na wageni?

La pili, ili kujenga mazingira mazuri ya kuleta maisha bora kwa kila mtanzania je, Serikali haioni kuwa kuna haja kubwa ya kubadilisha Sheria ya Ardhi ili kuwawezesha wanakiji kuwa na hisa katika mradi huo mkubwa unaoletwa na mwekezaji hasa kwa kuzingatia kwamba ardhi ni mali?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba hii miradi ya kilimo anayewekeza kwenye kilimo hutegemea anataka ile ardhi kuitumia kwa shughuli ipi. Sasa ukisema tu heka 500 na yeye anataka kuwekeza katika shamba la miwa kubwa ili kulisha kiwanda kikubwa.

Kwa hiyo, ukubwa wa ardhi unategemea na ukubwa wa mradi anaoutaka na mara nyingi miradi ya kilimo huwezi kuwekeza leo kesho ukaanza kupata faida. Inachukua muda mrefu mpaka arejeshe fedha alizotumia ndipo aanze kupata faida. Ndiyo maana hata muda wa ile *lease* unakuwa ni mrefu.

Lakini kwa vyovypote vile huyu tunampa *lease* baada ya muda kwisha ardhi inarudi tena kuwa ya umma. Kuna nchi nyingine inakuwa ukishampa hivi inakuwa ardhi ni yake milele. Sisi Sheria yetu inasema hapana tunampangisha baada ya muda kwisha inarudi tena mikononi mwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, sasa hivi Sheria haikatazi wanakijiji kuingia ubia na mwekezaji katika mradi pale kijijini. Kwa hiyo, hatuoni sababu ya kuibadilisha kwa sababu hiyo ruksa ipo tayari wanaweza wakafanya hivyo.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana kati ya wawekazaji na wananchi kuhusiana na masuala ya ardhi.

Mfano dhahiri ni ardhi ya Kawanga katika Kata ya Hunyari katika Wilaya Bunda kati ya mwekezaji wa VIP na wananchi wa vijiji vilivyopo katika Kata hiyo. Serikali inasema nini kuhusiana na mgogoro huo wa ardhi ya Kawanga kule Bunda.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Naibu Spika, huu mgogoro wa kijiji cha Kawanga ndiyo sasa hivi mimi nausikia kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge atuletee rasmi kwenye Wizara na mimi naahidi kwamba tutaushughulikia kwa kushirikiana na Halmashauri inayohusika.

Na. 35

Uhaba wa Ardhi kwa Wananchi wa Karagwe

MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. GOSBERT B. BLANDES)
aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi Wilayani Karagwe wanakabiliwa na tatizo la uhaba wa ardhi na kwamba hawajui ni utaratibu upi unaostahili kufuatwa katika kuomba ardhi ya kijiji:-

- (a) Je, Serikali iko tayari kutoa utaratibu wa kuomba ardhi ya kijiji?
- (b) Je, malalamiko yanayohusu ardhi ya vijiji hupelekwa katika vyombo gani?
- (c) Je, ni nani mmiliki wa vyombo hivyo?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuomba ardhi katika kijiji umeainishwa katika Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999. Kwa mujibu wa Sheria hii, maombi ya ardhi katika kijiji yanatakiwa kuwasilishwa katika Halmashauri ya kijiji husika. Serikali ya kijiji baada ya kupokea maombi hayo inatakiwa kuyajadili na kupendekeza au kutopendekeza kutolewa kwa ardhi ya kijiji.

Mapendekezo hayo yanatkiwa kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa kijiji (*Village Assembly*) ambao ndio wenyewe mamlaka ya mwisho ya kukubali au kukataa maombi ya kutolewa kwa ardhi ya kijiji. Utaratibu huo unatumika pale ambapo mwombaji ni mkazi wa kijiji husika au ni kikundi cha wakazi wa kijiji husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo maombi ya ardhi yanafanywa na kijiji kwa kijiji kingine ndani au nje ya Wilaya, kikundi cha wanakijiji kilichoteuliwa kwa niaba ya Halmashauri ya kijiji na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa kijiji kitawasilisha maombi yao katika Halmashauri ya kijiji ambacho kinaonekana kuwa kina ardhi ya ziada. Kijiji hiki chenye ardhi ya ziada kitatakiwa kufuata utaratibu ulioelezwa hapo juu katika kutoa uamuzi wa ombi la ardhi. Ushauri na maoni ya Halmashauri ya Wilaya ni muhimu kuzingatiwa na kijiji katika kutoa uamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maombi ya ardhi ya kijiji ya wawekezaji wa nje, Sera ya Taifa ya Ardhi inaelekeza kuwa watu wasio raia na makampuni ya kigeni hawataruhusiwa kupata ardhi inayomilikiwa kimila hata kama ni kununua. Maombi yao lazima kwanza yapitie kwenye Kituo cha Uwekezaji (*TIC*).

Hata hivyo, maombi ya ardhi kwas ajili ya wawekezaji ambao ni raia na iwapo eneo linalotakiwa ni kubwa, kijiji husika kinatakiwa kuandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji (*Village Land Use Plan*). Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi utabainisha mahitaji ya ardhi ya kijiji ya sasa na ya baadaye.

Aidha, kutokana na mpango huo itabainika iwapo kijiji kinayo ardhi ya ziada itakayotolewa kwa wawekezaji. Pale ambapo kijiji kitaridhika kuwa kinayo ardhi ya ziada na kuridhia kuitoa kwa wawekezaji, utaratibu wa kubadilisha ardhi ya kijiji kuwa ardhi ya kawaida (kuhawilisha) utafanyika. Mapendekezo ya kuhawilisha ardhi huanzia katika ngazi ya kijiji, Wilaya, Wizara ya Ardhi na hatimaye Rais ndiye mwenye mamlaka ya mwisho ya kubadilisha ardhi ya kijiji kuwa ardhi ya kawaida na akapewa mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusuluuhisha na kuamua migogoro ya ardhi, Sheria za Ardhi Na. 4 na Na. 5 za mwaka 1999 zimetaja vyombo vitakavyohusika katika utatuza wa migogoro ya madai ya ardhi. Vyombo hivi ni:- Baraza la Ardhi ya Vijiji, Baraza la Kata, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Mahakama Kuu (Kitengo cha Ardhi) na Mahakama ya Rufaa.

Vyombo hivi vimepewa mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya kutatua migogoro ya Ardhi na vilianza kushughulikia migogoro hiyo tangu tarehe 1 Oktoba, 2003.

Kuhusu nani anasimamia vyombo hivi, ni kwamba, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Mabaraza ya Kata yapo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yapo chini ya Wizara

ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mahakama Kuu (Kitengo cha Ardhi) na Mahakama ya Rufaa zipo chini ya Idara ya Mahakama katika Wizara ya Katiba na Sheria.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, suala la ardhi linahusiana na suala nyumba; kwa kuwa umiliki wa nyumba, wananchi wengi wanapenda sana kufanya hivyo, lakini wanashindwa kwa sababu ya vituo hivi vya kumiliki ni mpaka Wizarani ama Kanda na wananchi wengi hawana fedha.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami sasa ili kuwapunguzia wananchi mzigo na wananchi wengi waweze kumiliki nyumba zao, kwa maana ya kuwa na Hati, ni vema sasa huduma hii ikapelekwa Mikoani?

NAIBU SPIKA: Yaani huduma ya kutoa Hati! Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba yangu ya bajeti ambayo nilitoa katika Bunge lililokwisha, nilieleza na leo nataka nirudie tena kwa manufaa ya Watanzania wote kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2008, utaratibu wa kutoa hati kwanza unaanza kwenye Halmashauri ya Wilaya inayohusika. Ikishakamilika, zamani ile hati ilikuwa inaletwa Wizarani kutiwa saini.

Lakini kuanzia tarehe 1 Julai, 2008, hii huduma sasa inatolewa huku huku Mikoani kupitia Ofisi Tano za Kanda ambazo tumeishazianzisha na tumeishateua tayari Makamishina wa Ardhi Wasaidizi katika hizo Kanda Tano. Kwa hiyo, kazi sasa itaishia huku huku Mikoani, haitakuja Wizarani. (*Makofi*)

Kupanda kwa Bei za Mazao ya Nafaka

MHE. ALI JUMA HAJI aliuliza:-

Kwa kuwa bei za mazao hasa ya nafaka katika Soko la Dunia zinazidi kupanda na kusababisha mfumuko wa bei za vyakula; na kwa kuwa nchi za Afrika ni waagizaji wakubwa wa mazao hayo kuliko kusafirisha:-

- (a) Je, Serikali imejiandaa vipi kupitia kwa wakulima katika kukabiliana na janga hilo?
- (b) Je, Serikali imetoa msukumo gani kwa Mikoa au Wilaya zilizokumbwa na janga la njaa siku za nyuma, hasa katika kutoa pembejeo mbali mbali ili janga hili lisiwatokee tena?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mbunge wa Jimbo la Chaani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Katika kukabiliana na kupanda kwa bei za chakula hasa nafaka duniani, Serikali imejiandaa kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa kufanya yafuatayo:-
 - (i) Kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea na mbegu ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya nafaka kwa eneo.
 - (ii) Kuimarisha huduma za ugani ili kuwaelimisha wakulima mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya nafaka.
 - (iii) Kupanua kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na athari za mvua zisizo na uhakika.
 - (iv) Kuhamasisha wakulima kulima mazao kulingana na hali ya hewa ya eneo husika.
 - (v) Kuongeza matumizi ya zana bora katika kilimo.
 - (vi) Kuongeza uwezo wa Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa wa kununua nafaka kwa wingi kutoka kwa wakulima ili kuwatia moyo kuzalisha zaidi.
- (b) Katika kukabiliana na janga la njaa, Serikali imeendelea kutoa msaada wa mbegu za mahindi, mtama, mpunga na maharage kwa wakulima walioathirika na upungufu wa chakula. Mathalani, katika Msimu wa 2005/2006, jumla ya tani 1,367 za

mbegu za nafaka na mikunde zilitolewa katika Mikoa ya Arusha, Pwani, Dodoma, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mwanza, Shinyanga, Singida, Tabora, Mbeya, Morogoro, Mtwara na Tanga. Katika Msimu wa 2006/2007, tani 1,215 za mbegu za msaada zilisambazwa katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Singida, Tabora, Mbeya, Arusha, Iringa, Lindi, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Unguja na Pemba.

Shabaha ya Mpango huu ni kuiwezesha Mikoa yenyе upungufu wa chakula, kulima mazao yanayostahimili ukame. Aidha, katika Mikoa ambayo haikupata mavuno kwa kiwango cha kuridhisha, imepewa kipaumbele kwa kupewa mbolea na mbegu za ruzuku ili kuongeza uzalishaji wa mazao hususani mahindi na mpunga.

MHE. ALI JUMA HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo ni marefu kidogo, lakini, naomba kumwuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake alisema kwamba ataimarisha huduma za ugani ili kuwaelimisha wakulima wetu mbinu bora za uzalishaji wa mazao.

Je, kwa nini Serikali hadi sasa haijajikita katika kuwaelimisha wakulima wetu mbinu bora ya kuhifadhi mazao haya hasa ya chakula kule vijijini ili likitokea janga la njaa liweze kuwasaidia wao kwanza kule wenyewe badala ya kutegemea Hifadhi ya Taifa na misaada kutoka Serikali Kuu au nchi za nje?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuongeza idadi ya Wagani ili huduma hiyo iweze kufika. Kwa mfano, katika mwaka huu wa fedha tunasambaza Wagani 1250 katika eneo ambalo wamefuzu mafunzo yao Vyuo vya Kilimo.

Lakini vile vile kuhusu huduma ya kuwafundisha wananchi juu ya Hifadhi ya mazao, shughuli hiyo inaendelea katika ngazi ya Halmashauri, kuwaelimisha namna ya kuhifadhi na vile vile kuwaelimisha wasiuze chakula chote ili wasije wakajikuta wana njaa wakati wao walikuwa na chakula kingi.

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Mkutano wa *IPU* uliofanyika kule Geneva, Uswiss mwezi wa Kumi, ajenda muhimu au mahususi iliyozungmzwa ilikuwa ni *Global Food Crisis* yaani Mgogoro wa chakula hapa Duniani. Na kwa kuwa ilionekana dhahiri kwamba nchi zinazoendelea hususan Africa, South of Sahara ikiwemo Tanzania, zitaathirika sana kwa tatizo hilo.

Je, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ina mikakati gani madhubuti kuhakikisha kwamba Tanzania pamoja na kwamba iko Kusini mwa Jangwa la Sahara, haitaathirika sana na tatizo hilo la chakula Duniani?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoleza katika jibu la msingi, ziko hatua mbali mbali ambazo tunazichukua, lakini zote zinalenga katika kuongeza uzalishaji wa chakula. Sisi kama nchi maskini hatuwezi kutegemea kununua chakula. Kutegemea kununua chakula wakati bei za vyakula Duniani zimepanda ni jambo ambalo linaweza kutuathiri.

Kwa hiyo, namna peke yake ambayo tunaweza kujisaidia, ni kuweka mkakati ambao unawezesha wakulima wetu kuzalisha ziada ili itutosheleze wenywewe na ikibidi tuweze kuuza nje na kujipatia mapato zaidi yanayotokana na kupanda kwa bei yamazao hayo Duniani. Huo ndio mfumo ambao tunautumia na tunadhani ndio mkakati ambao unaweza kutusaidia zaidi.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuiliza swalii moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa moja ya mkakati wa kupunguza matatizo ya upungufu wa chakula ni kuingia katika Mkakati wa *Contract Farming* (Ulimaji wa Mashamba Makubwa); na kwa kuwa kwa maelezo ya Waziri wa Ardhi, inaonekana waziri kwamba vipo vipengele vingi kwa watu kupata ardhi hasa kwa upande wa uwekezaji na hata kwa upande wa vijijini.

Je, Waziri wa Kilimo anaweza kukaa na Waziri wa Ardhi wakaona ni Sheria gani zinaweza kurekebishwa ili kuharakisha *Contract Farming* kufanyika bila ya kuwa na urasimu mkubwa na kuwaondoa wawekezaji wengine katika kilimo cha chakula?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunashirikiana na Wizara ya Ardhi na vile vile Wizara ya Kilimo inacho Kikosi cha Hifadhi ya Ardhi ambacho kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji pamoja na Wizara ya Ardhi tunaanzisha Mkakati wa Kupima maeneo ambayo yataweza kutumiwa na wawekezaji wakubwa kwa ajili ya Kilimo cha Mkataba (*Contract Farming*) katika maeneo mbali mbali nchini. Hiyo ni sehemu moja wapo katika Mkakati wa kuongeza uzalishaji wa chakula.

Lakini, kama alivyoleza Waziri wa Ardhi sasa hivi, ni suala vile vile la ardhi na makubaliano baina ya ardhi ya vijiji na wawekezaji. Kwa hiyo, hakuna namna tunaweza kufanya kwa mkato. Kwa mfano, wako wawekezaji ambao tayari wana *interest*, lakini inabidi tuwapatie ardhi chini ya utaratibuwa *TIC*, ardhi ya akiba ambayo ndiyo itakayopimwa na Serikali na hatimaye waweze kupewa wawekezaji wanaihusika.

Na. 37

Kuendeleza Kilimo cha Michikichi Kigoma

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO (K.n.y. MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI aliuliza:-

- (a) Serikali iko tayari kuwa na mpango maalum wa kuendeleza kilimo cha Michikichi Mkoani Kigoma?
- (b) Je, Serikali inafahamu kuwa kilimo hiki kinaweza kuokoa fedha nyingi zinazotumika kuagiza mafuata nchi za nje na kuongeza ajira kwa wananchi?
- (c) Je, ni mafuta ghafi kiasi gani yanayoingizwa nchini na yanatoka nchi zipi?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, yenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiendeleza kilimo cha mchikichi Mkoani Kigoma. Kuanzia msimu wa mwaka 1987/1988, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa Kigoma na Wadau wengine imeweza kuingiza miche chotara (*Pre-germinate Hybrid Seeds*) 605,000 kutoka *Costa Rica, Ivory Coast* na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Aidha, mwaka 1999 Taasisi isiyokuwa ya Kiserikali *TACARE* ikisaidiana na *UNDP* ilianzisha mradi wa kusambaza mbegu na jumla ya miche 136,000 ilisambazwa kwa wakulima. Baada ya kipindi cha mradi huo kumalizika, Taasisi ya *TACARE* imeendelea kusambaza miche bora kati ya 100,000 – 250,000 kwa wakulima kila mwaka.

Aidha, kupitia Mpango wa ASDP mwaka 2008/2009 katika Halmashauri ya Kigoma itapandwa miche 25,000 katika vijiji vinne vya Ilagala, Matendo, Kalenge na Nyanganga na sh. 8,580,000 zitatumika katika kuboresha usindikaji wa mawese katika vijiji vya Bubango na Ipagala na Sh. 10,000,000 zitatumika kununulia mashine ya kusindika mafuta (*mise*) huko Nkokwa.

(b) Serikali inatambua umuhimu wa mchango mkubwa unaoweza kupatikana kwa kuendeleza kilimo cha michikichi hapa nchini hususan katika kuokoa fedha nyingi zinazotumika kuagiza mafuta kutoka nchi za nje.

(c) Kwa kiwango kikubwa mali ghafi ya mafuta yanayoingizwa hapa nchini yanaagizwa toka nchi mbali mbali duniani. Miongoni mwa nchi hizo ni pamoja na:-

Malaysia, Indonesia, Ujerumani, Marekani, Singapore, Afrika Kusini, Kenya na Uingereza. Kulingana na takwimu toka Mamlaka ya Mapato (*Tanzania Revenue Authority (TRA)* kiasi cha mafuta ghafi yaliyoingizwa nchini katika kipindi cha miaka minne iliyopita ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2004 Tani 13,507.40, Mwaka 2005 Tani 134,967.80, Mwaka 2006 Tani 175,368.50, Mwaka 2007 Tani 23,429.80.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika. Nina swali dogo tu la nyongeza. Mwuliza swali katika kipengele (a) alitaka kujua mpango maalum.

Ni kweli kumekuwa na *projects* mbali mbali chini ya *ASDP*, kumekuwa na *NGOs* zinafanya kazi pamoja na *TANCARE*.

Lakini nafikiri hapa hoja ya msingi aliyotaka kuuliza Mheshimiwa Mporogomyi ni lini Serikali sasa kupitia Wizara ya Kilimo itakuwa na *A National Project* ya Michikichi katika Mkoa wa Kigoma ambao una historia ya michikichi hiyo pamoja na juhudhi hizo za *NGOs*, *ASDP Projects* na kadhalika?

Nadhani Mheshimiwa Waziri, hoja ya msingi sasa ni lini Wizara yako itatazama michikichi sasa *as a National Project* katika Mkoa wa Kigoma, ndiyo ilikuwa hoja ya msingi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, hatujatengeneza *National Programme*, lakini nadhani kuna umuhimu wa kukaa na kushirikiana na viongozi wa Mkoa wa Kigoma ili kuandaa mpango wa namna hiyo.

Lakini hata kabla hatujafikia hapo, fedha zinazopelekwa Mikoani kwa ajili ya kusaidia kilimo zinaweza zikasaidia sana katika kuhakikisha kwamba wakulima wanapata miche mingi ili waanze kupanda. Huo ni mkakati mmoja.

Lakini mkakati mwingine ni ile *Contract Farming*, kwa sababu unaweza kueneza michikichi lakini unahitaji soko vile vile. Sasa tunao watu ambao wako tayari kwenda Kigoma chini ya mpango wa uwekezaji.

Tunachoweza kufanya ni kushirikiana na Mkoa wa Kigoma ili wakati tunawasaidia wakulima wadogo kueneza na kuongeza uzalishaji wa michikichi, wakulima wakubwa wanaotaka kwenda kulima kule na kuweka viwanda waweze kuwa soko ili uzalishaji wa wakulima wadogo usaidiwe na wakulima wakubwa chini ya

Contacting Farming. Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Mkoa wsa Kigoma kwa kazi hiyo.

Nchi za Kiafrika Kutawaliwa Tena

MHE. AME PANDU AME aliuliza:-

Kwa kuwa kuna nchi hapa Barani Afrika ambazo wakati wa kufanya uchaguzi lazima zipate uangalizi kutoka Mataifa ya nje kwa kisingizio cha demokrasia:-

- (a) Je, hiyo siyo dalili ya kuwa Bara la Afrika linaweza kutawaliwa tena?
- (b) Je, Umoja wa Nchi za Kiafrika unachukua hatua gani kukabiliana na hali hiyo?
- (c) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa kuhakikisha kwamba waangalizi wa Kimataifa hawaingiliii siasa na taratibu za nchi za Kiafrika?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA): alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi si lazima nchi inayofanya uchaguzi iwe na waangalizi kutoka nje. Suala la kuwaalika ama kutokuwaalika waangalizi kutoka nje kushuhudia uchaguzi ni uamuzi wa nchi inayohusika. Aidha, suala la kuwa na waangalizi wa Kimataifa kushuhudia uchaguzi katika nchi mbali mbali linatokana na Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kama njia ya kuongeza uwazi na demokrasia katika uchaguzi katika nchi mbali mbali ulimwenguni. Hivyo, dhana kuwa waangalizi wa uchaguzi kutoka nje ni dalili kuwa Bara letu linaweza kutawaliwa tena si sahihi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Nchi za Kiafrika (*AU*) unaunga mkono kwa dhati Azimio hilo na utaratibu wa kupeleka waangalizi wa uchaguzi. Hivyo, Umoja huo huwa unapeleka waangalizi wake kushuhudia uchaguzi kwenye nchi mbali mbali pale unapoalikwa kufanya hivyo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, waangalizi hawatakiwi kuingilia siasa na taratibu za nchi zinzofanya uchaguzi. Waangalizi hao wanatakiwa kushuhudia tu kama taratibu na kanuni zilizopo za kuendesha chaguzi kwa njia za kidemokrasia zinafuatwa na kisha kutoa tathmini yao baada ya uchaguzi. Ikiwa waangalizi watafanya kazi yao kwa umakini, ushuhuda wao unaweza kusaidia kupunguza malalamiko ya ukiukwaji wa taratibu zilizopo na kuhakikisha uchaguzi ulikuwa huru na wa haki.

MHE. AME PANDU AME: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa nchi zetu zilipata uhuru

wake kutoka mikononi mwa wakoloni. Je, ni kipi kinachopelekea sasa nchi hizi zinapofanya chaguzi kuu kupata shinikizo kubwa la kisiasa kutoka nchi kubwa Duniani?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba nia kubwa ya kuwepo na waangalizi ni kuona uchaguzi unakuwa huru, wa haki na wa kidemokrasia. Lakini si kwamba wanakuja kutoa shinikizo la namna ya kufanya uchaguzi. Ile ni kuwaalika kwa sababu huona Maendeleo ya uchaguzi na kutoa mapendekezo yao kwa nia ya kuwepo uhuru katika kufanya uchaguzi.

Na. 39

Utoaji wa Visa Katika Balozi za Tanzania

MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA) aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu ina vivutio vingi vya utalii na watalii wengi toka pande zote za Dunia hupenda kuja Tanzania; na kwa kuwa wanahitaji *Visa* ili waweze kuja:-

- (a) Je, ni Balozi zipi za Tanzania ambazo hazina tovuti?
- (b) Je, ni maduhuli kiasi gani yamepatikana toka katika Balozi zetu kwa mwaka wa fedha uliopita kutohana na utoaji wa *Visa*?
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya *outsourcing* katika mchakato wa kutoa *Visa*?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA): alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi za Tanzania zisizo na tovuti ni zifuatazo:- Abuja, Addis Ababa, Bujumbura, Brussels, Harare, Kampala, Kigali, Kinshasa, Lusaka, Lilongwe, Nairobi, *Beijing, Rome, Washington D.C, New Delhi, Brasilia, Kuala Lumpur*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi za Tanzania zenye tovuti ni zifuatazo:-

Abu Dhabi, Berlin, Cairo, Geneva, Paris, London, Maputo, Moscow, Muscat, Ottawa, Tokyo, Pretoria, Riyadh, Stockholm na New York.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha shilingi 13,847,793,830.17 zilipatikana kama mapato yatokanayo na VISA kupitia katika Balozi zetu kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2007/2008.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hutoa VISA kwa wageni wanaoingia kwa kutumia njia mbili:- Njia ya kwanza ni wageni kupata VISA zao kutoka kwenye Balozi zetu na kwa Wawakilishi wa Heshima wa Tanzania walioko nje ya nchi. Njia ya pili ni kwa wageni kupata VISA kutoka kwa Maafisa wa Uhamiaji walioko Mipakani, Viwanja vya Ndege na kwenye Bandari zetu. Aidha, baadhi ya Balozi zetu hasa zenye wageni wengi wanaokuja Tanzania zina Maafisa wa Uhamiaji kwenye Balozi hizo.

Kuhusu *outsourcing* katika mchakato wa kutoa VISA nje ya nchi, pamoja na suala zima la unyeti wake na usalama wa raia wasio wa Tanzania kutoa VISA hizo, Idara ya Uhamiaji ambayo ndiyo yenye jukumu la kutoa Sera katika nyanja hii ndio wanawenza kulitolea maamuzi kwa kuishirikisha Wizara yangu.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa miji mingi ambako kuna Balozi zetu hakuna tovuti (*Website*) na ukizingatia kwamba miji hiyo ni muhimu sana, kwa mfano kuna Mji wa *Beijing, Rome, Washington D.C, New Delhi, Brasilia na Kuala Lumpur*.

Je, Serikali sasa inasema nini kuhusu kuziwekea hizo Balozi tovuti kwa maana ya kurahisisha mawasiliano? Swali la pili; suala la *outsourcing* kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake kwamba Idara ya Uhamiaji ndiyo yenye jukumu la kutoa Sera katika nyanja hii; sasa kama Serikali inaona umuhimu wa kufanya *outsourcing* kama nchi nyingine zinavyofanya kwa mfano Kenya na hili pia kwa kweli linaweza likapunguza hata gharama kwa baaddhi ya Maafisa ambao kazi yao ni kwa ajili ya kutoa VISA; Serikali itachukua hatua gani kuwasiliana na Idara ya Uhamiaji ili waone umuhimu sasa wa kufanya *outsourcing* katika suala la kutoa VISA?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA): Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tovuti, Seriikali ingependa sana Balozi zake zote ziwe na tovuti, lakini kutokana na hali ya kifedha ndiyo inayosababisha kuwa na upungufu huo. Lakini hivi sasa jitihada zinafanya kuhakikisha kwamba kila Balozi yetu inakuwa na tovuti hatua kwa hatua pale fedha zitakapopatikana. Kuhusu suala la *outsourcing*, kwa kuwa hivi sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imo katika mchakato wa suala zima la Sera ya Uhamiaji, hivyo, naomnba Mheshimiwa Mbunge avute subira, mara pale Sera hii itakapokamilika, basin a utaratibu huu utakuwa umeangaliwa inavyofaa.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kuniona. Mimi nina swali dogo tu la nyongeza. Huko nyuma Balozi zetu nyingi ambazo wananchi wao wanakuja kufanya utalii kwetu zimekuwa zikiwa na Maafisa wa Utalii (*Tourist Promotion Officers*) katika *Embassies* zetu, na utaratibu huo wengi mnaukumbuka ulifanya kazi nzuri sana kwenye miaka ya 1980/1990. Mheshimiwa Naibu

Spika, mimi nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni lini sasa Serikali itaangalia utaratibu huu wa kuanza kuwa na *Tourist Promotion Officers* katika *Embassies* zetu kama ilivyokuwa katika *Embassy* ya Japan, *Washington D.C* pale na maeneo kama Sweden miaka ile? Nadhani ulikuwa utaratibu mzuri sana na ulisaidia sana kuvutia na kuleta watalii wengi katika nchi zetu.

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, badala ya tovuti, basi tena Mabalozi!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nsanzugwako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko katika majadiliano mbalimbali kuhusu kuhakikisha kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na Balozi zetu tuweze kuweka mafisa utalii huko, kwa sasa hivi kilichopo ni kwamba katika kuwashughulikia Bajeti na pia kuwapelekea vifaa ambavyo wataweza kutumia na kwa kuanzia tutaanza na New Delhi, India ambako tayari na tovuti imeshawekwa na mimi ndiyo nilikwenda kuizundua. Pia tutaweka Maafisa Utalii Ujerumanu na pia Marekani ambako kwa kweli tumeona huko sasa hivi kumechangamka sana na tunawatalii wengi wanaotoka katika sehemu za huko.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha.

Waheshimiwa Wabunge matangazo yetu leo ni kwamba, tunao wageni hapa Bungeni, Waandishi wa Habari kutoka vyombo mbalimbali wanaohudhuria Semina ya UKIMWI hapa Dodoma, yupo Ndugu Abby Nkungu, kutoka *Daily News*, Nowadia Mtimi kutoka Uhuru na Mzalendo, yupo Bi. Elizabeth Chitenje kutoka Iringa, Lilian Lucas kutoka gazeti la Mwananchi, Latifa Ganziel kutoka radio Uhuru na Aida Mushi kutoka Nipashe, *Guardian* Morogoro, karibuni sana tumefurahi kuwaona na hasa kwa kuwa wote ni akina Dada. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wengine amba ni wanafunzi kumi kutoka taasisi ya watu wazima tawi la Dodoma wasimame, ahsante na karibuni sana, tunawatakia masomo mema elimu haina mwisho.

Waheshimiwa Wabunge matangazo ya kazi leo, kwanza kabisa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Wilson Masilingi anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake leo tarehe 30 Oktoba, 2008 saa tano asubuhi. Kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika ukumbi namba 231 ghorofa ya pili jengo la utawala.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya kudumu ya Ardhi Maliasili na Mazingira Mheshimiwa Job Ndugai anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati na Mheshimiwa Waziri wa Mali Asili na Utalii, kikao kitafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa saba mchana wajumbe wote wa Kamati mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa *TAPAC* Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o anaomba niwatangazie Wajumbe wote wa *TAPAC* kwamba kutakuwa na kikao cha wajumbe wote leo mara baada ya kuahirishwa Bunge saa saba nadhani katika ukumbi 133, Wabunge wanawake wote katika chama chao cha Tanzania *Women Parliamentary Caucaus* watakuwa na kikao kifupi leo saa saba mchana huu katika ukumbi namba 227 ghorofa ya pili natangaza mwenyekiti wake mwenyewe Anna Makinda. (*Kicheko*)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(*Kusomwa kwa Mara ya Kwanza*)

Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Miliki za Sehemu za Majengo wa Mwaka 2008, [*The Unit Titles Bill, 2008*]

Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Nyumba wa Mwaka 2008 [*The Mortgage Financing (Special Provisions) Bill, 2008*]

(*Miswada yote miwili iliyotajwa hapo juu ilisomwa kwa mara ya Kwanza*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mtaona kwamba hii ni miswada ambayo imeletwa chini ya utaratibu wa hati ya dharura, ndiyo maana mnakuta kwenye *Order Paper* inasema Miswada hii itasomwa kwa mara ya kwanza na hatua zake zote.

Lakini pia kwa sababu miswada hii inawiana sana kwa hiyo Waziri ataisoma yote kwa pamoja na kwa Mwenyekiti, Muswada wa kwanza na wa Pili utasomwa kwa pamoja kwa hiyo na Kambi ya Upinzani watatoa maoni kwa misingi hiyo, lakini katika maamuzi tutaamua muswada mmoja baada ya mwingine, ila katika kujadili tutajadili yote miwili.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Miliki za Sehemu za Majengo wa Mwaka 2008, (*The Unit Titles Bill, 2008*)

na

Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Nyumba wa Mwaka 2008 (*The Mortgage Financing (Special*

(Provisions) Bill, 2008)

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha miswada miwili hii kwa pamoja, yaani muswada wa Sheria ya Miliki ya sehemu majengo (*The unit Titles Act, 2008*) na Muswada wa sheria wa kurekebisha sheria mbali kuwezesha ardhi itumike kwa wananchi kupata mikopo katika mabenki (*The Mortgage Financing Bill, 2008*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema miswada hii ni pacha yote inazungumzia jambo hilo hilo moja na madhumuni ni mamoja ndiyo maana nitaiwasilisha yote kwa pamoja, lakini kama ulivyosema vilevile Miswada hii Mheshimiwa Rais ameruhusu tuizungumze kwa njia ya haraka na ametoa hati ya dharura kwa sababu jambo lenyewe hili ni kilio cha wananchi kwa muda mrefu kweli kwamba wanataka kujenga nyumba bora hela za mfukoni kwa ajili ya kujengea hawana, kwa hiyo utaratibu huu sasa unakuja utaratibu wa kuweza kujenga nyumba kwa kutumia mikopo, kwa hiyo tunamshukuru Rais kwa kuidhinisha jambo hili lije kwa namna hii kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa niwasilishe Muswada wa kwanza unaohusu Muswada wa Sheria ya Miliki ya sehemu za Majengo, *The Unit Titles Act, 2008*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lengo la Muswada Muswada huu unakusudia kuweka utaratibu kisheria unaolenga kuwezesha kuwepo na utaratibu wa kutoa miliki za sehemu za majengo, kitendo ambacho kitawawezesha wananchi wengi hapa nchini kumiliki nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hapa nchini hatujawahi kuwa na Sheria maalum yenye utaratibu wa kutoa miliki katika sehemu za jengo, au nyumba zilizoungana, au nyumba zilizopo kwenye uzio mmoja kwenye kiwanja chenye hati moja. Nchi nyingi duniani zina utaratibu huu ambao wengine huuita “*Condominium*” ambao huwawezesha wananchi wengi kumiliki sehemu ya jengo badala ya kubaki kuwa wapangaji tu maisha yao yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hakuna Sheria yoyote inayosimamia utaratibu huu, hivyo basi Sheria inayopendekezwa kutungwa itaweka utaratibu wa Kisheria wa kutoa miliki kwa sehemu za majengo hasa kwenye “*flats*”, kitendo ambacho kitatoa fursa kwa watu wengi zaidi kumiliki nyumba au kuingia katika biashara ya ujenzi na uuzaji wa nyumba. Aidha, utaratibu huu utasaidia kuendeleza maeneo ambayo yamejengwa kiholela, kwani ni rahisi kwa waliojenga kiholela kuingia mkataba na mwekezaji ili abomoe nyumba zao kisha ajenge maghorofa ya kisasa ambapo wao watamilikishwa sehemu ya majengo hayo na sehemu inayobaki itakuwa ya mwekezaji.

Madhumuni ya Muswada, madhumuni ya Muswada huu ni kutunga Sheria ya Miliki za Sehemu za Majengo (*Unit Titles Act*) kwa lengo la uendelezaji wa nyumba ili wananchi wengi waweze kuzimiliki. Pia hali hii itawezesha miji kukua kwa kuelekea juu (*Shadidi*) badala ya tambarare (*tandavu*) hali ambayo italeta matumizi bora ya ardhi na, upunguzaji wa gharama za usafiri na uwekaji wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu ndani ya Muswada; baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Utaratibu wa kusajili sehemu za majengo, hususan *flats*.
- (ii) Haki na wajibu wa wanaomiliki sehemu za majengo.
- (iii) Masharti ya uuzaaji/utoaji wa miliki za sehemu za majengo.
- (iv) Usimamizi wa eneo la majengo lenye miliki za sehemu ya majengo.
- (v) Utaratibu wa kutatua migogoro katika maeneo yenye miliki za namna hii.
- (vi) Ufutaji wa utaratibu wa kuwa na miliki za sehemu katika jengo.
- (vii) Utaratibu wa malipo ya gharama mbalimbali zinazotozwa na mamlaka husika.
- (viii) Ushirikishwaji wa wadau wanaohusika na uwekaji wa miundombinu katika maeneo ya majengo.
- (ix) Uanzishaji wa vyama (*Association*) vya wanaomiliki sehemu ya jengo ambavyo vitakuwa na nguvu ya kisheria kusimamia masuala yote yahusuyo umilikaji wa pamoja wa majengo husika.
- (x) Umuhimu wa kutambua hati miliki za vipande (*Unit Titles*) kwenye Sheria ya Uandikishaji Ardhi (*Land Registration Act*).
- (xi) Ushirikishwaji wa wadau wanaohusika na uwekaji wa miundombinu katika maeneo ya majengo kama maji, barabara, umeme, mifereji ya maji taka, na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpangilio wa Muswada; Muswada umegawanyika katika sehemu kuu nane zinazopendekeza mambo mbalimbali kuhusu miliki za sehemu za majengo:-

- (i) Sehemu ya kwanza inahusu jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika, na matumizi ya tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya Sheria hii.

- (ii) Sehemu ya pili inahusu utaratibu wa kuanzisha na kusajili sehemu za majengo.
- (iii) Sehemu ya tatu inahusu haki za miliki na wajibu wa wanaomiliki sehemu za majengo.
- (iv) Sehemu ya nne inahusu miamala (*transactions*) ikiwa ni uhamishaji wa miliki kwa kuuza au kupeana zawadi au uwekaji wa rehani katika vyombo nya fedha ili kupata mikopo.
- (v) Sehemu ya tano inahusu uanzishwaji wa vyama (*associations*) ambavyo vitajihusisha na namna ya uendeshaji na usimamizi wa eneo la majengo lenye miliki za sehemu za majengo; kama ulipaji kodi ya kiwanja, ukarabati wa jengo, usafishaji wa maeneo ya huduma za pamoja kama ngazi, umiliki wa pamoja wa ardhi (*plot*) mahali jengo lilipo na kadhalika.
- (vi) Sehemu ya sita inahusu utaratibu wa kutatua migogoro; katika maeneo yenye miliki za sehemu ya majengo.
- (vii) Sehemu ya saba inahusu ufutaji wa utaratibu wa kuwa na miliki za sehemu katika jengo.
- (viii) Sehemu ya nane na ya mwisho inahusu masuala ya jumla kama vile, kodi, ushuru, kanuni, bima ya umiliki wa pamoja wa jengo na msisitizo wa kuitafsiri Sheria hii katika lugha ya Kiswahili ili wananchi waielewe na watumie fursa hii kujipatia nyumba bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho; kupitishwa kwa sheria hii, itakapoanza kufanya kazi pamoja na ile sheria inayoweka utaratibu na mazingira mazuri ya utoaji wa mikopo ya nyumba (*Mortgage Financing Bill*), italeta chachu na msisimko mkubwa katika maendeleo ya Sekta ya nyumba hapa nchini.

Wawekezaji katika ujenzi wa majumba (*Estate Developers*) watapata mikopo ya muda mrefu na yenye riba ndogo hivyo watajenga majumba kwa wingi, na wanunuzi watakuwa wengi kwani nao watakopa fedha kupitia mikopo ya nyumba na kununua sehemu ya nyumba. Wapangaji wengi watawezeshwaa kumiliki sehemu ya nyumba na hivyo kugeuka kutoka kuwa wapangaji na kuwa wamiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu unaotafsiri kwa vitendo sera ya upatikanaji wa nyumba bora kwa wananchi ikiwa ni mchakato sahihi wa kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Hivyo Waheshimiwa Wabunge mnaombwa muunge mkono muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika naingia katika kuwasilisha muswada wa pili ambaa ni:-

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali Kuwezesha Ardhi Kutumika Kupata Mikopo ya Kibenki (*The Mortgage Financing Bill*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Muswada: Muswada huu unakusudia kurekebisha sheria mbalimbali ili kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya uendelezaji wa nyumba (*Mortgage Financing Bill*); Sheria inakusudia kutatua tazito la ukosefu wa nyumba bora hapa nchini kwa kuwawezesha wananchi wa kawaida kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Ardhi, Sheria ya Usajili wa Ardhi na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho yanayopendekezwa katika Muswada huu yatarahisisha na kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya uendelezaji wa nyumba. Hivi sasa hapa nchini hakuna utaratibu mahsuswa wa mikopo ya nyumba, mikopo iliyopo ni ya kibashara ambayo ni ya muda mfupi na riba kubwa. Kwa kawaida mikopo ya nyumba huwa ni ya muda mrefu, takribani miaka 10 na kuendelea na riba huwa ipo chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna mapungufu ambayo yanaathiri mchango wa sekta za kibenki katika kutoa mikopo kwa ajili ya uendelezaji wa nyumba. Mapungufu hayo yanahusu taratibu za Sheria, mfumo wa mahakama ambao hauzingati mizania ya haki kati ya mkopaji na taasisi inayotoa mkopo, urasimu katika uandikishaji hati miliki za ardhi na uhamishaji wake, na kuwepo kwa mfumo wa soko la fedha ambao hautoi fursa kubwa za upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madhumuni ya Muswada; madhumuni ya Muswada huu ni kufanya marekebisho katika Sheria ya Ardhi, (*The Land Amendment Act No. 2*) ya mwaka 2004; Sheria ya Usajili wa Ardhi, (*The Land Registration Act Cap. 334*) na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai (*The Civil Procedure Act*).

Mheshimiwa Naibu Spika,, marekebisho yanayokusudiwa yataboresha mazingira na kujenga imani miongoni mwa Taasisi zinazotoa mikopo kwa ajili hiyo na kubainisha kwa uwazi zaidi majukumu yao kwa wateja. Aidha, marekebisho hayo yataondoa mazingira na mfumo wa mahakama wa sasa ambao unalinda wakopaji wanaoshindwa kulipa mikopo kwa sababu zisizokuwa za msingi. Mfumo uliopo hivi sasa unasababisha mabenki kusita kutoa mikopo, au kupandisha riba na kutoa mikopo ya muda mfupi ili kupunguza athari za uwezekano wa kutolipwa.

Muswada huu kwa hiyo unalengo la kujenga utamaduni mpya kwa Watanzania kupata mikopo ya nyumba na kuwa na nidhamu ya kurejesha mikopo kwa mujibu wa mikataba ya mikopo hiyo. Muswada unaondoa ujanja ujanja wa ‘kukopa harusi kulipa

matanga na ule wa kukimbilia Mahakamani na kuweka kizuizi (*injunction*) ili kukwepa au kuchelewesha ulipaji wa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu katika muswada; baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

- (1) Wajibu wa mkopaji kutoa taarifa sahihi kwa mkopeshaji kuhusiana na kibali cha mwenza au wenza (*spouses*) au mtu yoyote mwengine anayehusika na nyumba inayowekwa rehani kinachohitajika katika upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya nyumba, na kwamba utoaji wa taarifa potofu utakuwa ni kosa la jinai chini ya Sheria hii.
- (2) Wajibu wa Taasisi inayotoa mkopo kumpa taarifa zote muhimu mkopaji kwa uwazi kabisa kuhusiana na mkopo na masharti yake hususan riba.
- (3) Haki ya Taasisi inayotoa mikopo kutoa notisi ya siku sitini (60) endapo mkopaji ameshindwa kulipa mkopo kulingana na mkataba ili kuweza kuuza nyumba inayohusika bila kuomba kibali cha mahakama na haki ya mwananchi au Taasisi itakayonunua nyumba hiyo.
- (4) Mfumo wa sheria za mwenendo wa mashauri ambao hautatoa nafasi kwa mkopaji kutumia Mahakama kuchelewesha haki ya Taasisi inayotoa mkopo pale mkopaji anaposhindwa kulipa kulingana na Mikataba.
- (5) Marekebisho yanayopendekezwa yanaweka misingi miwili ambayo itamwezesha mkopaji kwenda Mahakamani, kwanza awe hajachukua mkopo unaohusika, pili awe amekwishalipa mkopo husika.
- (6) Kuweka utaratibu wa uandikishaji wa uhamishaji wa nyumba zinazohusika na mikopo ya nyumba kufanywa moja kwa moja na Msajili wa Ardhi bila kibali cha Kamishna wa Ardhi.

Kamishna wa Ardhi atafahamishwa na Msajili wa Hati baada ya uandikishaji kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpangilio wa Muswada; Muswada umegawanyika katika sehemu kuu nne.

Sehemu ya kwanza inahusu masuala ya Utangulizi kama vile Jina la Sheria na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria.

Sehemu ya pili inahusu mapendekezo ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Ardhi (Sura ya 113) kwa kuweka utaratibu wa utoaji taarifa unaohusu kibali cha mke au mume au mtu yejote mwingine anayehusika na nyumba inayokusudiwa kuwekwa rehani wakati wa kuomba mkopo na pia mkopeshaji kumpa taarifa zote muhimu mkopaji zinazohusu mkopo husika na masharti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vile vile marekebisho yanapendekeza kuwa Taasisi inayotoa mikopo kutoa ilani ya siku 60 endapo mkopaji ataonekana kushindwa kurudisha mkopo na hivyo mkopeshaji kuwa na uwezo wa kuiuza nyumba husika pasipo kuhusisha Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya tatu ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334) ambapo inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 41 ili uandikishaji na uhamishaji wa milki ya nyumba zinazohusiana na mkopo ufanywe moja kwa moja na Msajili wa Ardhi bila kibali cha Kamishna wa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya nne, inalenga kufanya marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai (Sura ya 33) na kwamba inapendekezwa vifungu 74 na 78 virekebishwe ili kuweka mfumo wa mwenendo wa mashauri kisheria ambao hautatoa nafasi kwa mkopaji kutumia Mahakama ili kuchelewesha haki ya Taasisi inayotoa mkopo pale mkopaji anaposhindwa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho; kupitishwa kwa Sheria hii kutaleta ukombozi mkubwa kwa mamilioni ya Watanzania ambao hawana fedha za mifukoni mwao za kujenga nyumba bora. Utaratibu huu utawawezesha kupata mikopo ya kibashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha; kwa kupitisha Sheria hii, Bunge letu tukufu litakuwa limeandika historia ya kuleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya ujenzi wa nyumba bora hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, Naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. JOB Y. NDUGAI-MWENYEKITI KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa sheria ya kurekebisha sheria mbalimbali kuwezesha ardhi kutumika kupata mikopo ya kibenki '*The Mortgage Finance Act 2008*' na Muswada wa Sheria ya Miliki za sehemu za Majengo '*The Unit Titles Act, 2008*'.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007 niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Muswada wa sheria ya kurekebisha sheria mbalimbali kuwezesha ardhi kutumika kupata mikopo ya kibenki *Mortgage Finance Act, 2008*, ambao unakusudia kurekebisha Sheria ya Ardhi ya mwaka 2004, Sheria ya Usajili wa Hati, Sheria ya Mahakama za Mahakimu Wakazi na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai. Na Muswada wa sheria ya miliki za sehemu za majengo *The Unit Titles Act, 2008* ambao unakusudia kuweka utaratibu kisheria unaolenga kuwezesha kuwepo na utaratibu wa kutoa miliki za sehemu za majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Miswada hii ni:-

(i)Kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali ili kuboresha mazingira na kuweka mfumo wa upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba kwa kumlinda mkopaji na mkopeshaji na kuweka haki na wajibu kwa wote.

(ii)Mapendekezo ya kisheria ya kutunga sheria ya kuwezesha kuwepo na utaratibu wa kusimamia na kuratibu miliki za sehemu za majengo zitakazomilikiwa na mtu mmoja au vikundi kwa pamoja kwa madhumuni ya kuwezesha watu wengi kumiliki nyumba na hivyo kuleta hali ya matumizi bora ya ardhi na kuwezeshwa kutumia raslimali hizo katika mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilikutana tarehe 28/10/2008 na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, kujadili kwa kina Miswada hii miwili ambayo ni ya dharura kwa lengo la kuboresha. Majadiliano hayo yalisaidia sana kuibua mawazo

mapya, maoni na hoja mbalimbali za kujenga Miswada hii. Maoni na Ushauri wa kamati ni matokeo ya mchakato huo wa kubadilishana mawazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, (Mb) ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, pamoja na Kamati nzima ya Fedha na Uchumi kwa kutoa maoni yao hapo awali ambayo yamepelekea Muswada huu kuwa na sura uliyonayo sasa Miswada yote miwili na kufikiwa hali ya kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba Miswada hii ni ya dharura kwa mujibu wa kanuni ya 80 (4) hivyo Kamati haikuwa na fursa ya kualika wadau kutoa maoni yao mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia Kamati katika kuchambua Miswada hii. Ila napenda kulitaharifu Bunge lako tukufu kwamba Kamati yangu ilikaa na kujadili kwa kina Miswada hii na kutoa mapendekezo yake ambayo nitaieleza muda si mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada hii imebeba sura tofauti tofauti zenyе maudhui ya kuhakikisha wadau wote wanapata haki na wajibu wa kumiliki kwa pamoja mali hizo, au mmoja mmoja, imeweka utaratibu wa namna ya kushughulikia migogoro mbalimbali itakayojitokeza na uanzishwaji wa chama cha hiari kitakachosimamia mali inayomilikiwa kwa pamoja. Pia imeainisha utaratibu wa malipo ya huduma za pamoja kama umeme, maji, upakaji rangi, usafi wa sehemu za pamoja kama ngazi na maeneo ya korido na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inakubaliana na inaunga mkono Serikali kuwasilisha miswada hii ya sheria mbele ya Bunge lako tukufu kwa kuzingatia sababu zifuatazo:-

- (i) Sekta za benki zitapata fursa ya kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na uendelezaji wa nyumba.
- (ii) Sheria itatoa fursa kwa watu wengi kumiliki nyumba au kuingia katika biashara ya ujenzi wa nyumba na upatikanaji wa ajira kwa vijana katika sekta ya ujenzi.
- (iii) Marekebisho haya yataboresha mazingira na kujenga imani mionganini mwa taasisi zinazotoa mikopo.
- (iv) Matumizi bora ya Ardhi yatazingatiwa.
- (v) Itasaidia kutatua migogoro katika maeneo yenye miliki zaidi ya mtu mmoja.
- (vi) Sheria imeelezea namna ya kuhamisha mali *disposition* kwenda sehemu nyingine kwa njia ya kuuza, kuweka rehani, kuhamisha miliki, kutoa kama zawadi, kupangisha na hata kukana miliki na kadhalika.

(vii) Pia ni maoni ya Kamati kwamba sheria italeta utaratibu wa ushirikishwaji wa wadau katika uwekaji wa miundo mbinu katika majengo.

Hivyo basi, Miswada hii italeta ufumbuzi wa upatikanaji wa nyumba za kuishi kwa maeneo ya mijini na vijijini.

Maoni na Ushauri wa Kamati Kuhusu Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali Kuwezesha Ardhi Kutumika Kupata Mikopo ya Kibenki (*Mortgage Finance Act 2008*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kuweza kuwasilisha Muswada huu wenye lengo la kuwakomboa Watanzania wengi ambao hawana uwezo wa kujenga nyumba za kuishi. Kamati inasisitiza kwamba, Wizara isimamie kikamilifu sheria zote za ardhi zitakazosimamia utoaji wa mikopo ili kuhakikisha haki inatendeka kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya ardhi bado inakabiliwa na migogoro mingi ya ardhi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba sheria hii ya *Mortgage Finance* haitakuwa chanzo cha migogoro mingine zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mabenki kwa kutoa mikopo ya nyumba, sheria hii inaweka mizania kati ya mkopaji na haki zake na mkopeshwaji na haki zake. Sheria zilizopo sasa zinamlinda mkopaji kupita kiasi .

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ikipitishwa na Bunge lako tukufu, itakuwa chachu ya maendeleo kwa watu wa kipato cha chini na kati. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha sekta za Benki zinatoa mikopo kwa watu wa chini na kati ili kuwawezesha kuwa na nyumba bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa fedha uliopo sasa ni ule ambao hautoi mikopo ya muda mrefu na riba ndogo. Kwa sheria hii mikopo hiyo itapatikana na tutaondokana na mfumo wa mabenki ya biashara wa sasa wa riba kubwa na muda mfupi wa mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa angalizo kwamba, Sheria hii isiwe chanzo cha wenye uwezo wa fedha wasio na hati miliki ya ardhi kuwarubuni watu wa kipato cha chini ambao wana hati miliki ya ardhi, haki itendeke kwa kila upande.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu wa sheria utaondoa mapungufu yanayohusu taratibu za kisheria hasa katika mfumo wa mahakama. Hivyo mizania ya haki ya mkopaji na taasisi inayotoa mikopo imezingatiwa ipasavyo. Mkopaji hatatumia Mahakama kuchelewesha malipo Benki na mahakama pekee itakayosikiliza kesi za masuala *Mortgage Finance* ni Mahakama kuu kitengo cha Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa wananchi namna sheria hii itakavyofanya kazi kwa sababu jambo hili ni jipya.

Maoni na Ushauri wa Kamati Kuhusu Muswada wa Sheria Miliki ya Sehemu za Majengo (*The Unit Titles Act, 2008*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini hatujawahi kuwa na sheria maalum yenye utaratibu wa kutoa miliki katika sehemu za jengo au nyumba zilizoungana, au nyumba zilizopo kwenye uzio mmoja kwenye kiwanja chenye hati moja. Kamati inaona kwamba hii ni fursa kwa wananchi wengi kumiliki nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la sheria hii ni kuwawezesha Watanzania kupata nyumba au fedha za kujenga nyumba na kumilikisha sehemu ya jengo husika. Mwananchi anaweza kukopa na kununua sehemu ya jengo na kupata hati miliki kwa sehemu husika ya jengo hilo. Kwa sheria hii kiwanja kimoja kinaweza kujengwa na watu wawili au watatu kwa pamoja na kila mtu akamiliki sehemu ya jengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitishwa kwa sheria hii, ikifanya kazi na ile sheria ya utoaji wa mikopo ya nyumba (*Mortgage Finance Bill*) italeta chachu na msisimko mkubwa katika maendeleo ya sekta ya nyumba hapa nchini kwa kuruhusu watu wenye uwezo kujenga majengo na kuyauza kwa *Units* moja moja kwa wenye nia ya kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata nyumba bora ikiwa ni changamoto ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzani, kwa vile nia ya sheria ni watu wengi zaidi waweze kumiliki nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inaishauri serikali iandae miundombinu ili iweze kukidhi haja ya wawekezaji katika ujenzi wa majumba (*Estate Developers*) ambao tunategemea watajenga nyumba kwa wingi kutokana na mikopo ya nyumba watakayopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii inayopendekezwa kutungwa itaweka utaratibu wa kisheria wa kutoa miliki kwa sehemu za majengo hasa kwenye *flats*, pia inaweka haki na wajibu wa wanaomiliki hilo jengo. Kamati inaona kwamba utaratibu huu utasaidia kuendeleza maeneo yaliyojengwa kiholela kwa kuingia mikataba na wawekezaji na hatimaye mwananchi kumilikishwa sehemu ya majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii itawezesha kukua kwa miji kwa kufanya miji kukua kwa ujenzi wa maghorofa yanayoenda juu kwa sababu juu kuna ploti za bure zinazotegemea uwezo wa mjenzi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kuwatambua kwa majina wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Maoni na Ushauri wa Miswada hii yote miwili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Hassan R. Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati wakati Wajumbe ni Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mjumbe Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa William V. Lukuvi,
Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji na Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo , Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelili, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Aziza S.Ally,
Mheshimiwa Lucy T. Mayenga na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ina wajumbe 25. Kamati inaikumbusha Serikali kuwa Benki ya Nyumba ilikufa kwa sababu ya kukosekana kwa umakini wa kutowalinda wakopeshaji na kuhakikisha kuwa dhamana zilikuwepo kweli, makosa haya tusiyarudie huko tunakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakumbusha Bunge lako tukufu kuwa hali mbaya ya Uchumi Duniani hivi sasa imesababishwa na *Mortgage Finance* hadi baadhi ya mabenki Marekani yametaifishwa.

Hali hii imetokana na kukosekana umakini katika kukopesha, kwa kuwakopesha hata kwa wale wasiostahili kukopeshwa, mikopo ya matrilioni ya dola imepotea na dhamana hazikuwepo. Matumaini yetu ni kwamba tutajifunza kutohana na hali hii hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani.napenda kumshukuru Kaimu Katibu wa Bunge Ndugu Thomas Kashililah kwa kuiwezesha kamati kufanya kazi zake bila

matatizo na Makatibu wa Kamati Ndugu Michael Kadebe na Elika Saanya kwa kuihudumia kamati vizuri wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ,Mhe Capt. John Z. Chiligati (Mb), Katibu Mkuu wa wizara na watendaji wote wa Wizara pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kushiriki kikamilifu kuandaa na kuboresha Miswada hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Miswada yote miwili.

MHE. MAGDALENE S. SAKAYA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI :
Mheshimiwa Naibu Spika,Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa kanuni za Bunge Kanuni ya 86 (6) toleo la mwaka 2007, napenda kutoa maoni kuhusu Muswada wa kurekebisha sheria mbali mbali ili kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya kutoa mikopo ya nyumba ya mwaka 2008, pamoja na Muswada wa Sheria ya kuwezesha kuwepo utaratibu wa kusimamia miliki za sehemu za majengo zitakazomilikiwa na mtu mmoja au vikundi kwa pamoja kwa madhumuni ya kuwezesha watu wengi kumiliki nyumba wa mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Capt. John Chiligati pamoja na watendaji wakuu wa Wizara kwa juhudhi zao za kutaka kuona Watanzania wote wanamiliki nyumba zenye hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana kwa kuboresha maisha ya Watanzania walio wengi, hivyo haukutakiwa kuleta chini ya hati ya dharura. Hii imewanyima haki ya kutoa maoni wadau muhimu ambaa ndio watekelezaji wakuu wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata mashaka kwamba wananchi wengi watapoteza nyumba zao pale ambapo watakuwa wamekopa na wanapoteza kazi kabla ya kumaliza mikopo yao benki. Nyumba zao zitapigwa minada hivyo kukosa makazi na wakati huo huo mtu amepoteza kazi yake.

Je, hii si kumzidishia Mtanzania umasikini? Kambi ya Upinzani inaona kwamba wadau ndio walitakiwa kutoa maoni yao katika hili kama hiyo ni jinsi gani sheria inamlinda mwananchi huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona muswada huu ulistahili kuitwa *miscelaneous ammendments* na sio *Mortgage financing (special provision)* kama

ambavyo unaitwa, ukizingatia kwamba zaidi ya asilimia 95% ya Muswada huu ni marekebisho ya sheria ya ardhi, ambayo katika muswada huu inaitwa *Principal Act*. Takribani asilimia zilizobaki ni marekebisho ya sheria ya usajili wa Ardhi, sura 334 na marekebisho ya sheria ya Mwenendo wa makosa ya Madai, sura ya 33.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inasema hivyo kwa kuzingatia kuwa muswada huu hauna tafsiri ya maneno na badala yake, tafsiri ya maneno inayotumiwa ni ile iliyomo kwenye sheria ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yetu pia inathibitishwa na aya ya kwanza uk. 14 ambayo inazungumizia madhumuni ya Muswada huu kuwa ni nanukuu: “kufanya marekebisho ya sheria mbali mbali ili kuboresha mazingira na kuweka mfumo wa upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya uendelezaji wa nyumba”.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani kwa ujumla inataka kutoa tahadhari kuhusu madhara ambayo yanaweza kutokea kutokana na sheria hii kutokutilia maanani hali halisi za vipato vya wananchi wa kawaida ambao ni walengwa wakuu wa Muswada huu, uwezo wao wa kurejesha mikopo, kwa ujumla Muswada huu umezingatia hali halisi ya ajira na ujira kwa Watanzania walio wengi na hili limezingatiwa kwa kiwango gani? Tunaweka angalizo kwa kuangalia hali halisi ya wakopaji wengi waliokopa fedha zinazoitwa za JK ni wangapi wamerejesha hadi sasa ili na wengine waendelee kukopeshwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kukopa na kurejesha ni tabia na haijalishi kuwa mkopo huo ni wa kufanya nini na udhamini wa mkopo huo ni mali gani iliyoudhamini, urejeshaji wa mikopo ni tabia tu au nidhamu ya kuheshimu vyta watu wengine. (*Makofi*)

Kambi inaona kuwa kama mambo hayo hayakufanyiwa upembusi yakinifu matokeo yake ni kulipa kundi fulani la wajanja wachache neema ya kupata fursa kisheria kuendelea kujichotea mabilioni ya shilingi za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna madhara makubwa yamelikumba soko la hisa la nchi ya Marekani pamoja na Nchi za Ulaya na Japan kutokana na madhara ambayo yalisababishwa na *Mortgage financing* katika nchi ya Marekani.

Hii imesababisha mabenki makubwa kufilisika na wananchi wengine waliokuwa na amana zao kwenye mabenki hayo, wamebaki masikini. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni Jambo gani la haraka inaloliwahi hadi kuleta Muswada huu wakati Dunia nzima kifedha haiko katika hali ya amani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona Serikali bado haijajifunza kutokana na yale yote ambayo yameikumba sekta ya fedha nchini Marekani na mtikisiko wake karibu kuiathiri Dunia nzima. Je, makosa hayo yaliyotokea Marekani yamezingatiwa kwa kiasi gani katika uandaaji wa Muswada huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada wa sheria inayohusu kuwawezesha wananchi ambao wanakaa katika maghorofa kuweza kumiliki nyumba ambazo wanaishi yaani *Unit Titles Act*.

Kwa ujumla Kambi ya Upinzani haina pingamizi na Muswada huu na kwa kweli unalengo zuri tu. Ila pamoja na lengo lake hilo zuri, tunatahadharisha wale ambao wanaachu wa kuwanyang'anya wadogo walichonacho, wasianze sasa kuwahamisha wapangaji ambao wamekuwa kwenye nyumba hizo kwa kipindi kirefu, halafu wao au ndugu zao ndio wapewe miliki za nyumba hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya tunayoyasema yamekwisha jitokeza pale wapangaji wanapohamishwa kwa kisingizio kuwa nyumba inauzwa halafu wanapangishwa wengine ambao wanaweza kulipa kodi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa mangalizo hayo muhimu, nawashukuru wote kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kwanza niseme kwamba naunga mkono hoja zote mbili kwa sababu zinaeleweka lakini labda niseme kwamba kilichonifanya nikaona nichangie labda itamsaidia Waziri wakati akiandaa kanuni regulations anaweza akazingatia baadhi ya mawazo haya.

Huko nyuma miaka ya 90 niliwahi kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa shirika la nyumba ambapo niliunganisha lilikuwa shirika la nyumba la taifa lile la mwanzo na msajili wa majengo na kuanzisha shirika la sasa la nyumba la sasa kama tunavyolifahamu.

Kwa hiyo wakati wa kipindi hicho cha uenyeketi wangu wa shirika la nyumba nilijifunza mambo mengi sana juu ya matatizo ya majengo matatizo ya nyumba, matatizo ya wapangaji na haya ndiyo yaliyonifanya niseme kwamba labda naweza nikachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kwamba sasa hivi nafikiri kuna watu tayari wako kwenye utaratibu huu wa unit trust bila kuwa sheria na hakika kuna watu ambao wako kwenye utaratibu huu ingawa sheria hii ilikuwa haipo. Sasa nilikuwa nataka kuuliza je si vema watu hawa wakatakiwa kuandikisha hizo unit za kwao chini ya sheria hii ili baadaye tuje kukwepa migogoro.

La pili hivi sasa kuna wanaojenga nyumba majengo makubwa kwa kuchangisha wengine anasema mimi ninataka kujenga gorofa tano, sita anayetaka *flat* huko ndani au *flow* nzima alipe kiasi fulani cha fedha mimi niendelee kujenga ikifika imekamilika yeye ataweba kuchukua *flat* yake humo ndani. Na hakika watu wa namna hii kuna sheria wanazo tumia kuharalisha jambo hilo, lakini baadaye jambo la namna hii litazidi kuwepo na litazidi kubwa na hasa kama litahusu watu ambaeo hawana fedha nyingi.

Mimi nafikiri kuna haja ya kuwa na utaratibu kwa mtu anayetaka kujenga nyumba za namna hiyo kwa kuokota hela kwa watengi kulinda wale wanaompa hizo fedha maana huyu anaweza wajanja wataamka tu watatangaza anayetaka kushirikishwa kwenye nyumba iliyo *plot* fulani mahali fulani atoe shilingi fulani atapata *flat* ya saizi fulani kisha huyu kafanya mambo mengine au kajenga majengo rojorojo baadaye chini ya sheria tulioipitisha hapa juzi kuamkia jana ile ya *contractor registration* baadaye labda makandarasi wakaenda wakaisimamisha fikiria kama ungelikuwa uko kwenye *unit* ya jengo lililoanguka hivi karibuni pale Dar es Salaam, itakuwaje na wewe umeshatoa fedha na yule amejenga jengo rojorojo na limeanguka au linatishia kuanguka itakuwaje.

Kwa hiyo, mimi nafikiri watu wa namna kuna haja ya kuwalinda hawa waliotoa fedha na kuweka utaratibu wa kumdhiliti mtu anayejenga ili asifanye mambo hovyo hovyo na asitoroke na fedha za hawa ambaeo anajidai anataka kushirikiana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu nilitaka kuchangia ni kwamba mle ndani hii *tenancy association* inayotajwa hapa nafikiri ni jambo muhimu sana nadhani kwenye nchi nyingine Amerika nadhani *home owners association*.

Nafikiri ni muhimu sana kwenye *regulations* labda tukaweka mambo ambayo unaweza ukasema *dooms* mambo ambayo yasifanyike yasitendeke kwa watu ambaeo wanaishi kwa utaratibu huu wa *units* nao ni kwa mfano wasiruhusiwe kufanya biashara mle ndani yaani wasifungue maduka au *bar* au migahawa au vitu vyaa namna ile mle ndani kwa sababu hii inaweza ikawa ni chanzo kimojawapo cha migogoro yaani wale *tenancy* wale *owners* wa *unit* na *tenancy*.

Ya pili kuwepo na *standards* za usafi kwa maeneo na majengo yenye, majengo yatapigwaje rangi je maji machafu yatahibitiwa namna gani kwa taratibu gani je takataka zitatupwa wapi kwa utaratibu gani mambo ya namna hiyo je, kama kule ndani waruhusiwe kufuga paka, mbwa, wanyama wengine mbuzi ng'ombe, kondoo, nguruwe, kuku ufugaji kwa maeneo kama haya ni lazima udhibitiwe kabisa.

Je, watu wakikaa mle ndani wakawa wanacheza muziki kila wakati mpaka usiku wa manane vijana wacheza muziki tu na wazee wako kule wanakoroma lakini hawawezi kwa sababu muziki unawasumbua sasa itakuwaje yaani kitu wanaita *noise, noise control music* kwa hiyo hata muziki unaweza ukawa ni *noise*.

Kwa hiyo, mambo ya namna hii migogoro kati ya mwenye unit moja na unit nyingine au mpangaji na mpangaji migogoro mle ndani ishughulikiweje. Na mimi nilikuwa napendekeza kwamba katika hali kama hiyo ingewezekana kabisa wakazi wa unit wakashughulikia hata barabara hata mtaa ule ambao unit zile zimo kwa mfano mimi nasikia kwamba kwenye mtaa mmoja unaitwa Boboyo nadhani kuna Naibu Waziri Dr. Maua ni mkazi wa mtaa huo.

Mtaa ule una nidhamu sana wakazi wa mtaa ule baada ya kukabidhiwa nyumba hizi za Serikali wameunda chama cha kulinda mtaa, usalama, usafi, mtaa, maji na ninavyosikia mifano wa watu kujitunza wenyewe bila kutegemea Serikali.

Na mimi nadhani maeneo kama ya namna hii ndani ya eneo lao na hata lile eneo la barabara linalowahusu wanaweza pia wakawa na utaratibu wa kumiliki.

Sasa na sheria hii vilevile nadhani ingesema kuhusiana na kile chama tunakiita *Association* kiendeshwe kwa utaratibu gani na kiweje je ni chama cha kujitolea au ni chama ambacho kinaajiri watu nusu kujitolea nusu kuajiri na utaratibu utakuwaje ili kusudi chama hicho kiweze kuwa na meno kiasi fulani na vilevile kiweze kuendeshwa kistaarabu sio kihuni huni au kuwa kama vyama vyaya wacheza mpira ambavyo kila siku vina migogoro.

Nafikiri kwenye sheria sikuona nimeona tu Mwenyekiti tu na Katibu nafikiri ni muhimu pia awekwe na mweka hazina kwa sababu mara ingine wakazi wale watapenda kuchanga fedha kwa shughuli fulani fulani za eneo lao kwa hiyo ni vizuri wawe na hata kukopa fedha unaweza ukakopa kufanya mambo fulani kwa hiyo ni vizuri kuwa na mweka hazina na wajumbe ukweli kingkuwa kitu kama bodi hivi *board of directors* ambao wana Mwenyekiti, wana Katibu wana mweka hazina na wajumbe na uamuzi wao ujulikane uwe na nguvu kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamalizia ningependa baada ya kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Miswada hii nikumbushie Serikali kwamba kuna Muswada mwengine ambao unaendana na huu wa *Mortgage Finance* ambao haujatoka nao.

Muswada wa *higher purchase* ni Muswada wa *Higher Purchase* kukopa vifaa. Ambao unafanafana kwa kiasi kikubwa na huu wa *mortgage finance* ningependa kutoa rai Serikali kwamba Muswada huu nao uje upesi ili sasa tuweze kukamilisha eneo hili la kukopa na kufanya shughuli na mikopo hiyo na baadaye zile mali zilizokopwa kuweza kuwa za wale waliokopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana mchango wangu ni huo natumaini langu ni kwamba muda si muda utaanza kufanya kazi ili wengine ambao tuna *interest* na mambo haya tuweze kufaidika. Naomba tena kuunga mkono hoja hii. (*Makofit*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango kidogo kwenye Miswada hii miwili; Muswada wa Utoaji wa Miliki ya Sehemu za Majengo wa Mwaka 2008 (*The Unit Titles Bill, 2008*), pamoja na Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Nyumba wa Mwaka 2008 (*The Mortgage Financing (special provisions) Bill, 2008*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sasa tumefika mahali pa kuihudumia jamii kwa sababu kwa muda mrefu watu wanahangaika kuhusu makazi. Hawana uwezo wa kujenga kwa kutumia vipato vya mishahara wala kwa kutumia vipato vya biashara zao ndogo ndogo. Kwa hiyo, ujenzi wa nyumba umekaa kwa watu ambao wana uwezo na wametumia nafasi hiyo kwa nguvu sana na wamejitajirisha kweli kweli. Nadhani hapa tutapenda kuipongeza Serikali kwa hatua hii iliyochukuliwa. Labda la kufanya ni ule ucharaka uliokuja kwenye Miswada hii; ucharaka huo huo uende kwenye kutoa mikopo, kwenye kupangisha zile sehemu za majengo na Wizara ya Ardhi iwe karibu kabisa na pengine ingeteua kitengo kimoja cha kufuatilia maovu ambayo yanaweza kujitokeza katika kuitekeleza sheria hii itakapoanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na benki, bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ameitaja; Benki ya Nyumba (*Tanzania Housing Bank*). Baada ya kufutwa benki hiyo maalum kumekuwa na pengo kabisa, kwa hiyo, watu wa hali ya chini hasa watumishi wamekuwa ni watu wa kuhangaika. Wanapostaa fu wanakuwa na matatizo, inabidi wang'anga'anie kubaki kwenye nyumba za Serikali au Mashirika na kuleta hoja mbalimbali kwa sababu hawakuwezeshwa ili wajenge nyumba zao wajitegemee. Sasa nadhani katika Serikali kuwe na utarataibu kabisa mtu anapoajiriwa akishamaliza kipindi kile cha matazamio cha miaka miwili, ashauriwe kuchukua mkopo ili aweze kujitengenezea makazi yake na tuondokane sasa na hii kazi ya Serikali kuwajengea wafanyakazi wake nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliajiriwa siku nyingi na wakati huo hii *Tanzania Housing Bank* ilikuwepo. Nakumbuka mwaka 1977 nilichukua mkopo wa shilingi 80,000 nikiwa Mkurugenzi wa Maendeleo wa Mkoa wa Arusha. Nilipewa muda wa miaka kumi kuurudisha, kwa hiyo niliurudisha mwaka 1988. Nilikuwa bado hata sijafikia kustaafu, nilikuwa kijana wa katikati hapa. Sasa tusije tukashikilia zaidi huku juu, tuwahamasishe vijana wanaoingia kazini hawa wasitazamie mtu yejote kuwatafutia nyumba, nyumba ni jukumu lao. Maadam sasa tunaweka utaratibu wa kukopesha mikopo ambayo ina riba ndogo na ya muda mrefu, ule niliopewa mimi ulikuwa ni wa miaka kumi, kwa hiyo, nadhani ukimpa mtu muda mrefu inakuwa ni rahisi zaidi kuweza kurejesha mkopo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ujenzi wa nyumba, mimi kwa uzoefu wangu bahati nzuri wakati huo vifaa vya ujenzi vilikuwa rahisi kwa hiyo nyumba ile niliisimamia mwenyewe Arusha. Wakati huo kule *Wazo Hill* walikuwa wanamruhusu mtu mmoja mmoja kwenda kununua simenti mpaka tani kumi, lakini sasa hivi ukimpa mkopo mtumishi wa Serikali kwenda kupata simenti *Wazo Hill* itakuwa ni ndoto labda ahamie kabisa weke kambi pale, akae kwenye hema kufuatilia hilo. Kwa hiyo, nashauri kwamba, tuwashauri hawa watakaochukua mikopo wasichukue mikopo wakasimamia kujenga nyumba hizo wenyewe hawatamatiliza; ni vizuri wanunue nyumba. Sasa katika hali hiyo ni vizuri Serikali isijitoe, isaidie kuhimiza na kuhamasisha watu wenyewe uwezo wasaidiwe maeneo ya kujenga nyumba. *Estate involvement* wasiachwe peke yao na katika hili kuna maeneo ambayo Serikali na mashirika yake kwa hivi sasa ambayo yanaendesha huduma mbalimbali hayawezi kujitoa.

TANESCO haiwezi kujitoa itahusika, mashirika haya ya maji yatahusika, mashirika ya posta yatahusika na mashirika ya simu yatahusika. Pengine yale mashirika ambayo serikali ina hisa, yanepewa umuhimu wa kwanza wa kusaidiwa kuweka miundombinu katika maeneo ambayo hawa waendelezaji wa ujenzi wa nyumba za kuza watafanya hiyo kazi. Iifikanyika hivyo, hata gharama za ujenzi zitakuwa ni ndogo lakini kama *estate developer* atawajibika kujenga barabara mwenyewe, kupeleka ule mtandao wa kwanza au wa mwanzo wa umeme, hizo nyumba zitakuwa ghali sana. Kwa hiyo, katika hili maadam tumeamua kusaidia watu wa kipato cha chini, basi tuendelee hivyo hivyo tuwasaidie waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana kabisa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, amelisisitiza hili la kuwasaidia hawa *developers* waelekezwe maeneo ambayo ni mazuri. Kwa mfano, kwa Dar es Salaam, sasa hivi tusijenge karibu sana na mji; tufungue *satellite towns* hao *developers* waoneshwe huko ili mji upanuke na kupunguza msongamano katika maeneo. Halikadhalika makampuni yanayoanzisha ofisi yaelekezwe ofisi hizo zitoke katikati ya Dar es Salaam, vinginevyo watakosa watu wa kwenda kufanya kazi huko. Likitokea lolote lile, mvua ikinyesha watu wanachukua zaidi ya saa mbili kufika kwenye ofisi zilizoko maeneo ya katikati ya Mji. Tatizo la msongamano wa magari nalisema kwa sababu sasa hivi limejitokeza, hata Rais amelisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la mikopo nadhani hapa ni vizuri pengine wangeajiri hata watu wa taasisi yetu ya kuzuwa rushwa. Tuondoe urasimu na tuweke mazingira ya kuondoa rushwa kabisa katika mikopo hii, kwa sababu kama hatukuweka hizi mbinu, kuna watu watakuwa na nia nzuri sana ya kuchukua mikopo, lakini watakuta mazingira ambayo wanashindwa hata kufikia kwenda kuchukua fomu ya kujaza. Kwa hiyo, nadhani tuanzie hapo kwamba, katika hili tusiwe na huruma na mtu yeoyote kwa sababu inawekwa kwa nia njema ya kusaidia watu wa kipato cha chini. Kuhusu hizi *unit*, utoaji wa sehemu za majengo nitazungumzia hasa majengo yale ambayo ni ya *National Housing Corporation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitaunga mkono hoja ya Wapinzani, wamesema kitu kizuri sana kwamba, kunaweza kutokea mchezo. *I am serious*, wakashakia

majengo hayo, vipande hivyo vitauzwa, watu wataanza kutolewa wataingizwa wengine, hili linafanyika. Kwa hiyo, nawashukuru sana wenzetu wa Upinzani kwa kusaidia kulieleza na mimi naliunga mkono hili kwamba ni lazima tuwe *serious* kuanzia leo hii, mtu aliyepo kwenye nyumba hiyo ambayo inahusika na vipande akitolewa, ichunguzwe ametolewa kwa sababu gain isije ikawa kuna bili yake ya nyumba hapelekewi. Kwa hiyo, analimbikiziwa kodi halafu anakuja kutolewa kwa kutolipa kodi kumbe bili hazikupelekwa. Kwa maana hiyo, kuna ndugu amelengwa kupewa hiyo sehemu, hili suala tuliangalie sana. Mimi nina mfano, kuna kijana wangu anakaa pale *Sea View*, sasa hivi amekwenda kusoma *Masters* yake nje ya nchi; huku nyuma akaletewa barua kwamba arudishe funguo kwa sababu ye ye amehama hakai hapa Tanzania anaishi Uingereza. Ilikuwa ni kwa miezi tisa tu ikabidi niingilie kati kwamba alipewa nyumba hii kwa uhalali na ameeleza kwamba anakwenda kusoma; sasa huyu anayetaka kumtoa anamtoa kwa sababu gani? Vitu vyake vipo mle, analipa kodi na kuna wadogo zake wanakwenda kufagia nyumba yake na vitu kama hivyo. Sasa kama mtu kwenda kusoma ndio unakosa huo upangaji na wakati utarudi si vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo mifano ya namna hii, tuidhibiti tuhakikishe kwamba haki inatendeka na hasa sisi wakubwa isije ikawa sisi Wabunge ndio wa kwanza kwenda kuomba fulani atoke mimi nataka ile *flat* pale, tuwe mfano sisi wa kutenda haki. Watu waliomo ndani wabaki hao hao isipokuwa tu kama watashindwa kwa sababu ambazo zipo wazi kabisa. Mchafuaji wa nyumba kuna utaratibu wa kuweza kumshughulikia huyo.

Muswada huu nadhani tukizungumza tunauchelewesha, mimi naunga mkono tuukamilishe uwe sheria ya kwanza ya utoaji wa hati miliki ya vipande, pamoja na huu wa mikopo ya ujenzi wa nyumba. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, amewasilisha vizuri sana na ninadhani hata kusimamia atausimamia kwa ufanisi wa kutosha. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichukue nafasi hii, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Miswada hii miwili iliyoko mbele yetu. Kimsingi niseme naishukuru sana Serikali kwa kuleta Miswada hii kwa Hati ya Dharura. Nianze kwa kutoa ushauri kwa Serikali kwamba ni kweli Miswada hii imefika kwa wakati muafaka kabisa, ambapo nchi yetu tunatakiwa kutazama suala zima la kuwasaidia Watanzania kuwa na nyumba ambazo watazimiliki kwa manufaa yao. Katika kuleta Miswada hapa Bungeni, basi niseme kidogo kwamba, msukumo huo ungeenda mbali; na zile sheria nyingine ambazo zimepitwa na wakati na zinawaumiza Watanzania wengi basi ziletwe chini ya Hati ya Dharura ziweze kusaidia sana maendeleo ya Watanzania. Zipo sheria mfano za mirathi na ndoa, matunzo kwa watoto, mpaka sasa hivi matunzo ya mtoto ni shilingi 100 tu kwa mwezi, ndio wanatakiwa wapewe katika kulindwa. Nasema tu haya kama mfano, basi hizo Hati za Dharura ziingie hata katika sheria hizo nyingine za kufanyiwa mabadiliko na sheria mpya. Hii ilikuwa ni changamoto yangu tu ya kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme kilichofanywa na Serikali yetu ni kitu cha kupongezwa. Kabla sijasahau ama kabla sijaenda mbele niseme kwamba, ninaunga mkono kwa asilimia mia moja sheria zote mbili; Sheria ya Mikopo Katika Ujenzi wa Nyumba lakini na Sheria hiyo ya Umilikaji wa Vipande kwa maana ya nyumba moja ikaweza kumilikwa na watu zaidi ya mmoja. Nilikuwa nasoma Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2008/2009 na ninaamini kabisa sheria hizi tunapozileta, lengo letu ni kutekeleza kwanza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ambayo kimsingi ni kuwaleta Watanzania maisha bora, ambayo wamekuwa wakiyasubiri kila siku.

Tumeona kwamba, katika mipango hii ya maendeleo kwenye nchi yetu ya Tanzania ni kweli kabisa mipango mingi ilikuwa inaendelea kujikita katika zile sekta ambazo sisi tunafikiri ni sekta kiongozi kama Sekta ya Kilimo, Viwanda na Biashara, Sekta ya Madini, Maliasili na kadhalika. Tulikuwa tunasahau kwa upande mwingine kwamba, Sekta hii ya Ardhi pia ni sekta nyingine ambayo itawasaidia sana Watanzania kuondokana na umaskini na hasa umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kabisa kwamba, katika Mpango huu wa Maendeleo wa Mwaka 2008/2009, mapitio ya mwaka 2007/2008 tuliona ni lazima katika Sekta hii ya Ardhi kuandaa mazingira mazuri ya makazi ya gharama nafuu na endelevu kwa wananchi wa Tanzania. Sasa leo hii Miswada miwili nafikiri ndio inatupeleka katika malengo hayo, ambayo yalikuwa ni mapitio ya mwaka 2007/2008, lakini tunaona kwamba kwa mwaka ule wa 2007/2008, wamiliki 150 ndio walitumia leseni za makazi katika kupata mikopo kutoka katika taasisi mbalimbali za fedha. Sasa ukichukua Wananchi wa Tanzania 150 kwa *population* tuliyonayo ya takriban sasa hivi karibu tunafikia 40,000,000 tuseme. Sasa 40,000,000 kwa Watanzania 150 ambao ndio wana leseni za makazi, zilizowawezesha kupata mikopo na kujiwezesha kuondokana na umaskini na kupata maisha bora kwa kila Mtanzania. Nakubali kwamba, bado tulikuwa tupo nyuma sana.

Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Serikali yetu kwa kuleta Miswada hii. Mimi naamini sasa itaweza kuwasaidia wananchi wengi wa Tanzania angalau katika kutumia hati, kutumia leseni za makazi, kutumia nyumba kuweka dhamana na kukopa ili kujenga nyumba zenyewe. Wanaweza pia wakatumia dhamana hizo katika kujiendeleza zaidi katika maisha yao ya kila siku. Kwa hiyo, ninasema kwa kweli tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme nampongeza sana mchangiaji aliyepita, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Shellukindo. Kimsingi hapa ni kupata picha; je, kanuni na taratibu zitakazotungwa chini ya sheria hizi ndizo hasa zitakazotusaidia kuwafanya Watanzania ambao ndio wenge Muswada, wanaomiliki sheria hii kweli waweze kusaidiwa na kunufaika na sheria yenyewe?

Vinginevyo, tumekuwa mashahidi, sheria nyingi tunazozitunga na hasa kama Watanzania hawatapata elimu ya kutosha, wakatambua umuhimu wa sheria hizi katika kujiletea maendeleo, makundi yale ambayo yanalengwa na wananchi wa chini; wananchi wa vijiji wanaweza wasifaidike na wasinufaika kabisa na sheria kama inavyojikita.

Sasa cha msingi kwanza ni elimu ya kutosha. Mwenyekiti wa Kamati amezungumza na mimi ninakubaliana kabisa hilo lifanyike, Watanzania waelewe vizuri kabisa sheria hizi zote mbili na haki itendeke na ikiwezekana Waziri mwenye dhamana, atusaidie kutunga kanuni ambazo zitawalinda hasa wananchi wenyе vipato vya chini; wananchi wanaoishi katika maeneo ya miji midogo kwa mfano Miji ya Peramiho, Madaba, Mpitimbi, lakini vilevile wananchi wanaoishi kwenye miji mikubwa kama majiji yetu ya Dar es Salaam na maeneo kadha wa kadha. Kwa hiyo, kuwe na uwiano wa kutosha wa kuhakikisha kwamba sheria hii inamlinda kila mmoja kwa nafasi yake na kwa wakati wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme ninaipongeza sana Serikali katika sheria hii na hasa sheria ya mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, tumeona kwamba upo uwezekano sasa wa kuweka rehani hata hayo majengo ambayo yatakuwa yamejengwa. Sheria sasa inatuambia ni lazima kuwe na mashauriano ya karibu kati ya *partners*; mume na mke ili kuwa na makubaliano. Hili ninalipongeza sana, wanawake wengi walipoteza haki zao kwa sababu wanaume walikuwa wanaweka rehani majengo wakati wanawake hawana habari, mwisho wa siku nyumba inauzwa, familia inakosa mahali pa kukaa, watoto wanahangaika lakini hakuna wa kumuuliza inabaki kuwa ni kitendawili. Wapo pia wanawake waliokuwa wanaweka rehani nyumba zinauzwa wakati waume zao hawana habari. Unakuta kabisa baba na yeze hana habari; mama ameshauza nyumba huko alishaweka rehani, basi ilikuwa ni vurugu tupu. Hakukuwa na uwiano wa kisheria kati ya mahusiano haya na hasa ya kijinsia kwenye familia zetu na kusababisha uone badala ya kutumia mikopo hiyo katika kuendelea ilikuwa inaleta migogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nakubali kwamba, sheria hizi zitatusaidia sana na hasa kwenye vyombo vya fedha kama mabenki yetu kutoa mikopo yenyе riba nafuu, itakayowawezesha Watanzania kujenga nyumba. Nikwambie tu kwamba, Watanzania sasa hivi wameamka kiasi cha kutosha na ni kweli kabisa wengi wamegundua; bila kukopa hakuna maendeleo. Mtu usipokopa huwi na mwamko wa maendeleo kwa sababu wewe kila siku utakuwa unajua kwamba, hakuna anayekudai kwa hiyo hata ari ya kufanya kazi inapungua. Usipokuwa na deni ari ya kufanya kazi inapungua sana, lakini ukiwa na deni hulali kabisa, unawaza usiku kucha ufanye nini ili deni lako liweze kurudishwa. Kwa hiyo kama ulikuwa unaamka saa 01.00 utaamka saa 11.00, *automatically* ile saa 11.00 unapoamka utakuwa umefanya kazi za kulipa deni na za kutengeneza faida kwa ajili ya kujenga maisha yako na kujletea maisha bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakubali lakini ni lazima vyombo vya fedha viangalie umuhimu wa kuweka riba zinazoweza kufikika na wananchi wa kipato cha chini na hasa kama nilivyosema wale wa vijijini na kwenye miji midogo. Hatutakuwa na maana kuendelea kutengeneza makazi bora bila kuangalia asilimia kubwa ya wananchi wanaoishi maeneo ya miji midogo na vijijini wakashindwa kufikiwa na mpango huu ambao unaweza ukawasaidia sana. Niendelee kuiomba Serikali ihakikishe kwamba inafanya taratibu hizi zote, leo tutapitisha sheria zote mbili; Sheria ya Umilikaji wa Vipande na Sheria ya Mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

Tumesema sasa hivi tunaanzisha benki itakayoshughulikia masuala ya kilimo, mikopo hii ni lazima iwe ya muda mrefu. Sina uhakika sana, asilimia kubwa ya mabenki yetu Tanzania ni ya kibiashara; sasa sijui tutafanya nini ili kuhakikisha kwamba

tunawezesha kuwa na chombo achilia mbali ushirika ule wa wenyre nyumba uliotajwa kwenye sheria, ambao mimi pia ninahoji ni kwa nini hata ile *committee* haijaundwa kijinsia; imekaa kimya haizungumzi suala la jinsia? Nashauri Mheshimiwa Waziri aiandike vizuri ile *committee* kwa sababu ni lazima iwe na uwiano wa kijinsia ili kuweza kuteta maslahi ya pande zote mbili ama jinsia zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudi upande mwingine, ninasema kwamba, kama mabenki yetu yote ni ya kibiashara; mabenki haya ya kibiashara yanawezaje kukubaliana na hali halisi ya mfumo huu wa sheria tunaouweka ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na urasimu wowote ambao utajitokeza katika kutafuta mikopo? Mimi nadhani hili pia Serikali inatakiwa kulingalia, tumejifunza kwenye mikopo ya JK, mikopo ya uwezeshaji jamii; tulipeleka mikopo kwenye mabenki yetu ya biashara lakini kuna benki nyingine kwa kweli zilionesha kutokuwa na ushirikiano wa kutosha kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu na ilikuwa ni kazi kubwa sana. Ninaamini tukijipanga vizuri tukafanya maandalizi mazuri, mabenki haya yakifikika bila kuwa na matatizo na wananchi wakakopa, kwa kweli wananchi wetu wa Tanzania wataondokana na tatizo la kutokuwa na nyumba, watamiliki nyumba na watakuwa na makazi bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa niyaseme hayo na baada ya hapo kwa kweli niipongeze sana Serikali yetu kwa uamuzi huu. Ninaamini kwa taarifa ijayo ya mapitio ya maendeleo ya hali ya uchumi kwenye nchi yetu, basi wamiliki wa hati za nyumba na wamiliki wa nyumba wataongezeka na idadi ya wamiliki hao katika kumiliki, kukopa na kuendeleza makazi itakuwa imeongezeka, kwa maana ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo kwa ujumla.

Naunga mkono hoja hii na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Miswada hii miwili. (*Makofi*)

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi nichangie katika Miswada hii miwili ambayo ni muhimu sana katika nchi yetu. Kwanza, kitu kinachosikitisha sijui kwa nini imeletwa kwa *Certificate of Urgency* kwa sababu inagusa Watanzania wengi. Waziri amesema ilichelewa ilikuwa itoke miaka mingi iliyopita, kwa hiyo, Serikali ilikuwa inajua hii haja ipo, sasa sababu ya kuichelewesa mpaka leo halafu sasa hivi inatolewa wakati tuna matatizo ya mafisadi walioiba pesa wakajenga *flats* ambazo zinataka sasa kugeuzwa kwenye *units* zihalalishwe ziuzwe; ni hatari sana! (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mzee Ndesamburo, una ushahidi?

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Naam?

NAIBU SPIKA: Una ushahidi kwamba ndio madhumuni ya sheria hii?

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Naibu Spika, hapana. Madhumuni ya sheria hii ni kuwasaidia wananchi wapate pesa. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Basi tuendelee.

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ni mfano. Sasa jambo la pili, nadhani tusichanganye mambo mawili; *mortgage* maana yake una *mortgage something* kwenye pesa upate. Kwenye *mortgage* ni lazima pawe na kitu tayari, *mortgage* haina maana ya kwenda kukopa pesa ukajenge, naomba lieleweke hilo maana yake kuna wengine wana-*confuse* ku-*mortgage* na kujenga. Unapokwenda kuchukua pesa za kufanya *mortgage* ni lazima pawe na kitu ambacho unaki-*mortgage* ndio uweze kupata zile pesa, kwa hiyo tuelewane katika hilo, sio pesa za kwenda kujenga nyumba. Sasa hivi watakaojenga nyumba hizi za kuchukulia *mortgage* ni matajiri wakubwa, ambao watakuwa wanakopa kwenye mabenki wajenge majumba halafu *units* zile ndogo ndogo ndio sisi maskini wadogo wadogo tutakwenda kununua kule. Nadhani hilo linaeleweka na ndilo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa majumba ya kisasa ambayo yana-*qualify* kwenye mabenki haya ni nyumba ambazo ni ghali sana. Niambieni Mtanzania wa kawaida au Mfanyakazi wa Serikali ni nani anayeweza kununua *unit* kwenye maghorofa ya Dar es Salaam kwa dola 200,000 au 300,000? Hakuna. Tunawajengea mabepari wazidi kuishi katika nchi yetu. Tunawaleta wenyе mabenki makubwa ambaо ndio watajenga hizi nyumba, haya mabenki sio yetu ni ya nje faida yote itatolewa nje. Nchi hii itabakia na faida gani?

Serikali ingeniambia ya kuwa *registrar of building* ni pamoja na *National Housing*, nadhani hiyo ni moja siku hizi, ingekuwa ndiyo hiyo itakayojenga haya majumba halafu ikauza hizo *units* kwa watu, hapo ningelewa. Tutazidi kuinyonya nchi hii iishiwe isiwe na chochote, kwa sababu hawa ambaо watakuja kujenga haya maghorofa ni matajiri wakubwa, wenyе pesa nyingi na watakopa pesa katika mabenki makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *mortgage* ina matatizo; misingi ya *mortgage* mtikisiko wa dunia ya sasa. Uchumi wa Uingereza upo kwenye matofali na ile simenti inayokamatia na yote ni mambo ya *mortgage*. *Mortgage* kama isiposimamiwa vizuri, wale wanaotoa *mortgage* wanaweza kuja kuutikisa uchumi wetu tusipokuwa waangalifu. Waswahili wanasema; mwenzako akinyolewa na wewe nenda katie maji; tikisiko lililoko duniani sasa hivi limeanzia kwa Stanley Morgan, nenda *Northern Rock* kule Ulaya ndio hao shauri ya *mortgages* ambazo nyingine zimejengwa nyumba hazipo na hayo yanaweza kutokea hata hapa Tanzania.

Mimi sioni ajabu kwa sababu ni haya haya mabenki yaliyofanya madhambi huko nje ndio yatakayokuja hapa kutukopesha sisi tupate *units* na mwisho wake zile *units* watakuja kuzichukua. Sheria hii inasema wewe una *unit* yako, labda baada ya miaka mitatu, mine, ukishindwa ukapelekwa mahakamani hata *appeal* huna. (*Makofi*)

Huwezi kwenda ku-*appeal* kwenye *court* ya juu ili angalau hata ufaidike; hii ni hatari kabisa. Mimi naiunga mkono hoja sio kwamba naipinga, lakini jaribu kuonyesha

matatizo yatakayowafika Watanzania. Kwa hiyo, wakati atakapotunga *regulations* au utakapoleta *amendment* katika *bills* hizi, lazima mambo haya tuyaweke wazi sana ili watu waelewe ni nini kinachohusika katika hili.

Katika hizi *units* unakuwa na ghorofa moja kubwa, lenye *flats* karibu 40, mtu anajenga anaanza kuuza *flat* moja moja na pana *title deed* moja ya ardhi pale chini. Katika *appeal* tunasema *title deed* moja tutaikata vipande kufuatana na maghorofa yaliyopo kule juu, yaani wote ni *common* tuna *own title deed*. Mimi ninge-*propose* mwenye ardhi anayewajibika kulipa *land rent* awe ni mmoja; mwenye *title deed*. Itaondoa utata kwa sababu hata unapokuja kwenye mambo madogo madogo, inakuwa ni vigumu kuwafuata watu 40 badala ya kumfuata mtu mmoja ambaye unamaliza kazi yako pale pale. (*Makofi*)

Ni mawazo tu ambayo wenzetu wa nje wanayatumia, sio lazima myachukue na si vibaya na sisi vilevile tukiyatumia kama inawezekana. Tatizo lingine ambalo ningeomba hii Wizara iliangalie katika ku-*implement* hizi *bills*; kuna watu wanakaa katika nyumba za *National Housing* na wamelipa kodi ambayo imeshazidi *value* ya ile nyumba; tunawafikiriaje watu hawa kuwapa *ownership* ya hizi *units* au kuwapa *discount* kwa sababu ya muda ule waliokaa pale? Kama hatutawafikiria hawa watu, kwa kweli tutakuwa hatuwatendei haki.

Ninadhani Mheshimiwa Waziri angelifikiria jambo hilo, maana yake tukiwaachia wajenzi wa hizi *units* wakawa ni watu wanaotoka nje, wananchi wetu watakuja kufukuzwa mjini halafu mji utakuwa wa wageni au utakuwa mji wa watu wenye uwezo, maskini hawataweza kujenga. *National Housing* iliingia katika kazi hii ikajenga hizi *units* kwa ajili ya wafanyakazi, pamoja na wengine ambao wana uwezo kidogo, halafu tukaiacha tu ikaenda kwenye *commercial price*, yaani katika mazingira ya kifaida ya biashara hii, hili tumewatengenezea watu wachache sana. *Less than one percent* ya Watanzania, hata one percent haiwezi kufika, watu wachache sana ambao watafaidi hiki kitu; wakulima na wakaaji wa vijijini hakuna hata mmoja ambaye atafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza nikasema tusijenge tabaka la watu ambao wataishi vijijini kwa sababu watakaoishi mjini ni wale watakuwa na uwezo wa kununua hivi vipande; watu wenye pesa na ni wafanyakazi wa Serikali wala mfanyakazi yeoyote hataweza kununua. Kwa kuwa nyumba za mjini ni ghali sana na huwezi kuniambia hata ukimpa *a long term for repayment* iwe miaka 50 haiwezekani, *maximum* labda itakuwa miaka 30; uhai wa mtu, lazima utazame hata kumlipa deni haitawezekana. Lazima tutafute namna ya kumfanya Mtanzania wa kawaiida awe na faida na aweze kufaidi. Kama tutaweka shirika au tutakuwa na mabenki yetu wenyewe, tusitumie mabenki ya nje kwa kuwa tukiyatumia yatatukamua na kupeleka nje, lakini tukiunda benki ambayo itakuwa inakopesha pesa hizi kwenye *mortgages*, labda hapo tutaondoa hilo tatizo.

Kwa kuwa mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati iliyochambua Muswada huu, sina mengi zaidi ya hapo, isipokuwa naunga mkono hoja. Nadhani haya machache

niliyoyazungumza tutayazingatia ili Watanzania wote kwa ujumla wao, waweze kufaidika kwa *bills* hizi mbili. (*Makofî*)

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika Miswada hii miwili. Nianze kwa kusema, naiunga mkono yote. Napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Miswada kwa *Certificate of Urgency* ili tusiendelee kuchelewa, tumechelewa vya kutosha ilitakiwa Miswada hii ipite miaka mingi iliyopita kutuwekea utaratibu wa kutekeleza haya mambo mazuri yanayopendekezwa katika Miswada hii. Kutokana na muda mwingi kuwa umepita, basi Serikali ikaona ni muhimu kuleta kwa *Certificate of Urgency* ili tuufanyie uamuzi na tuwezeshe sasa mambo mazuri kutekelezwa.

Kwa upande wa hii *Unit Title Act*, mimi nina machache sana ya kusema; Muswada huu sasa unatuwekea utaratibu utakaowezesha watu kujenga majumba makubwa yenye *flats*, ambayo yatauzwa kwa mtu ambaye atayamiliki kisheria ni utaratibu mzuri sana na ninaupongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu utatusaidia, watu wenye mapesa yao watajenga majengo makubwa sasa na yenye *flats* za kupangisha na hivyo kufanya upatikanaji wa nyumba uwe mzuri zaidi katika miji yetu. Huu ni utaratibu mzuri sana utatuwezesha kutumia vizuri zaidi ardhi yetu kuliko tunavyofanya hivi sasa. Wale wanaolifahamu Jiji la Dar es Salaam, sasa hivi limeshajaza mkoaa wote na linaendelea kujaza Kibaha na Bagamoyo. Utaratibu huu utatuwezesha kujenga majengo makubwa, yenye *flats* nyingi katika ardhi iliyopo na kwa hiyo, tutatumia vizuri ardhi yetu na kupunguza kukua kwa kasi kwa miji yetu.

Baada ya hayo machache, naomba niende kwenye huu Muswada mwagine wa mikopo na rehani.

Mimi naomba nikubaliane na utaratibu wa kuyawezesha mabenki na vyombo vya fedha, kukopesha na kuwa na hakika ya kulipwa. Muswada huu ni mzuri sana, kwa sababu unatuwekea utaratibu utakaotuwezesha kujengae utamaduni wa kukopa na kulipa. Ningombaa ihakikishwe kwamba, wakopaji wanalindwa pia katika utaratibu huu. Kwa mfano, sasa hivi ukikopa kutoka kwenye mabenki, mali zako zinauzwa wakati mwagine kwa minada ya hadhara. Mara nyingi sana ile thamani ya mali inayohusika haizingatiwi, mtu ana nyumba yenye thamani pengine ya shilingi 50 milioni, inauzwa kwenye mnada kwa shilingi milioni kumi anapata hasara ya shilingi 40 milioni! Kwa hiyo, tunaomba Sheria ihakikishe kwamba, ile mali itakayouzwa itauzwa kwa kiwango kinachofanana na thamani yake na sio kuuzwa tu ili benki ipate fedha zake. Mimi nimeona katika Miji ya Dar es Salaam na Iringa nilipokuwa kufanya kazi, nyumba za watu zilikuwa zinauzwa na dalali anapita kwenye mji akitangaza nauza nyumba ya fulani njooni kwenye mnada nitakuuzia kwa bei nafuu, lakini huyo mtu ananunua kwa bei nafuu ni hasara kubwa sana na bei kubwa sana kwa mwenye nyumba. Kwa hiyo, hili ningombaa lizingatiwe katika sheria.

Nafikiri katika kifungu cha 17 cha sheria hii, kuna kipengele kimewekwa chini ya *section b* kinachosema kwamba, Mahakama inaweza ikamruhusu mtu auze male yake, kama bei itakayopatikana itawezesha kulipa deni na kufanana zaidi na mkopo ambao ameuchukua. Hili lilitakiwa liwe ndilo utaratibu kwamba, mali inapouzwa inauzwa kwa thamani yake, kiasi cha fedha kichukuliwe kulipa deni na kiasi cha fedha kitakachobaki kama kitabaki apewe mkopaji badala ya kuuza tu kwa lengo la kupata pesa za kulipa deni.

La pili, ambalo linanistusha sana ni hili la riba, una kopa kwenye benki wakati riba ni asilimia 15, baada ya muda benki inaanua kupandisha riba kuwa asilimia 20. Maana ya kubadilika kwa riba ni kwamba, kiasi unachotakiwa kulipa kimeongezeka badala ya kuwa kiwango kile mllichokubaliana kitaongezeka sambamba na kuongezeka kwa riba.

Sasa ingebidi basi mkataba ujadiliwe upya, mkopaji na mkopeshaji wakae wakubaliane upya, juu ya utaratibu wa kulipana na jinsi ya kuzingatia hiyo riba ilioongezeka. Usipofanya hivyo ni kwamba, huyu mkopaji atafika mahali atashindwa kulipa, kwa sababu hakuwa amejiandaa kulipa kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sheria hii iangalie hilo na iweke utaratibu sasa utakaohakikisha kwamba, riba itakapobadilika kunakuwepo *negotiations* mpya za utaratibu wa kulipa huo mkopo. Isiwe tu kwamba, huyu mtu anabanwa na akishindwa mali zake ziuzwe kwa sababu maskini ni wengi sana watapoteza mali zao kwa utaratibu huu.

Lingine ambalo ningeomba niligusie ni hili la kukopa, mathalani unakopa ukajenge nyumba, sasa inawezekana huna mali nyingi za kuweka rehan; kwa nini hiyo nyumba unayojenga isiwe ndiyo rehani yenye kwa sababu pesa ulizochukua umejengea na kwa hiyo nyumba iwekwe rehani kama utashindwa kulipa iuzwe na si nyumba nyingine ambayo ipo mahali pengine. Tungeomba sana Mheshimiwa Waziri alitazame hili na kuangalia ni jinsi gani linavyoweza kuzingatiwa katika Muswada huu.

Lingine ambalo limenipa tabu kidogo ni hili la kwamba, unapotaka kukopa ni lazima ueleze kama una *spouse* au huna. Inazungumzia *spouse* mmoja, Watanzania wengi wana wake wawili au zaidi, sasa ukienda kutangaza una *spouse* mmoja wakati kuna wengine watatu ndani hao watatu; wanazingatiwaje? Unawenza ukachukua yule ambaye unajua hana matatizo ndiyo ukaenda kumwonyesha kwamba, nimeoa na mke wangu ndiyo huyu kumbe ile mali sio ya mke huyu ni ya mke mkubwa ambaye hukumleta. Sasa sheria inazingatiaje tatizo hili kuhakikisha kwamba, yule mama ambaye ndiye aliyeshiriki katika uzalishaji wa mali ile ndiye atakayefikishwa kwa mkopeshaji ili akubali ama akatae hiyo rehani. Tusipofanya hivyo, tunaweza kufika mahali tukakuta kuna utapeli mwingi sana na wenye matatizo makubwa kwa wanaohusika.

Hapa napenda nisisitize kwamba, katika familia zetu mali ni ya mume na mke ama wake zake. Kwa hiyo, anapoamua kwenda kukopa na kuweka rehani mali zilizopo ni lazima awashirikishe hawa wengine ambao wameshiriki katika uzalishaji wa mali hizo.

Sheria basi iseme hivyo, maana haisemi kwamba hawa watatakiwa wapewe ridhaa. Inasema utatangaza tu kwamba una mke na mkopeshaji atakwenda kuchunguza na akiridhika basi mambo yamekuwa sawasawa. Huyu mke angetakiwa atoe ridhaa kwamba ukopaji huu naukubali na kwa hiyo uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na hayo machache, naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu, ambao kama ambavyo wachangiaji wengine walivyosema, tena wazee wazoefu kabisa; katika masuala ya kiuchumi katika taifa letu na masuala ya kibiashara na vilevile kufuatia mchango wa Msemaji Mkuu wa Kamabi ya Upinzani kwa Wizara hii, nilikuwa na mambo kadhaa ya kuweza kuchangia katika Muswada huu.

Kimsingi Muswada wa *Mortgage Finance* ni kitu muhimu na nataka kutofautisha kati ya hiyo; *mortgage finance* ni Muswada ambao umeletwa na kimsingi sipingani na uamuzi wa Serikali wa kuuleta Muswada huu sasa. Lakini kama ambavyo wengine wamesema, nina mashaka na kuletwa kwa Hati ya Dharura, kwa sababu Muswada huu haukupata mjadala mpana katika jamii, ingawa madhara yake katika jamii ni makubwa sana lakini tayari Muswada umekuja na hakuna jinsi lazima tuujadili ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto, naomba ukae. Wewe ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi. Kanuni ya 80(4) inasema hivi; Muswada wowote wa Sheria wa Serikali wa dharura hautaingizwa kwenye shughuli za Bunge bila ya kuwa na hati iliyowekwa saini na Rais inayoeleza kuwa Muswada uliotajwa katika hati hiyo ni wa dharura. Kanuni ya (5) inasema; Muswada huo utawasilishwa kwanza kwenye Kamati ya Uongozi ukiwa umeambatanishwa na hati ya dharura ili Kamati hiyo iweze kujiridhisha iwapo Muswada husika wa sheria unastahili kuwasilishwa kwa dharura au la. Kabwe ye ye ni Mjumbe wa Kamati, tumekaa jana tukakubaliana, kama tusingekubaliana tungekataa sisi kule. Kwa hiyo, wengine nakubali kwa sababu hatujawaambia kwa nini sisi tulikubali, kwa hiyo naomba uendelee kujadili. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wakati mwingine uwe unasubiri Wabunge wamalize, kwa sababu naomba unisikilize ...

NAIBU SPIKA: *No! No!* Mimi nasema kwa sababu tumekaa kwenye Kamati ya Uongozi sisi ndiyo wenyewe. Pamoja na ye ye, Wabunge wengine wana haki ya kusema hivyo kwa sababu hawajaambiwa kwa nini tulifanya hivyo. Tuliopitisha Muswada huu kwamba uje hapa ni sisi Kamati ya Uongozi; Mheshimiwa Zitto ni Mjumbe wa Kamati hiyo. Tusiwfanye watu waelewe kwamba ni kitu ambacho si sawa sawa. Tumepitisha kwenye Kamati ya Uongozi kwa mujibu wa Kanuni. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia kusema kwamba, sijapinga Muswada na wala sijapinga Hati ya Dharura; ninaelezea mashaka ambayo yatachangia kwa sababu haina maana kwamba, Muswada huu tukiupitisha

hautaboreshw. Wabunge wanapochangia haina maana kwamba, kile wanachochangia kitarekebishwa leo, yatachukuliwa maoni na Serikali itaweza kuboresha. Ndiyo jambo ambalo nilikuwa nalizungumza na kama ungenipa fursa nikazungumza mpaka mwisho, kwa vyovoyote vile ningesema hivi ninavyosema. Ndiyo maana nikasema kwamba, wakati mwingine ni lazima utoe fursa Wabunge kumaliza kile ambacho tunakizungumza.

Sasa taswira ambayo umeijenga kwa jamii ni kwamba, mimi naenda kinyume na maamuzi ya Kamati ya Uongozi, kitu ambacho si kweli kwa sababu nilikuwa sijamaliza kile nilichokuwa nakizungumza. Kwa hiyo, nadhani ungeniachia tu haki yangu ya kuzungumza nikamaliza *then* ukatoa mwongozo ambao unautoa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto, tusibishane ndani ya Bunge; tunajua wote ni mafundi wa kuzungumza. Tunachokisemea hatukatai maudhui ya Muswada lakini unapo-*challenge Certificate of Urgency* kama Mjumbe wa Kamati ya Uongozi, ndicho ninachozungumza mimi kwamba, wewe ungeendelea na maudhui tunaruhusu kabisa. Nataka uzungumzie maudhui ya Muswada ndiyo maana nimekupa nafasi.

Wabunge wengine sikuwaliza kwa sababu wao hawakushiriki kwenye Kamati ya Uongozi ya kukubali kwamba Muswada huu uje. Tunaomba tusiwa-*misguide* wananchi. Wabunge wengine si Wajumbe Kamati hiyo na hivyo kama sisi Kamati ya Uongozi tungekataa, hata kama *certificate* ingekuja pale sisi tungekataa. Tulikaa tukakubaliana jamani sawa ipite wakasema upite, ndivyo tulivyofanya naomba tusiendelee kubishana endelea kujadili. Jadili Muswada lakini siyo *argument* hiyo.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, *I did not challenge Certificate of Urgency and I am not challenging it.*

NAIBU SPIKA: Naomba uchangie Muswada au nimwite mtu mwingine kujadili?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo mwanzo kwamba, Muswada huu ni muhimu sana katika uchumi wowote unaokua na ukiangalia takwimu za ukuaji wa uchumi utaona kwamba *real estate* kwa maana ya *construction sector* ni moja ya sekta ambazo zinakua sana. Wananchi wengi sana hivi sasa wanajenga nyumba zao kwa kutumia *cash*. Kwa hiyo, tumejikuta tunaendesha uchumi kwa *cash economy*, kitu ambacho siyo kizuri na kinapaswa kuondolewa ili kuhakikisha kwamba watu wote hata kama mtu hana uwezo wa kujenga nyumba leo, awe na uhakika kwamba akifanya kazi miaka kumi anaweza akapata nyumba.

Sasa tatizo ambalo tunalionia katika *real estate* ya Tanzania ni kwamba, haina *regulation* kwa hiyo, kila mtu anaweza akaamua leo akawa na *real estate company* hakuna *regulator* yeoyote, yaani chombo ambacho kinadhibiti masuala ya sekta hii ndogo ndani ya sekta ya ujenzi wa nyumba. Kwa maana hiyo, naamini kabisa kwamba, Serikali hii kupitia Sera yake ya Nyumba na Sera ya Makazi, inaweza ikaangalia uwezekano wa kuweza kufanya marekebisho ya sheria zinazohusika ili kuweka chombo ambacho

kitakuwa kina-regulate sekta ndogo ya *real estate*. Hicho ndiyo kitu cha msingi ambacho nilikuwa nataka niweze kukizungumzia kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi uchumi wetu umegawanyika katika sehemu mbili; tuna *rural economy* na *urban economy*. Tunapozungumza ya kwamba, uchumi wa taifa unakua na takwimu ambazo zinatoka, kimsingi *urban economy* ndiyo inayokua na hata sheria hii ambayo tunaitengeneza itajibu matatizo ya uchumi wa mijini kwa maana ya *urban economy*, kwa sababu sekta ambazo zinakua hivi sasa zinahusiana moja kwa moja na watu ambao wanaishi mijini. Hata ukiangalia *trend* ya michango ya wachangiaji wengi, utakuta kwamba suala la *mortgage* litasaidia zaidi wakazi wa mijini. Hili ndiyo suala ambalo ningependa Wizara ya Ardhi iweze kuliangalia, kwa sababu tunaacha sehemu kubwa sana ya wananchi kwa maana ya *rural economy* na hakuna mtu anayehusika na sekta hii na hakuna mabenki ambayo yanaweza yakaenda kuwekeza katika maeneo ya vijijini. Kwa sababu *rural economy* hivi sasa ina-*stagnate* kwa sababu *rural economy* kwa kiasi kikubwa inategemea sekta ya kilimo na sekta ya kilimo kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita haikui ipo pale pale kwenye asilimia 4, asilimia 4.1 asilimia 4.3; ukuaji wake haujazidi asilimia 4.3.

Kwa hiyo, shughuli za uzalishaji mali, shughuli za kilimo na uwezekano wa wananchi wa vijijini kupata mapato haupo. Mtakumbuka pia kwamba, masuala haya ya *mortgage* yamekuwa yakijadiliwa kama sehemu ya *Second Generation Financial Sector Reforms* na mmoja wa Wabunge hapa Mheshimiwa Mrema, Mbunge wa Arusha Mjini, amekuwa askari wa mbele sana katika kulieleza suala hili. Lakini bado hatujaweza *ku-deepen financial sector* katika maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, Muswada huu haujaweza kufafanua ni vipi ambavyo tutaweza kulieleza suala hili. Njia pekee ya kulifanya suala hili la *mortgaging* na *real estate* kuweza kuendelea vijijini ili wananchi wa vijijini nao pia wawe na nyumba nzuri na wawe na unafuu wa suala la ujenzi wa nyumba ni kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ndiyo maana kwenye nchi nyingine kuna nyumba za Halmashauri (*Council Houses*), kwa sababu mabenki hayawezi kujenga nyumba na *ku-mortgage* kwa wananchi. Kwa hiyo, Halmashauri katika maeneo ambayo siyo mijini ndiyo ambazo zinapaswa kuwa na jukumu la kuweza kuhakikisha kwamba wananchi kule wanapata nyumba ambazo ni nzuri.

Kwa hiyo, napenda Wizara ya Ardhi iweze kuangalia uwezekano kwa dhati kabisa na zoezi hilo lingeanza mapema iwezekano, kuona jinsi ambavyo Mamlaka za Halmashauri za Wilaya zinavyoweza kushiriki katika mchakato huu mzima wa *mortgaging* ili kuweza kuhakikisha kwamba, wananchi wa vijijini nao wanaweza kupata nyumba. Wananchi wa Vijijini wana mapato yao yanayotokana na kilimo. Halmashauri zinaweza zikawa na *register* ya wakulima na kuweza kujua kama huyu mtu analima kahawa Kalinzi, anapata kiasi gani kwenye kahawa yake na anaweza akalipia vipi mkopo huu ambao ameuchukua kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nzuri. Kwa hiyo, nilikuwa naomba changamoto hiyo Wizara ya Ardhi iweze kuichukua katika uboreshaji wa baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ambalo nataka kulizungumza na watu wengi wamelizungumza ni kwamba, *mortgage* ina madhara yake ambayo ni kama haya

tuliyoyaona hivi sasa katika Masoko ya Kimataifa. Mmesikia juzi juzi Marekani imenationalize mabenki yake ambayo yalikuwa yanatoa *mortgage*. Kampuni kubwa kama Fred Mine na Fred Mark zimefilisika na Serikali ya nchi zao imeweza kuzichukua. Inaunda makampuni ya umma kwa muda huu. Kwa hiyo, wanarudi kwenye Serikali kumiliki makampuni. Muswada huu baadaye uweze kuangalia uwezekano wa kuwa na chombo cha umma ambacho kinaweza kikafanya shughuli za ukopeshaji. Najua huko nyuma tulikuwa tuna Benki ya Nyumba ikafilisika; sababu za kafilisika kwake kwa vyovoyote vile Serikali inazijua.

Tunaweza kuangalia uwezekano wa kuwa na *Housing Bank* ya Umma, ambayo inaweza ikatumika kwa shughuli za ukopeshaji wa nyumba kwa wananchi. Vilevile tuangalie uwezekano hata kama hatutakuwa na shirika ambalo Serikali inalimiliki asilimia mia moja, tunaweza kuwa na shirika ambalo Serikali ina hisa ili tujifunze kutokana na matatizo ambayo yametokea hivi sasa katika masoko mbalimbali duniani. *Credit crunch* iliyotokea kwa kiasi kikubwa imesababishwa na *real estate*, kwa sababu watu wameshindwa kulipwa na wamenyang'anywa nyumba zao ambazo wamekaa nazo kwa muda mrefu; na walionyang'anywa nyumba ni watu maskini zaidi.

Kwa hiyo, ni vizuri kuweza kuliangalia na labda inaweza ikaingia kwenye *regulation*. Waziri anaweza kuliweka kwenye kanuni za utekelezaji wa sheria hii ili kuweza kuona jinsi gani litatekelezwa.

La mwisho kabisa, kwenye sheria hii sijaona nafasi ya Benki Kuu, kwa sababu kwa sehemu kubwa hii ni mikopo na ni mikopo ya *kibenki*. Sijaona na wala sijapata fursa, kwa sababu imekuja kama Hati ya Dharura ya kuweza kulinganisha mabadiliko haya ya Sheria ya *Financial Institutions Act* na Sheria ya *Bank of Tanzania Act*, ambazo tumezipitisha mwaka 2006. Kuna mahusiano ya namna gani; ni maeneo yepi ya sheria hizi yanaweza yakafanyiwa marekebisho ili kuhakikisha kwamba sekta hii ya ujenzi wa nyumba inadhibitiwa vizuri?

Imeonyesha kwenye Muswada huu kwamba, kanuni zitaandikwa na Waziri wa Ardhi, hakuna maeneo ambayo kuna *role* ya Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, hilo nalo lingepaswa liweze kuangaliwa kwa sababu hii ni mikopo, mwisho wa siku taasisi zinazokopesha zitatumia Sheria ya Benki Kuu na Sheria ya Taasisi za Kifedha. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali pia hilo suala siku za usoni iliangularie, kuweza kuona ni vipi ambavyo Benki Kuu inashiriki katika hili ili kuweza kudhibiti madhara ambayo yanaweza yakatokea baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi naunga mkono Muswada huu, lakini nilikuwa naomba mambo haya yaweze kuangaliwa ili kuweza kulinda wananchi kwa sababu siku ya mwisho *mortgaging* inaweza ikajikuta inawafaidisha matajiri kuliko maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

MHE. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii adhimu katika kuchangia Miswada miwili iliyoko mbele yetu;

Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Miliki za Sehemu za Majengo na Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Nyumba yote ya mwaka huu wa 2008. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nazidi kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu Muswada wa kwanza wa Sheria ya Utoaji wa Miliki wa Sehemu za Majengo, naomba nizungumze mambo machache yafuatayo, ambayo kusema kweli kipekee nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu nzima iliyohusika katika kutuletea Muswada huu mzuri. Miswada hii yote imekuja kwa *Certificate of Urgency* kutokana na ule umuhimu wake na ni katika ile nia na dhamira njema kabisa ya Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi katika kuleta ukombozi kwa wananchi wake. (*Makofi*)

Hapa tunachotaka kusema ni kwamba, tunataka kudhihirisha mojawapo ya hatua ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Kwa hiyo, niipongeze pia Serikali kwa hatua hii tulioifikia hivi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme katika hali hii, Mheshimiwa Mhagama amezungumzia kwamba, tunayo mambo mengine ndani ya nchi yetu ambayo pia tunaweza kuyaleta kwa Hati za Dharura. Ningependekeza tuweze kutumia nafasi hiyo tulete sijui tutakuwa tunaita ni Muswada huo mwingine lakini katika kuiwezesha Benki yetu ya *TIB* ambayo Mheshimiwa Rais ameshasema, kuna fedha zitapelekwa pale kusaidia kilimo. Kwa hiyo, hicho tuweze kukifanya nacho tukilete katika Hati ya Dharura ili wananchi wetu kuanzia mkulima mdogo au yule wa kat, naye aweze kuwezeshewa katika kilimo chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho naweza nikakisemea, huu Muswada wa kwanza utatusaidia katika mipango miji yetu katika usafi wa mazingira na hatimaye kuongeza kiwango cha ustaarabu katika maisha ya Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo ambalo Mataifa yaliyoendelea yanafanya na hata yale Mataifa mengine ambayo yalikuwa nyuma kama sisi, yameweza kutumia utaratibu kama huu na hatimaye kuwasogezza wananchi wake maendeleo ambayo leo tunachukulia kama ni mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho nitakisisitiza hapa katika taaluma ni umuhimu wa nidhamu ya *industry* nzima ya *construction* kwamba, Mheshimiwa Basil Mramba alionyesha wasiwasi kwa mfano yale majengo yanayodondoka. Nitaomba sheria hii na sheria nyingine tulizonazo; katika ubora wa majengo tuliyonayo au majengo ambayo yatakuwa yanajengwa kwa kusudio la kukodisha kwa wananchi, sheria iwe kali na usimamizi wake uwe mzuri sana ili kusiwepo na utapeli kwamba mtu amejenga majengo yaliyo chini ya viwango, akijua kwamba kesho na keshokutwa anapokwenda kuyauza au kupangisha watu, atakuwa ameshajivua lawama. Kwa hiyo, nitaomba hizi sheria zetu zote tuweze kuzitumia vizuri kwa maana ya kumlinda pia na yule anayeenda kupangisha au kuuziwa ile nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba pia tuyasukume na kuyataka mashirika yetu mfano *National Housing* na hii Mifuko ya Kijamii, ndio iwe vinara katika kazi ya kuweza kujenga nyumba na kukodisha au kuuza kwa wananchi wetu. Hii itatoa ile dhana au wasiwasi uliopo kwamba ni watu wachache wameandaliwa ili wafaidike na hii Miswada, lakini tunayo mashirika muhimu sana na ambayo tayari yanafanya kazi kama hizi. Kwa hiyo, ningeomba pia tuyasukume na kuyashawishi au kuyataka yawe ndio vinara katika shughuli nzima hii ya ujenzi wa kujenga za kukodisha, pamoja na kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize tu umuhimu wa elimu kwa umma; ni vizuri tutoke hapa na tumtake Mheshimiwa Waziri, aweke mikakati thabiti ya kwenda kuelimisha umma juu ya hii Miswada miwili. Miswada hii ni muhimu sana lakini isipoeleweka vizuri kwa wananchi wetu, itatia shaka kwa hiyo nisisitize elimu kwa umma kwenye upande wa *mortgage finance*; utoaji wa mikopo kwa majengo au nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi bora ni haki ya kila mwanadamu, ubora ninaouona au uzuri wa hii Miswada miwili itatusaidia sana kupunguza kasi ya vijana ambao wanaajiriwa siku za karibuni, hawana uhakika wa kuwa na nyumba wala uwezo wa kupanga. Maadam watakuwa na ajira inayotambulika, itawapa uhakika kwamba wanawenza kupanga nyumba na baada ya muda nyumba zile zikawa ni zao. Niseme kwamba, itakuwa ni kitu; nitumie neno gani; ni kupunguza ushawishi wa vijana kushawishika kupokea rushwa au kutaka rushwa kwa sababu sasa mtu anaanza maisha yake akiwa kijana kama Mzee Shellukindo alivyotangulia kusema, lakini una uhakika kwamba, utaweza kupangisha ile nyumba na baada ya muda ile nyumba inaweza kuwa yako, yaani utamilikishwa ile nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kwamba, huu Muswada pia utatusaidia katika kilio kingine kikubwa tulichonacho cha baadhi ya watu kushawishika kutaka rushwa ili kuwa na uhakika wa kuwa na makazi. Cha kushangaza ni kwamba, Tanzania ni nchi mojawapo kabla ya huu Muswada tunaoupitisha hapa leo ambao mtu unalazimika kujenga nyumba yako kutoka mfukoni mwako asilimia 100, sasa niambie ni Mtanzania gani au kwa mshahara upi, ambaye atawenza kujenga nyumba yenyе thamani labda ya milioni 50, milioni 100, milioni 150 au milioni 200 wakati huo watoto wake wakiishi na kuendelea na maisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninashukuru sana huu Muswada umekuja kwa wakati muafaka, tena niseme ulikuwa umechelewa kidogo. Kwa hiyo, hatuna muda mwingu wa kuuchelewesha, niungane na wenzangu waliotangulia kuunga mkono nami ninaunga mkono haraka sana tuweze kuupitisha. Ninaomba zikawe sheria na tuanze kuitumia haraka iwezekanavyo, itatusaidia katika mambo mengi sana na nasema hii itakuwa ndio tiba ya tamaa au wale wanaotaka kuhongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri wa sheria ni kule kuondoa urasimu au mlolongo mrefu katika kupata mikopo. Tunapoweka rehani majengo yetu au vitu vingine katika ku-*mortgage* ule utaratibu wa zamani, mlolongo mzima wa kwenda mpaka kwa Kamishna wa Ardhi aweze kuweka saini na vitu vingine hautakuwepo. Kamishna wa

Ardhi atakuwa anapewa taarifa tu, hapa kuna *title* yako ulioitia saini imekuwa-*mortgaged*, kwa hiyo, niseme kwamba itaharakisha shughuli zetu za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba tu wale watu ambao wamezoea kuishi katika hali ya ubabaishaji ya kusema kwamba nitaenda kukopa pesa hapa ili kesho na keshokutwa nikaweke *court injunction*, ninapoanza kudaiwa wajue kwamba, nafasi hiyo haitakuwepo. Ukitoma Miswada yote miwili, inaweka bayana ubabaishaji wa kwenda kuchelewesha baada ya kutokuweza kulipa deni hautakuwepo, maana yake kuna watu wamezoea kukopa pesa inapofikia muda wa kulipa basi *court injunction*. Ninashukuru sana kwamba, kipengele hicho kimeonekana na kimepewa umuhimu, labda kwa sababu nipo kwenye Kamati iliyosughulikia huu Muswada; nimtoe wasiwasi kijana mwenzangu Mheshimiwa Zitto Kabwe kwamba, Benki Kuu imehusishwa. Mheshimiwa Waziri, tulimuuliza hilo swalii na akatuhakikishia kabisa Benki Kuu itakuwa ina-regulate, haya mabenki yatakavyokuwa yanatoa hizi pesa ili kuondokana na dharura au na balaa kubwa iliyotokea huko Marekani kwamba, taasisi za kifedha zisije zikatoa mikopo kupita uwezo wake. Mheshimiwa Waziri, ninamshukuru kwamba aliweza kutufafanulia, kwa hiyo nitoe wasiwasi pia na wale wote ambao walikuwa wana wasiwasi kama huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatangulia kusema kwamba, ninaunga mkono Miswada yote miwili na niombe tusipoteze muda mwingi tuweze kuipitisha haraka iweze kwenda kufanya kazi. Namshukuru Mheshimiwa Waziri pia ameweza kutuhakikishia Miswada yote miwili itatafsiriwa katika Luga ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi wetu wote kupata uelewa wa hii Miswada miwili tunayoipitisha leo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru na kukupongeza kwa kazi nzuri uliyoifanya pamoja na timu yako na niwaombe Watanzania tukaielewe vizuri hii Miswada ili kwamba sisi ndio tuwe tunafaidika na hii Miswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, ahsante kwa nafasi hii. (*Makofii*)

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Miswada miwili iliyio mbele yetu. Kwanza, niseme naunga mkono hoja hizi mbili au Miswada hii na vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuileta japokuwa imechelewa, lakini nasema hatujachelewa sana. Imechelewa kwa sababu imeshazalisha matatizo mengi ya ardhi katika nchi yetu, lakini hii sheria ingekuja mapema labda yale matatizo yangekuwa siyo mengi kama hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nawapongeza wataalam wa Wizara, kwa kuweza kukaa, kutafakari na kuleta Miswada hii ili kuboresha maisha ya wananchi. Makazi kwa binadamu ni kitu muhimu; ni moja katika nafasi kubwa ya binadamu kuishi mahali pazuri ambapo afya yake itaendelea kuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, katika Muswada wa Mikopo ya Nyumba, wenzangu wameshazungumzia tatizo kubwa ni riba. Taasisi za fedha ambazo zitatoa pesa hizi, zisifanye kwamba hii *mortgage finance* iwe ni sehemu kubwa ya kujilimbikizia faida wakati kazi kubwa hapa ni kuona kwamba inatoa huduma zaidi kuliko faida kubwa

sana. La msingi, wao wanarudisha faida zao na iridhishe kwamba, faida wanazozipata zinalingana na kiwango cha Kimataifa, lakini tusimumize mwananchi kwa kutaka faida kubwa na hatimaye kumfanya mwananchi yule asiweze kufikia lile lengo la Muswada ambao uko mbele yetu.

Riba ni kitu muhimu, kutoza riba ya asilimia 10, 12 mpaka 16 kwa kweli ni benki chache Duniani na wengi wanatushangaa, labda kwa sababu ya hali ya uchumi wa nchi. Imekuwa *too much exaggerated*, unamkopesha mtu kujenga nyumba usitegemee kwamba anafanya biashara, ni mfanyakazi, mkulima mdogo mdogo au ni mchimba madini mdogo mdogo na yeze ana haki ya kuwa na nyumba nzuri katika nchi hii. Kwa hiyo, haya mabenki yaone yatoe huduma kwa kuwasaidia wananchi. La msingi, ile dhamana ya yeze kurudisha mkopo inakuwepo kwamba pesa zake hazitapotea na ile faida ambayo anatakiwa aikusanye iwe ni ya uhakika na ambayo haitamuumiza mwananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nisisitize kwamba, suala la riba lizingatiwe sana ili tuone kwamba kasi ya ujenzi wa majengo katika nchi yetu inaenda vizuri na hatimaye wananchi wanajenga nyumba nzuri. Ukimwekea riba kubwa hata ujenzi wake utakuwa ni dhaifu, nyumba itakuwa ni dhaifu kwa sababu atakopa kidogo kulingana na hali yake, lakini hatimaye ile nyumba mategemo yake ni kwamba, watoto nao warithi na hatimaye waweze kuishi kule baada ya yeze kuondoka Duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nisisitize kwamba, Serikali ione uwezekano wa kuanzisha mabenki maalum hapa nchini ya kuweza kukopesha badala ya kuachia Mabenki ya Kimataifa au Mabenki ya Nje kuja kufanya shughuli hii. Wao kwa hakika masharti yao kidogo ni magumu na riba yao itakuwa ni ngumu, vilevile pesa ambayo itakuwa inakusanywa na mabenki hayo asilimia kubwa itatoka nje, hatimaye hizi pesa zitabaki nchini na kuweza *ku-rotate* katika misingi ya ujenzi wa makazi kwa wananchi itakuwa ni jambo la busara. Hata hivyo, *justification* ya Wizara kuwaambia wananchi ambao sasa hivi wanamiliki maeneo ya kwenda kuishi ninyi mmewapa muda baada ya miaka mitatu hivi muwe mmeshajenga, msipojenga basi tutafuta hatimilihi hizo na tuwape wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwaambia vile na hatimaye hakuna utaratibu wa *mortgage financing* kama sheria hii inavyosema, tulikuwa tunawaonea wananchi. Sasa kwa kuleta Muswada huu na kuweka nafasi nzuri kwa wananchi kuweza kukopa na kujenga, nina hakika wale wote ambao wanamiliki viwanja na wale waliopewa muda wawe wameshajenga. Mimi naomba Serikali irudi nyuma, baada ya kupitishwa Muswada huu, agizo lile litolewe upya; kuanzia sasa tunatoa muda wa miaka mitatu uendeleze kiwanja chako kwa kukijenga. Kutakuwa hakuna sababu ya yule mtu kusema kwamba, ninakusanya nguvu kama utaratibu wa kukopa benki na kujenga nyumba utakuwa umerahisisha kwa mwananchi yule kuchukua mkopo na kujenga. Hapo tutakuwa tumempa nafasi nzuri ya yeze kujenga nyumba yake na ili aweze kuona matunda ya yeze kumiliki kile kiwanja. Kuna viwanja vimekaa miaka mingi sana havijengwi kwa sababu ya uwezo, wengi wao ni wafanyakazi na wengine wameshastaafu, lakini madhari ana kiwanja ambacho kina hatimilihi ni moja ya njia nzuri ya kuweza kukopa na hatimaye kuweza kujenga nyumba yake. Kwa hiyo, *justification* sasa ya kumpa muda mwananchi ajenge nyumba yake sasa hivi itakuwa ni sahihi kuliko hapo mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika suala zima la miliki za sehemu ya majengo, mimi niseme kwamba, kwanza, itasaidia wale wenye kipato cha chini kuweza kupata makazi mazuri ya kuishi. Kwa wale ambao hawana viwanja au wanaishi katika maeneo ya miji, wana nafasi nzuri sasa ya kuweza kupata nafasi. Kubwa hapa ninachotaka kusema ni kwamba, Jiji la Dar es Salaam eneo kubwa ni *squatter*, sheria hii sasa inaweza ikawa ni utatizo wa matatizo ya *squatter*. Yale maeneo ambayo hayajapimwa na watu wamejenga kiholela, leo ukitaka kuwaondoa inabidi uwalipe fidia na fidia ya hapa Jijini Dar es Salaam ni kubwa sana na Serikali haimudu. Tuone hizi *squatter* sasa tunazioanisha vizuri, nikichukua mfano wa Manzese hakuna *sewage system* nzuri, hakuna utaratibu mzuri wa barabara wala hakuna utaratibu mzuri wa kusambaza umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vyema Serikali ikapanga, ikatengeneza michoro na hatimaye katika zile *squatters* badala ya kumlipa fidia yule mwenye kiwanja ambaye hatimaye kisheria anatakiwa aondoke pale, lakini huwezi ukamwondoa kwa sababu yuko pale kwa zaidi ya miaka 10, 20; mnaoanisha mtaa ule na kwamba eneo hili limepimwa na barabara zake ziko hivi, ninyi badala ya kulipwa fidia ondokeni. Eneo lile sasa lipimwe zижengwe nyumba kama ni ghorofa moja au mawili hatimaye wale wananchi wanaoishi katika yale maeneo wapewe zile *flats*. Kwa hiyo, kama ni viwanja vya watu watatu, zikijengwa nyumba za *flats* wataishi labda kumi na mbili badala ya tatu. Sasa badala ya kumpa fidia mwambie gharama ya fidia tutakupa *flat* lile na kilichobaki utakuwa unalipa kodi au unalipa gharama ya lile *flat* kama unainunua na hatimaye aimiliki moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumepunguza matatizo ya kuwashamisha wananchi kuwapeleka sehemu ambayo hakuna utaratibu mzima wa barabara, maji, umeme, wala usafiri. Ukimwambia unabaki hapa hapa, tunabomoa sehemu ya eneo hili tunajenga *flats* hatimaye nyumba yako itakuwa hapa hapa na kiasi kilichobakia utalipa; sasa kazi hiyo itafanywa na nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa ikae itazame, tuna taasisi mbalimbali za Serikali ambazo zinafanya kazi hizo. Tuna *NSSF* wanafanya hizo kazi, pengine mzigo utakuwa mkubwa kwao lakini zipo nyingine watakuwa tayari. Zinaweza zikaundwa taasisi nyingine zikafanya kazi hiyo, lakini hizo taasisi zipata wapi pesa? Zitapata pesa kutoka benki ili tuweze sasa kuipanga miji yetu vizuri na hatimaye wananchi waishi maeneo yale yale kwa utaratibu mzuri na bila kulipa fidia kubwa Serikalini hatimaye abaki na aweze kupata nyumba nzuri. Hivyo ndivyo tutakavyoweza kuyatatua matatizo ya *squatter* katika Jiji la Dar es Salaam na ndio eneo kubwa la majengo yaliyokuwepo katika Jiji letu la Dar es Salaam. Vipi tunalitatu tatizo hili? Suala zima la hii *mortgage financing* litasaidia kuweza kutatua hayo matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaiomba Serikali ikae pamoja na wataalam, waone uwezekano wa kutumia sheria hizo kuboresha *squatter* zetu katika miji yote siyo tu Dar es Salaam lakini miji mikubwa. Tuwe sasa na utaratibu kwa miji mingine ambayo haina *squatter*, tuweze kupanga mipango mizuri. Hili ndio lilikuwa la msingi, yapo maeneo katika Jiji la Dar es Salaam sasa hivi yanatakiwa yaendelezwe na ni nyumba za

zamani nyingine zinamilikiwa na *National Housing* lakini kuna utaratibu sasa hivi nyumba nyingi za *National Housing* hawana kumbukumbu za hatimiliki ya majengo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Waziri afanye jitihada kubwa Wizara imalize tatizo la kupata kumbukumbu za hatimiliki za majengo ambazo hazijakamilika. Nyumba nyingi zinashindwa kuendelezwa kwa sababu kumbukumbu za hatimiliki hazipatikani. Labda kwa wakati ule, wale waliokuwa wanamiliki zile nyumba, kumbukumbu zilipotea na hivi sasa Serikali inaweza ikatoa hatimiliki mpya na hatimaye shughuli za maendeleo ya ujenzi katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine ziweze kuendelea kwa kasi. Shughuli nyingi ambazo wafanyabiashara wameingia ubia na *National Housing*, wanashindwa kuendeleza majengo yale kwa sababu ya kukosekana kumbukumbu za hatimiliki. Hili nimeliona na itasaidia vilevile kuharakisha maendeleo ya jumla, kwa sababu tunafahamu kwamba, Serikali siyo kazi yake kujenga majumba ni kuwapa watu binafsi wafanye hizi shughuli na Serikali ikusanye kodi yake ili kuweza kuendeleza maeneo mengine ya sekta ya ardhi na majumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tena ninaipongeza Miswada yote miwili na ninawataki kila la kheri Wizara ya Ardhi, kuweza kufanikisha na kuitumia vizuri Miswada hii. Baada ya kupitishwa na Mheshimiwa Rais, mwananchi aweze kunufaika moja kwa moja katika masuala ya makazi. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia ni dakika kumi, haziwezi kutosha kwa msemaji mwingine. Tutakaporudi mchana atakuwepo Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Raynald Mrope.

Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 06.47 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge nilikuwa nimewataja Wabunge watakaochangia mchana. Ninasikitika kusema kwamba, nitaishia wanne kwa sababu Muswada huu ni lazima uishe leo. Kwa hiyo, kuna wachache hapa ambao hawatafikiwa na kwa hiyo tutaanza na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu halafu Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi na Mheshimiwa Joseph Mungai.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Muswada huu muhimu wa *units*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali; huu hasa ndiyo muda na ndiyo hasa inavyotakiwa Serikali yetu iwajali wananchi wake kwa mtindo wa kuwahakikishia wanakaa katika makazi mazuri na bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu sisi Halmashauri ya Manispaa ya Ilala tuliuanza mwaka 2006, tulipopata mwekezaji kutoka Malaysia na alikuwa anakuja katika zile nyumba za kota pale Mchikichini. Mpango ambao tuliufanya na yule mwekezaji alikuwa anajenga nyumba za kukaa na kuwahamisha wakazi wa pale kuwaweka katika maeneo yale yale lakini kwa kupewa *low costing blocks* na baadaye kuwamilikisha ili waweze kutumia hati zile ziwaendeshee maisha yao. Upande mwingine ulikuwa sasa wa wale wenye uwezo wa kulipia gharama za juu na kuwafidia wale ambao uwezo wao ni mdogo, lakini ukakwama kutohuna na sababu ambazo hazikuwa za msingi sana lakini tutajitahidi kuurudisha tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha Watanzania sasa kimepata jibu, wanyonge wanaokaa katika nyumba hizi za mashirika; yaani nyumba hizi za *National Housing*, furaha yao ipo kwa Serikali yao ambayo leo inawakomboa na kuwatambua kwani na wao sasa wana haki ya kumiliki nyumba katika maeneo ambayo sasa hivi wanapanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema kwamba, mpango huu na Sheria hii ni nzuri lakini kunatokea matatizo mengine kwamba, Sheria zinapotungwa katika Kanuni kuna wajanja huanza kuingiza mambo yao na kufanya Bunge linapoamua kutunga Sheria kufuta maazimio mazuri ambayo Bunge linataka lakini na wao kujivekaa vipande vyao kwa kuona sasa imekuwa ni shughuli ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa wamekaa katika nyumba hizi zaidi ya miaka 40, wamelipa kodi zaidi ya miaka 40 na ukitazama hata nchi za Ulaya; *mortgage system* kuna kipindi unapolipa kodi unatakiwa nyumba zile upewe bure na uzimiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake, aelewé ya kuwa kwanza, gharama za kuwauzia nyumba watu hawa isiwe gharama ya kuwafanya wakimbie halafu wengine ambao wana uwezo mkubwa zaidi ya hawa waliokaa sasa hivi. Hilo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulipaji wa nyumba hizi usiwe wa kushtukiza kwamba, kwa sasa tunakupa hati utakuwa unakaa hapa, umeshakaa miaka 40 lakini tunakupa miezi mitatu umalize kulilipia jengo hili ili sasa umilikishwe kwa kiwango kikubwa cha kumfanya huyu ahame na kuweka tabaka la kubadilisha watu wengine kuingia katika maeneo mengine ambayo hawa watu tayari ni makazi yao na wameyazoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitamwomba Mheshimiwa Waziri alizingatie sana hili; wastaafu wengi wanakaa kwenye nyumba hizi, wamelitumikia taifa hili kwa muda mrefu sana, hebu sasa na wao tuwatazame kwa maana sasa tuwape nyumba hizi kwa gharama ndogo na kwa muda wa kutosha ili waweze kulipia na waweze kuzimiliki ziwe mali yao na vizazi vyao na shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nyumba za mashirika na tunaziona sasa hivi zinauzwa kiholela tu. Hakuna utaratibu unaofuatwa, kwani anaingia mwenye uwezo anachukua nyumba hizi na wale wasiokuwa na uwezo ndiyo wanaowekwa pembedi, tunawa-*displace* wananchi na kuwapeleka katika maeneo ambayo hawajayazoea na huko tunakowapeleka wanapata tabu kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano tunauona sasa hivi Dar es Salaam, watu wengi wamekuwa *displaced* kwa sababu wanashindwa kuendana nayo. Hili suala la kusema asiyekuwa na uwezo aondoke siyo sahihi. Malaysia wana mpango kama huu na siyo tu kwenye *units* hizi, mpaka kwenye viwanja kuna maeneo yanatengwa mahususi kwa watu wenyе uwezo wa chini na yule mwenye uwezo wake mkubwa haruhusiwi kuingia hapo wala haruhusiwi kununua eneo hilo na akigundulika ananyang'anywa. Yote hii ni kuwafanya watu kuishi kwa amani na wale wenyе uwezo mdogo kutambulika na Serikali yao kusaidiwa na wao waishi katika mazingira yale yanayozunguka wenzi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uliona juzi mpirani kwenye mechii ya Simba na Yanga, wote tuliutazama mpira; mpira ule ule tumeutazama katika viti tofauti. Kwa hiyo, naiomba Serikali nayo ilione hili. Hawa wakazi wa Dar es Salaam na wao wanataka kukaa katika nyumba bora, lakini nyumba hizi bora wanazokaa wao zisije zikawa zinachukuliwa na watu wenyе uwezo ili wao wazidi kusukumwa, ule mpira wakawa wanautazama sasa kwenye runinga wakashindwa kuja uwanjani kuutazama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri hili alone.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutakuwa na tatizo watakapoanza kuamua kutangaza tenda za nyumba hizi, nyumba za Serikali zinauzwa bila tenda, wewe mtumishi wa Serikali unaambiwa lipa hiki. Wakazi wa sasa wapewe *privilege* hiyo ili na wao watambue kuwa taifa lao na Serikali yao sasa inaona umuhimu wa wao kubaki pale na kumiliki nyumba zile kwa gharama ambazo tutaziona zina unafuu za kumsaidia hata yule aliystaaufu akimpiga mzinga mwanaye analipa gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi sana wanafikiri tunavyoona taratibu za kidunia zinavyokwenda, suala la ujamaa sasa hivi halipo si kweli. Marekani kuna matatizo makubwa sana kiuchumi; imetaifisha mabenki, Uingereza imetaifisha mabenki, hii yote ni kulinda maslahi ya watu wake. Kwa hiyo na sisi Tanzania vilevile, Serikali ina nafasi kubwa sana ya *ku-chip in* kusaidia watu kuwa katika makazi mazuri na ndiyo hiki Serikali inachokifanya na wananchi sasa hivi wameshatambua kwamba hii ndiyo Serikali inayotujali. Kwa mpango huu, amani na maendeleo yatapatikana kwa watu wengi, kwa wao kutambua namna Serikali yao inavyowajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango mkubwa sana wa Serikali kupima viwanja vingi sana nje ya miji. Huu siyo utaratibu wa kujenga miji, Dar es Salaam bado siyo kubwa. Kuna maeneo ya Magomeni na Ilala, wananchi waelimishwe kubadilisha mfumo wa miji baadaye wauze nyumba zao kwa watu na wao waondoke wapelekwe

maeneo ya mbali. Kuwe na elimu kwa wananchi waingie ubia na watu wenye uwezo wajenge maghorofa makubwa ya *flats* 20 na huyu mwenye nyumba ambaye siku zote anakaa kwenye nyumba yake ya kiswahili pale Magomeni, badala ya kukaa chumba kimoja au viwili na familia yake, apewe *flats* 6 mpaka 7 katika eneo lilelile.

Mheshimiwa Naibu Spika, miji haijengwi kwa kupanua maeneo; miji inapanuliwa kwenda juu. Wananchi wetu wanayo nafasi ya kuelimishwa manufaa na faida ya kubaki katika eneo lake, badala ya kuwa na nyumba moja anakuwa na nyumba saba na maduka 20. Yakijengwa chini na yeze anapewa maduka saba ili aendeshe maisha yake. Hili linahitaji elimu tu, wananchi wetu wakielimishwa wataelewa na utauona mji wetu unakua kwa kipindi kifupi.

Sasa hivi Kariakoo nyumba zinauzwa. Nyumba hizi ni za wazazi wetu na wazazi wetu kwa mtindo wa zamani walioa wanawake watatu, watoto 12, nyumba inauzwa shilingi milioni 600; mnagawana vipi watoto 12? Matokeo yake kila mtu anapata shilingi milioni 40 anazipokea anaona raha, anajimwaga mitaani, lakini baada ya miezi sita watu wanarudi katika mchacho wanaanza kuichukia nchi Vilevile wanachukia mpaka mambo ambayo wamejingiza wenyewe katika matatizo kama hayo. Tuwaelimishe hawa watu waingie ubia na watu wenye uwezo, majina yao ya asili yatabaki katika maeneo yale, haki zao zitabaki pale, uwezo wao utazidi kuongezeka na mapenzi yao na nchi yatazidi kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kengele ya kwanza imelia na muda uliobakia ni mchache, niwaache na wengine nao wachangaie.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia zote. Hiki ndiyo kitu tunachokitaka sasa kiwafikie wanyonge na wao waone kuwa sasa nao wanatambulika na meseji hii iende kwa Mzee Bwao na asikie kuwa Serikali yao sasa inamjali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, lakini kwa nini Mzee Bwao?

Sasa namwita Mheshimiwa Suleiman Kumchaya na Mheshimiwa Manyinyi ajiandae.

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo katika Miswada hii miwili. Mimi nitajikita zaidi katika *mortgage finance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa na mimi ninapenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii ya Ardhi, kwa kuleta Muswada huu ambao tumeupigia kelele kwa muda mrefu, kwa nia na dhamira ya kutaka kuboresha maisha ya

Watanzania. Nasema ahsante sana na moja kwa moja ningependa kuunga mkono Miswada yote miwili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeanza kwa kuchangia katika eneo hili la wakopaji na benki. Bado mabenki yetu haya hayana mwelekeo sahihi ama unaoeleweka kwa wananchi wa kuchangia katika maisha bora ya Watanzania. Nasema hivyo kwa sababu suala la *high risks* katika mabenki ya Tanzania bado wanalo kwamba, unapotoa mikopo kwa Watanzania, uwezekano wa kurudisha mikopo hiyo ni mdogo sana. Matokeo yake, Sheria hii ya *mortgage finance* itashindwa kufanya kazi, hata wale ambao watapata nafasi ya kukopa huenda pengine wakashindwa njiani kwa sababu ya riba kubwa. Sasa hili ni tatizo katika Sheria kama hizi. Tunayaomba mabenki yetu haya, pamoja na ukweli kwamba, yanafanya biashara lakini yajenge mazingira mazuri ya kuwafanya Watanzania waweze kufaidika na Sheria hii na wao benki pia waweze kufaidika.

Sasa hivi hali ya uchumi wetu siyo mbaya kiasi hicho na mimi ningependa kusema hata Watanzania wenyewe sasa hivi wameanza kuwa na mwamko mkubwa wa kujua kwamba, unapokopa lazima ulipe. Kwa hiyo, tungependa kuwaambia hawa wenzetu, yaani mabenki haya waanze kubadilisha fikra zao, waanze kubadilisha mfumo wao. Bila kusahau kazi yao ya kufanya biashara, washiriki katika kuleta maendeleo katika nchi yetu, hasa kwa upande huu wa nyumba bora kwa Watanzania. Hilo lilikuwa la kwanza kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wengi tunafahamu kitu kinachoitwa *money laundering*; tatizo hili ni kubwa katika dunia hii na wanaofanya kazi hii wanasubiri vitu kama hivi; *mortgage finance* na mambo mengine mengine zaidi ili waweze kuhalalisha pesa zao zitumike rasmi. Kwa kufanya hivyo; ni hatari kwa taifa lolote likiwemo Taifa letu la Tanzania. Tunaiomba Serikali na vyombo vyote vinavyohusika katika kutengeneza kanuni na taratibu za kutumika Sheria hii, basi wawe macho sana katika kuziba mianya ya wenzetu hawa kuja kutumia Sheria hii ili kuhalalisha pesa chafu zikaleta athari katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nilipo nina nyaraka nyingi tu ambazo zinalezea hawa wajanja wa *money laundering*, walivyotumia nafasi hii kuhalalisha pamoja na nchi zilizoendelea maana huko ndiko wanakoanzia. Huku kwetu kama ikija itakuwa ni rahisi tu. Kwa hiyo, ni vyema na Serikali yetu ikawa na uhakika; huyu Suleiman Kumchaya anayekwenda kukopa kweli ni huyu? Pesa alizokubaliwa na benki ni hizi? Eneo hili analokwenda kujenga kweli ni lake?

Kwa kufanya hivyo, Sheria hii itawasaidia sana Watanzania ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakisubiri kwa hamu kubwa, maana tumechoka kukaa katika nyumba ambazo hazifanani na nchi huru, hazifanani na ustaarabu wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi Sheria hizi tunapozitunga zinafaa mijini ama katika miji mikubwa, maeneo mengine ya nchi yetu wanasilka katika redio na kusoma katika magazeti au mtu akizungumza pengine kutoka Dar es Salaam, Mwanza au Arusha, lakini wao kuona kwa vitendo kwamba Sheria hii inatumika hawaoni. Kwa hiyo,

ninaiomba Serikali yetu, mabenki yetu na wadau wote, ambao kwa njia moja ama nyingine watashiriki katika kuitekeleza Sheria hii; hii Sheria isambazwe nchi nzima, ifahamike kwa wananchi na ikubalike nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mfano; Mkoa wa Mtwara sasa hivi una bandari nzuri na mimi ningependa kusema kwamba ni moja kati ya bandari nzuri katika Bara la Afrika; imekaa mahali pazuri, ina kina kirefu zaidi kuliko Mombasa, Dar es Salaam, Cape Town na bandari nyingine zote tunazozifahamu. Mkoa wa Mtwara sasa hivi kuna umeme wa uhakika wa Mnazi Bay na tunaambiwa kwamba, uhakika wa umeme huu sisi tutaondoka, vizazi vyetu vitakuja vitaondoka na hivyo vingine vitakuja vitaondoka na kadhalika, bado umeme huu utakuwepo. Si hivyo tu, kwa sababu ya umeme huu na miundombinu hii, watu wameshaanza kutaka kuitumia Bandari ya Mtwara na kuwekeza viwanda mbalimbali katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba, kusiwe na mambo mengine tena ambayo yanaweza yakazuia kutumika kwa Sheria hii eti kwa kusema huko Mtwara kuna hili na lile ama Mikoa ya Kusini kuna hili na lile. Tunaomba Sheria hii kama nilivyosema, basi na kule kwetu tuione, maana kuna wenzetu wengine wanafikiria kwamba, Bandari ni Dar es Salaam tu, wanasahau kama kuna Mtwara na Tanga. Huko pia kuna watu wanataka kubadilisha maisha yao wafaidike na Sheria hii. Mazingira yanaruhusu na mimi ningependa kuungana na wenzangu wote ambao wameipongeza Serikali yetu kwa kuleta Muswada huu, kupitia Wizara yetu ya Ardhi.

Haya ndiyo mambo ambayo tumekuwa tukiyasubiri, tunatakiwa tufanye maamuzi ya makusudi kabisa ya Watanzania kufaidika na uhuru wao na uchumi wao. Tusifikiri kwamba, kuna mtu atakuja kutoka juu ama sehemu nyingine kuja kutuendeleza, hata kidogo! Ni sisi wenyewe Watanzania, kwa kutumia vitu kama hivi na mimi ninaamini yapo mengine yanakuja mazuri zaidi ili kuwafanya Watanzania watulie na wakitulia nchi hii itakuwa na amani, umoja na udugu hautakuwisha, pia tutakuwa na jina kubwa katika dunia hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika nimezungumza na nimeeleweka; ni matarajio yangu kwamba, wenzetu hawa watakapokuwa wanamalizia, watayazingatia haya ambayo leo hii tunawaambia kwa faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja kwa Miswada yote miwili. (*Makofi*)

MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Miswada yote miwili, inayohusu utoaji wa hati miliki katika sehemu ya nyumba lakini vilevile na Muswada unaohusu mikopo kwa ajili ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba kuungana na wenzangu kwamba mpango huu mzuri na ni mpango ambao unaweza kuwasaidia wananchi wetu katika

kujikwamua kimaisha kuliko maisha wanayoishi hivi sasa, ambapo wananchi hawana uhakika sana wa kuishi kwa sababu hawana makazi mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu naomba tu nichangie kidogo kuhusiana na huu umilikishwaji wa sehemu ya nyumba. Pamoja na kwamba, mpango huu ni mzuri, lakini naomba nitoe tahadhari kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, hivi sasa inaonekana tayari kuna waliokwishapata taarifa kwamba, mpango huu unakuja na hata mimi juzi niliona kwangu pale Musoma kabla sijaondoka, yaani siku moja kabla watu walianza kupewa *notice* ya kuhama katika hizi nyumba za Serikali na hawa Wakala wa Majengo. Kwa hiyo, isije ikawa ndiyo huu mpango kwamba ili hawa watoke na wale wanaohitaji waingie humo ili muda utakapofika, basi hawa wa sasa ndiyo wamilikishwe wakati kuna watu wamekaa pale kwa muda mrefu. Kwa hiyo, hilo nilipenda tu kutoa tahadhari ili Serikali iweze kuliangalia, watu wasije wakaondoshwa ndani ya hizo nyumba ambazo wanaishi halafu kesho watu wengine waingie na kuuziwa hapo hapo. Kwa hiyo, nilipenda tu niitoe kama tahadhari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Muswada wa pili ni huu unaohusu *mortgage finance*; mimi nimeona mara nyingi Miswada kama hii ya utungaji wa Sheria imekuja Bungeni, lakini vilevile tumefanya mipango mingi Bungeni hapa kwa ajili ya manufaa ya watu wetu. Kitu ambacho kinanipa tabu sana ni kwamba, kile ambacho tunakubaliana hapa kila mmoja unakuta amekifurahia sana, lakini kinapokwenda kwenye utekelezaji kule mambo yake hayaendi vizuri kama ambavyo tulitegemea. Kwa hiyo, nadhani hii mipango pamoja na kwamba sisi tuna-*copy* kutoka katika nchi nyingine, yaani nchi zilizoendelea ni vizuri inapofika kabla hatujaanza utekelezaji wake, tukae na kuileta katika hali halisi ya hapa kwetu tuone matatizo yaliko.

Labda mimi nitoe mfano mmoja ambao ulikuja kwetu na sisi tukaufurahia, tukaona kama wananchi wetu wanaweza kufaidika sana. Nakumbuka ulikuja mpango huu wa fedha za JK, watu wetu wengi walifurahi na sisi tulifurahi na ikaonekana kwamba watu wetu wataweza kukopa fedha hizo kwa riba nafuu na kweli ndivyo namna ilivyokwenda. Cha kusikitisha sasa mpango huo huo kusema kweli hauna mafanikio mazuri, kwa sababu mojawapo ya sababu ni watu wetu kutokuwa na yale mazoea ya kukopa. Kwa hiyo, watu wengine kama sisi wa Mara wakati mwengine unakopa unakwenda kuo mke wa pili na wa tatu, kwa hiyo, matokeo yake siku ya siku unakuja kudaiwa fedha; fedha hazipo namna ya kuzirudisha huwezi sasa matokeo yake unabaki kuilamu Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini mimi niseme hivyo? Huu mpango wa *mortgage finance* ni mpango ambao utatuwezesha sisi wananchi au wananchi wa kawaida kuweza kukopa fedha ili tuweze kujenga nyumba. Kwa hiyo, kama hatukuweka utaratibu mzuri, matokeo yake baadhi yetu tutakopa fedha hizi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, lakini tutakwenda kufanya mambo mengine. Matokeo yake, zile dhamana tutakazokuwa tumeziweka zitakuja kuchukuliwa halafu kesho tena sisi hao hao tutaanza kulia na kuanza kuilaumu Serikali.

Kwa hiyo, mimi nadhani ni vizuri Waziri akaendelea kulifanya kazi ili tuweze kuona ni kiasi gani zoezi hili ambalo tunategemea kwamba litamkomboa mwananchi hasa watumishi wetu na wale watu wenye uwezo wa chini, hebu tuendelee kuwa makini ili kesho lisije likarudi kuwa kero. Sasa katika ufanikishaji wa hii *mortgage finance*, mimi nashauri mambo yafuatayo:-

Kwanza ni vizuri Serikali au Wizara ya Ardhi ikaendelea kutenga fedha zaidi kwa ajili ya upimaji wa viwanja ili viwanja vingi zaidi viweze kupatikana hasa katika maeneo ya mikoani na kule vijijini. Haya maeneo yatakapokuwa yamepatikana sasa, kwa mfano na viwanja vikishapimwa; ni rahisi zaidi watu kama wa *TANESCO* kukahakikisha wanapeleka pale miundombinu ya umeme, watu wa Idara ya Maji wapeleke pale maji, ndipo sasa zile nyumba ziweze kujengwa katika maeneo hayo.

Kwa mfano, upande wa watumishi; kwa kweli tuna tatizo kubwa la watumishi wetu wengi kutokuwa na nyumba za kuishi. Wengine wangependa wanunue nyumba zao wenyewe na uwezo wa mtu mtumishi kujenga nyumba ya shilingi milioni 50 wakati mwengine ni mdogo. Ikijengwa *flat* moja ambayo inachukua karibu watu 50 mpaka watu 100 ni rahisi mtumishi kuweza kupata nafasi hapo nyumba itakapojengwa. Atapata *apartment* ambayo atailipia kwa muda wa miaka 10 au 15 katika kipindi alichoko katika ajira yake ya utumishi. Kwa kufanya hivyo, watumishi wengi zaidi watakuwa wamepata nyumba na wataishi maisha mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata kwa wale ambaeo ni watumishi wanaotaka kwa mfano katika Taasisi kama Wizara zetu hizi; ukiangalia walimu wetu wengi hawana nyumba za kuishi; waganga na madaktari hawana nyumba za kuishi. Hivi viwanja kama tayari vimeshapimwa ni rahisi sana hizo nyumba zikajengwa na ikiwezekana basi hizi Wizara zitenge fedha katika bajeti zao kila mwaka kwa ajili ya kulipia lile deni. Tunadhani kwamba, kwa kufanya hivyo, watumishi wengi katika Wizara zetu basi watakuwa wamepata mahali pa kuishi na wakati mwengine namna ya kuwapata itakuwa ni rahisi, kwa maana ya kutumia usafiri wa aina moja kwenda makazini. Kwa hiyo, tunadhani kwamba, kama hii mipango itatekelezwa vizuri, basi itakuwa imewasaidia watu wetu zaidi hasa wale wanaoishi katika mazingira ambayo si ya kawaida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwa wale watu binafsi wako watu wetu, *especially* wale wanaoishi mjini lakini wanavyo viwanja na wanazo nyumba ambazo zimechoka zilipaswa ziondolewe na baada ya kuondolewa zijengwe nyumba nzuri. Sasa unakuta kwa kuwa wengine hawana uwezo, matokeo yake ni yule mwenye fedha ndiyo anakwenda pale ananunua kiwanja chake kwa bei ya chini, halafu yeye anahamia maeneo ya mbali kabisa na baada ya hapo sasa huyu ndipo anaweza kukiendeleza kiwanja hiki. Tunadhani kwamba, kuitia utaratibu huo wa *mortgage finance* kama utakuwa umeandaliwa vizuri hata kwa wale ambaeo hawana *security* ya kuweka pale kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo basi ni vizuri hata ile ardhi yenyewe ikawa dhamana ya ujenzi wa nyumba anayohitaji kuijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linawezekana kwa utaratibu ufuatao; kama tayari ramani itakuwa imeshaonekana kwamba hapa anataka kujenga aina fulani ambayo labda

kiasi cha nyumba kitatumika kama nyumba za watu kupanga au nyumba ya biashara ni rahisi akaonyesha mchanganuo wa hatua anazotegemea kujenga. Kwa hiyo, kama mkopo wake ule labda utagharimu shilingi milioni 200, lakini msingi unaonyesha kwamba msingi ni shilingi milioni 30 basi kwa kutumia ile *engineers estimate* inakuwa ni rahisi sana ataomba ile milioni 30 akajengea msingi akaomba shilingi milioni 20 akajenga ukuta, akaomba fedha nyingine akaenda hatua kwa hatua na hatimaye ile nyumba ikafika mahali ikaisha. Nyumba ile itakuwa imebaki ya kwake na ataendelea kuitumia, kiasi cha fedha anachokipata kutokana na mapato hayo atatumia kwa ajili ya kulipia deni hilo.

Kwa hiyo, tunadhani kwa kutumia utaratibu kama huo na wa aina nyingine kwa kadiri utakavyoboreshwa kumbe basi itatuwezesha au utawawezesha watu wetu wengi hata wale ambao uwezo wao kifedha ni mdogo nao waweze kufaidika na mpango huu. Kama tutaangalia tu kwamba ilimradi una dhamana mahali fulani upewe shilingi milioni 100 au milioni 200, kuna watu wengine maisha yetu tumekua lakini hatujawahi kushika kwa mkupuo moja shilingi milioni 50. Sasa nikija kupokea shilingi milioni 200, matokeo yake nitaanza kufanya mambo mengine hiyo nyumba itaishia kwenye msingi na shilingi milioni 200 zimekwisha halafu kesho ninaanza kuona kwamba Serikali imeleta kero badala ya sisi kuufurahia mpango huu ambao ni mpango mzuri ambao umeletwa na Serikali kwa manufaa ya wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo basi na mimi naungana na wenzangu kuunga mkono Miswada yote miwili ili iweze kupitishwa kama sheria na hatimaye utekelezaji wake uweze kwenda haraka. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH J. MUNGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri. Tangu mwanzo napenda niseme wazi kabisa kwamba, naziona hoja hizi mbili ama sheria hizi mbili na hoja inayozileta ni nzuri na naunga mkono kwa moyo mkunjufu. Hoja hizi zinahusu umiliki wa sehemu ya jengo au sehemu ya eneo, yaani kutoa *unit title* katika vijisehemu na pia kutumia ardhi au jengo kukopea au kwa lugha ya wenzetu, zinahusu *mortgage finance*. Mambo yote mawili katika hali yetu ya uchumi unaosonga mbele, yanahitaji hatua za aina hii.

Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa kuyaona matatizo yaliyopo katika uchumi na kuyachukulia hatua haraka na hata kwa kutumia Hati ya Dharura ya Mheshimiwa Rais. Ningependa kunukuu kama ifuatavyo kwa Lugha ya Kiingereza: “*Time is always right to do what is right*” hayo yalisemwa na Dr. Martin Luther King. Kwa hiyo, wanachosema wenzetu kwamba tunakwenda kwa *speed* kubwa mno, mimi nadhani sio sahihi Mawaziri wawe tayari kuchukua hatua za aina hii kila wakati inapobidi na sisi Wabunge tutawaunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kupitisha hati ya dharura na pia nawapongeza sana wenzetu mlion wajumbe katika Kamati ya Uongozi, kwa kuungana mkono na Mheshimiwa Rais na kutuletea sheria hizi mbili kwa

Hati ya Dharura. Kipengele hiki kiliwekwa katika taratibu zetu ili kiweze kutumika katika maeneo kama haya, lililochelewa lisingojee kesho. Baba wa Taifa aliwahi kutuambia inapobidi *we must run while we walk*, wakati wengine wanatembea sisi lazima tukimbie. Kwa hiyo, hatua kama hizi ni za kutekeleza pia maelekezo hayo ya Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Waziri aendelee kwa kasi kuikarabati Sheria ya Ardhi ili kila kipengele ambacho kinaonekana ni kikwazo kwa maendeleo, kifanyiwe marekebisho upesi. Nimeyasikiliza maneno waliyoyasema wenzetu wa Kambi ya Upinzani waliochangia asubuhi, Mheshimiwa Ndesamburo, ningemshauri aisome vizuri ibara ya 8(b), kwa sababu pale inazungumziwa *Certificate of Title* kwa wenye sehemu ya jengo au kiwanja. Kwa hiyo, alichokuwa anashauri kifanyike kwamba wale wapewe hati ya kumiliki tofauti na ile *title deed* ya lile eneo kubwa kwa kweli ndivyo ilivyo katika sheria.

Mheshimiwa Kabwe Zitto, alionyesha mashaka ya kutokuwa na *regulatory authority* katika maeneo ya *mortgage*. Napenda niitumie nafasi hii kukumbusha kwamba, sheria hii ukiisoma vizuri sio ya *mortgage* tu bali ni ya *mortgage finance*. Ukishaweka *mortgage finance*, basi moja kwa moja sheria inasimamiwa pia chini ya Sheria ya Mabenki na asasi za fedha. Kwa hiyo, katika sheria ile *regulatory authority* ipo na ni Benki Kuu. Kwa hiyo, *gap* waliyokuwa wanasesma ipo mimi naona kabisa haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali muhimu sana katika nchi na hili limetamkwa wazi katika Azimio la Arusha kwamba, ili tuendelee tunahitaji vitu vinne; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Mimi naona tamko hilo katika Azimio la Arusha lilikuwa sahihi wakati ule na ni sahihi mpaka leo kwamba, hizi ni rasilimali muhimu kabisa kwa maendeleo. Takwimu za Kitaifa tumesomewa mara nyingi na tumetaarifiwa mara nyingi na tumekumbushana mara nyingi hapa Bungeni kwamba, tuna ardhi kubwa sana hapa Tanzania. Inaonyesha kwamba, tuna hekta milioni 40 zinazowezwa kulimwa kwa jembe la mkono, tunalima hekta milioni 6 au 7. Kwa hiyo, tuna hekta zaidi ya milioni 30 ambazo zinahitaji kuendelezwa; kwa jembe la mkono, hatuwezi kutegemea kuzifikia kwa upesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukitazama takwimu hizo hatuna uhaba wa ardhi. Ukweli ni kwamba, ardhi unayoiona isiyo na mimea wala isiyovunwa zao lolote lenye faida, kweli ardhi ya namna hiyo haina faida. Kwa hiyo, ningependa sana kumshauri Waziri kwamba, hatua kama hizi alizoanza kuchukua aendelee kuzichukua mpaka aifikishe sheria yetu ya ardhi iwe ni sheria inayokuza utumiaji wa ardhi kwa maana ya kuongeza kasi ya kujenga na kasi ya kuanzisha mashamba. Sheria ifike mahali iwe *ina-promote land use*, isiwe na vipengele vinavyokwaza matumizi ya ardhi au maendeleo ya ardhi kwa kasi. Kwa hiyo, nashauri kwamba, Waziri aendelee na hatua hiyo ya ukarabati wa sheria hii, akiyaona maeneo mengine ambayo yanakwamisha asisite kuyaleta hapa Bungeni kwa Hati ya Dharura, kwa sababu hiyo ndiyo ari mpya na kasi mpya tunayoithaji katika kufanya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hizi tusizione kwa ufinyu tu kwamba, zinaruhusu *mortgage finance* na zinaruhusu ardhi iweze kutumika katika mikopo. Mabadiliko haya yaliyoletwa katika sheria hizi, yatasaidia sana kukuza ajira hapa nchini. Unapohamasisha kujenga majengo mapya, unapoiweka sheria iruhusu *mortgage finance* ni kujenga majengo mapya na utakapojenga majengo mapya ni ajira mpya. Kwa hiyo, ile ahadi ambayo ipo katika Ilani ya CCM inatekelezwa kwa kuitisha sheria hii tunatekeleza ahadi tuliyoitao katika Ilani ya Uchaguzi kwa vitendo kabisa, kwa sababu yanapojengwa majengo mapya zinakuwepo ajira mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi nilimsikiliza kwa makini Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na nina hakika Wabunge wenzangu walimsikiliza alipojibu maswali namba 33 na 35 Swali namba 34 liliulizwa na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya na namba 35 liliulizwa na Mheshimiwa Gosbert Blandes. Katika maelezo aliyyoatao Mheshimiwa Waziri hapa, ilionesa wazi kwamba, kuna mlolongo mkubwa sana; mwekezaji anapotaka kuwekeza katika ardhi anafanya maombi. Ardhi yetu inamiliikiwa na Serikali za Vijiji, kwa hiyo, anafanya maombi kwanza pale vijijini, maombi yale inabidi yapitishwe ngazi ya Wilaya, Mkoa yaende ngazi ya Taifa, yaende kwa Waziri lakini ili uwe mwekezaji ambaye sheria sasa hivi inamruhusu kuweza kupewa hati ya miaka 99, kufika kwa Waziri bado haijatosha kwa mlolongo uliopo sasa katika sheria inabidi pia ipelekwe kwa Mheshimiwa Rais aweze kutoa kibali.

Ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri alitazame eneo hili. Nimesema katika zile takwimu tuna hekta zaidi ya milioni 30 tunazohitaji kuziendeleza. Wanapojitokeza wawekezaji wa kutoka nje wanahitaji maeneo ya kuyaendeleza, ningeshauri speed yetu ya kuwapatia hayo maeneo wawe na hatimiliki katika maeneo hayo tungeiongeza. Kupeleka kila ombi kwa Mheshimiwa Rais, naona inachukua muda mrefu na kwa taarifa nilizonazo, utoaji wa hati ulikwama kwa muda mrefu. Wengine wanasema tangu Serikali ya Awamu ya Nne imeingia madarakani, wengine wanasema Mheshimiwa Rais ameshatoa kibali katika maombi manne tu na tupo zaidi ya nusu ya muda wa maisha ya Bunge hili. Mimi naona speed hiyo ni ndogo, kama hizi takwimu zinazosema sio sahihi ningependa Mheshimiwa Waziri atuambie kwamba, je, katika kipindi hiki cha miaka mitano cha maisha ya Bunge hili ni wawekezaji wangapi ambao tayari wamekwishapata vibali ambavyo Rais amekwishatoa idhini?

Mimi ningeshauri kwamba, utoaji wa idhini ya mwisho ungefanywa kwenye sheria uwe unaishia kwa Waziri. Kwa sababu Wabunge tunaweza kumhoji Mheshimiwa Waziri hapa kama kuna kuchelewa, lakini si rahisi katika Bunge hili kuanza kumhoji Mheshimiwa Rais kama mambo yamekwama. Wakati mwingine yanakwama kwa Rais kwa sababu hayakupelekwa upesi kwake na Rais ana ratiba ndefu na mambo mengi ya kufanya. Kwa hiyo, nashauri kwamba, eneo hili Mheshimiwa Waziri nalo aliangalie alete marekebisho.

Pamoja na kurekebisha hilo, ningependa pia ndani ya sheria yawepo masharti kwa hao wanaopewa ardhi kwamba, ardhi hii wanayopewa wataitumia sio tu kwa yale wanayolenga wao, lakini uwekezaji wao pia uwe una manufaa kwa wananchi ambao

wametoa ile ardhi. Kwa mfano, kama tunavyofanya sisi kule Mufindi yale Makampuni ya Chai yanamiliki maeneo makubwa, lakini pale pale tumesema wakulima wa nje wanawenza wakauza chai katika viwanda vyao au Makampuni ambayo tumeyapa eneo kubwa kama ile Kampuni ya Kiwanda cha Karatasi kule Mgololo tumewapa hekta 28,000, tumekubaliana nao kwamba, wanapotengeneza miche na wao wanatumia teknolojia ya *tissue culture* miche ile wawape pia wananchi nao wapande miche iliyokuzwa kwa teknolojia ya *tissue culture* kwa maelewano kwamba nao watauza miti yao kule kiwandani.

Kwa hiyo, mimi ningeshauri Mheshimiwa Waziri alitazame hili jambo yawekwe masharti na Waziri pia apewe uwezo wa kukasimu madaraka kwa Wakuu wa Mikoa ili *speed* ya kutoa hatimiliki kwa maeneo ya zile hekta milioni 30 ambazo hatuwezi kuziendeleza kwa jembe la mkono, liweze kuwa kubwa zaidi kwa wawekezaji wanaotoka nje ambao wala hawaombi ruzuku ya mbolea na hawatumii jembe la mkono wanakuja na dhana kamilifu. Tukifanya hivyo, naamini *speed* yetu ya kuendeleza ardhi ambayo ndiyo rasilimali yetu kubwa inaweza ikaendelea kwa kasi kubwa. Nilipenda nichukue nafasi hii kutoa hilo wazo Mheshimiwa Waziri aliangalie kama ni eneo la kuendeleza ukarabati mzuri anaoufanya kwa Sheria ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda nimalizie tena kwa kusema nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu yake na naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, wale niliowataja asubuhi kwamba watazungumza watanisamahe kwa sababu nilipitiwa, tuna Miswada miwili ambayo inapaswa kupitishwa mmoja baada ya mwagine. Kwa hiyo, itachukua muda mrefu, wasemaji watatu itabidi wasiitwe.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, natoa pongezi zangu za dhati kwa Wizara ya Ardhi na Katibu Mkuu, kwa kutuletea sheria hii, ingawa kwa mawazo yangu imechelewa lakini hata hivyo si haba kuwa imeletwa.

Naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja, kwani ndio ukombozi wa Watanzania wa rika zote; wafanyakazi wanyonge na hata wenye nacho au wanaojiweza. Bali si hilo tu, ni Muswada utakaota faraja na hasa kwa wafanyakazi na kuzuia angalau kwa kiasi fulani, wimbi kubwa la rushwa na wizi usio na mipaka serikalini na mashirika ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu lipitishe Muswada huu na *Inshallah* utapita na ukipita, nina hakika utaondoa mfumo mbaya wa fedha na mikopo uliopo sasa, ambao ni kikwazo kikubwa kwa Watanzania wanaotaka kukopa kwa ajili ya kujiendeleza kimakazi, kwani sheria iliyopo sasa hutoa muda mfupi wa kuirejesha na riba

kubwa kwa wananchi. Mfumo wa sasa wa mabenki na taratibu zao za mikopo haupo tena duniani na umepitwa na wakati.

Ni mfumo dume na wala hautoi manufaa tuyatakayo kwa maendeleo ya nchi na wananchi wenye. Naipongeza tena Wizara, hata hivyo, wakati tunaikubali sheria hii tuna mambo mengi ambayo yanahitaji nayo yatakekelezwe:-

1. Elimu kwa wananchi ya namna sheria hii itakavyofanya kazi kwani bila ya kuelimishwa wahusika wajanja wataikwaza/na itawanufaisha wao zaidi.
2. Serikali kwa makusudi wapunguze urasimu wa ujazaji wa makaratasi.
3. Benki Kuu ihusishwe na utaratibu mzima wa ukopaji huo.
4. Riba iwe ndogo itakayowawezesha wakopaji kulipa.
5. Ikiwezekana taasisi na mashirika kama *NHC* yahusishwe hasa mkopaji atakapofikia hatua za ujenzi ili kuzuia wakopaji wasizitumie pesa hizo kwa shughuli nytingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Wizara na mabenki hasa pale itakapofika hatua za mwisho za mkopaji kupata fedha na mkopeshaji kutoa hela, ziwepo taasisi ambazo zitakabidhiwa *contract* ya ujenzi ule baada ya mkopaji kuridhika na ramani aitakayo ili ye ye badala ya kujenga akabidhiwe nyumba iliyokwisha jengwa. Hati ya nyumba ibaki benki mpaka pale mkopaji atakapomaliza deni lake na kama mkopaji atashindwa, mkopeshaji hatakiwi na haja ya kutafuta ufilisi wa mali aliyonayo bali ni kuuza nyumba yenye na kupata fedha zake.

Kwa mantiki hiyo, nashauri mkopaji aingie mkataba na vikosi vya ujenzi kama vile J.K.T, Jeshi la Magereza na *contractors* wanaojulikana (waaminifu) na benki iwe mlipaji baada ya kumaliza jengo kwa niaba ya mkopeshwaji; utaratibu huu utasaidia sana: Kuona kweli dhamira ya mkopo ule inatimizwa; nyumba inavyojengwa ina viwango vinavyokubalika; na upangaji mzuri wa ramani ya nyumba na kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri; katika hali hii tunayotaka kwenda nayo sasa, pana haja kubwa ya kuanzishwa kwa Benki ya Nyumba kama vile tunavyotaka kuanzisha Benki ya Kilimo na Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa fika kuwa, Wizara ya Ardhi sio chombo cha Muungano na unaelewa Sheria za Ardhi (Wizara hizi) kila moja ina sheria zake.

Tanzania ni moja; je, kwa wale walio upande wa pili wa Muungano kwa maana ya Zanzibar; wakihitaji huduma/mkopo huu wafanye nini au watafaidika vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Pamoja na nia nzuri ya serikali kwa wananchi wake, lakini bado serikali inawajibika kutoa mchango wake katika kuboresha benki zake kwa kuziongezea mitaji mikubwa mfano *T.I. Bank, BANKCOP*, kwa kuzingatia itakuwa inajali na kuratibu vizuri mapato ya uwekezaji huu, kwa kuwa serikali haina fedha za kutosha lakini pia inaweza kuomba msaada kupitia taasisi ya kimataifa kama Shirika la Makazi ya Binadamu - *UN HABITAT*. Mwisho, naiomba serikali ipeleke wataalam nje katika nchi ambazo mpango huu wameanza kuufanya zoezi kwa muda mrefu. Kwa kuwa zoezi hili litakuwa ni mkombozi kwa wenye vipato vyema elimu ya kutosha ingeanza kutolewa katika Wizara zote na wananchi kwa jumla.

Pia napendekeza zoezi hili lipewe kipaumbele zaidi kwa walimu, wanajeshi na manesi kabla ya mikopo hii kuelekezwa kwa wengine. Si vibaya watumishi hawa ndio ingekuwa ni *pilot project*, ingependeza sana.

Serikali pia ingeanza kupanga wanasheria waliobobea katika kusimamia mikataba ya walengwa.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyopo mbele yetu ina umuhimu wa kipekee kwa Watanzania. Kwa bahati mbaya na bila sababu za kujitosheleza, wananchi hawakupewa fursa ya kutoa maoni na Miswada hii imeletwa kwa Hati ya Dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli sheria hii itawanufaisha Watanzania wengi wa kipato cha chini na kati? Je, upo uwiano wa mapato/mishahara na gharama za kununua nyumba leo? Je, watanzania wangapi amba wana uhakika na ajira zao na kuweza kulipa mikopo hiyo?

Je, hawa amba watajenga nyumba (*Estate Developers*), watakuwa tayari kujenga nyumba katika miji midogo na miji inayokua hata vijijini ili hao Watanzania amba wameahidiwa maisha bora waweze kukopa nyumba hizo; au sheria hii itanufaisha watu wa mjini tu, miji ambayo inakidhi haja na matakwa ya hao watakaowekeza katika kujenga?

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu yangu watakaonufaika si Watanzania wengi kama wanavyotaka tuamini kwamba, sasa maisha bora kwa kila Mtanzania kwa maana ya kupata makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa haki ya kusikilizwa mahakamani kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri. Kama sheria inafunga haki ya kukata rufaa, inapingana na Katiba; hivyo ni jambo ambalo tunapaswa kuliangalia vyema, haki zote zinazotolewa na Katiba ni lazima ziheshimike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MHE. MASOLWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Miswada yote miwili, ambayo ina malengo mazuri ya kuinua hali za wananchi hasa kwa kuwa na nyumba bora na za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba ya kisasa bali ya gharama nyingi pia unahitaji utaalam kwa maana ya taaluma ya ujenzi wake kuitia makandarasi. Kwa kuwa wananchi wengi hawana uwezo wa kumpa mkandarasi kujenga nyumba yake, ninashauri kuwa *NHC*, *TBA* na mashirika mengine ya umma kama vile *NSSF*, *PPF* na kadhalika, yapewe majukumu ya kujenga nyumba hizo ambazo wananchi watakopeshwa kwa riba ndogo na mikopo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia kuwa nyumba zitakazojengwa kwa ajili ya mikopo/kuuziwa wananchi, zijengwe kwenye miji midogo na mikubwa nchini kote, ambako uvamizi wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ni wa kiwango cha juu, kitu ambacho kinasababisha kuwa na miji iliyojengeka kiholela. Kwa mantiki hii, endapo mashirika haya yatachukua dhamana ya ujenzi wa nyumba za mikopo, miji yetu itakuwa imejengeka kwa mpango na ujenzi holela utapungua kama si kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza pia kuwa nyumba zitakazojengwa hasa kwenye miji, zianzie ghorofa mbili ili kutumia vizuri ardhi yetu ambapo idadi ya watu wanaongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *TBA* na *NHC* zinafanya kazi zinazofanana, ninapendekeza kuwa mashirika haya yaunganishwe na kupewa uwezo zaidi kifedha ili yajenge nyumba nyingi zaidi na kuzikopesha/kuziuza kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wengi wanapomaliza muda wao wa utumishi, huambulia kuishi kwenye nyumba duni, ninapendekeza kuwa kila Mbunge alazimishwe kwa kukatwa mshahara wake, kujengewa nyumba kwa njia hii ya mkopo katika eneo atakalopendekeza mwenyewe ili uwe mfano kwa wananchi wake.

MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono Miswada yote miwili ya Sheria ya Utoaji wa Miliki za Sehemu za Majengo wa Mwaka 2008 na Sheria ya Mikopo ya Nyumba wa Mwaka 2008.

Miswada hii ingepaswa kuja hapa Bungeni juzi, kutokana na kilio cha wananchi kuhusu maendeleo ya makazi ya kuishi siku nyingi. Hivyo, naunga mkono kuileta hapa Bungeni kwa Hati ya Dharura. Hii ni dhahiri inatokana na dhamira na nia njema ya serikali hii. Hongera sana kwa hatua hii.

Miswada hii ni moja ya njia na mkakati mmojawapo wa kuwawezesha wananchi wa kawaida na kati maana sasa watapata mikopo ya kupata/kununua nyumba au mafleti kwa kuishi wao na familia zao.

Fursa ya kumiliki sehemu ya majengo ni suala muafaka, mwenye sehemu hiyo ataishi kwa uhakika. Aidha, hati miliki hiyo anaweza kuitumia kwa kupata mkopo kwa shughuli nyingine za maisha yake na ya familia yake.

Kujenga nyumba kutoka mfukoni mwao siyo sahihi na inachukua muda mrefu kujenga nyumba au kununua fleti. Ni muhimu pia kuzingatia viwango vya riba kutoka katika mabenki ya biashara, ingawa baadhi yameanza kutoa mikopo kwa riba nafuu. Ni muhimu pia kwa serikali kuanzisha tena Benki ya Nyumba. Kinachotakiwa ni kutengeneza kanuni mwafaka ili benki hii isifilisike.

Suala la kuandaa miundombinu katika maeneo ambayo nyumba zitajengwa ni muhimu sana. Miundombinu hii ni barabara (mitaa), umeme na maji. Hili litasaida kuharakisha ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Uongozi wote wa Wizara, kwa kuleta Miswada hii mizuri wakati huu. Mimi naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri kuwe na uwezekano wa rufaa baada ya maamuzi ya Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi.

- Ili kupunguza madhara kwa wakopaji, ingekuwa vizuri nyumba inayojengwa ndio iuzwe kufidia mkopo, labda kama thamani yake haijafikia kiwango cha mkopo.
- Muswada uweke viwango vya hali ya juu katika ujenzi wa nyumba. *Quality construction must be highly enforced.*
- Umakini uwepo katika kuweka riba na muda wa kujenga ni muhimu.

MHE. MAULIDAH ANNA KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kuishukuru serikali kwa kukaa kufikiria jambo muhimu kama hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Tanzania wanaomba na kukaa kuwaza ni lini na wao wataweza kuishi maisha mazuri; maisha mazuri kwanza kukaa kwenye nyumba safi na nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, serikali iangalie sana Watanzania hawa ambaa ndio tunalenga kuwasaidia waishi kwa raha. Sasa kama tutatoa nafasi kwa kuwapa matajiri wenye nacho wajenge majumba hayo na kuyakopesha au kuuza, basi hapo ni kuwanufaisha zaidi matajiri na kuwaacha Watanzania wakiendelea kuishi kwenye dimbwi la nyumba mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri na wote wataoshughulikia mpango huu, naomba nianze kwa kusema/kuandika yafuatayo:-

1. Wale wote ambao tayari wamepanga ndani ya Nyumba za NHC, wapewe kipaumbele kupata nyumba hizo.
2. Wale wapangaji wa muda mrefu wa Nyumba za NHC waangaliwe muda walioishi ndani ya nyumba hizo, thamani ya nyumba hizo na kodi waliyolipa kwa muda wote waliokaa humo ili zikatwe kwenye fedha ambazo itabidi walipe.
3. Shirika la Nyumba la Taifa liwe makini sana katika kutekeleza sheria zinazowekwa bila ya kuwepo upendeleo.
4. Shirika la Nyumba la Taifa lichukue mpango huu wa kujenga nyumba hizo, hasa kwenye maeneo mengi yaliyo wazi na kuwa na ubia na benki yoyote ya taifa hili, kwa kutoa mikopo na kupokea marudisho. Utaratibu unaopendekezwa kuzingatiwa kwa wale watakaokopeshwa nyumba za NHC.
5. Kukaa na kufikiria njia ya mkopaji yoyote ataposhindwa kurudisha mkopo, benki ifanye nini bila ya kumwathiri mkopaji huyo.
6. Kuwa na uhakika wa yejote atakayepewa mkopo huo anaurudishaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukopa ili mwananchi aweze kujenga nyumba yake na baadae arudishe mkopo huo, naomba kushauri yafuatayo:-

1. Mwananchi anaeomba mkopo wa kujenga nyumba yake yeye mwenye angaliwe kwanza uwezo wa marudisho.
2. Akabidhi hati ya nyumba hiyo kwenye taasisi atakayokopa mpaka atakapomaliza deni, ili asije akachukua mkopo maeneo mengine kwa kutumia hati hizo hizo.
3. Pindi mhusika akifariki, serikali iangalie upya yule atakayechukua fursa ya kuendeleza deni hilo, ili warithi wasije wakanyang'anywa haki hiyo, kwani inawezekana yule aliyechukua akawa ameshalipa fungu kubwa la deni, lililobaki ni dogo lakini akalipa na kuchukua jengo hilo kwa kusingizia kwamba amemaliza deni.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuomba tena na tena, Mheshimiwa Waziri na Watendaji kama ambavyo kwa moyo safi tunalileta jambo zuri hili, basi naomba na utekelezaji usiwe wa vituko, tusitake malipo ya matendo mazuri tuyatendayo basi malipo yawe ya hapo kwa hapo. Tukumbuke sisi ni wanadamu na malipo mema tunayahitaji huko tuendako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono mia na mia na sabini na saba.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Waziri wa Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa hotuba nzuri. Vilevile nawapongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa maoni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kiwepo chombo muhimu cha kushughulikia (Benki Maalum) kwa ajili ya mikopo.

Wananchi wa kawaida hawatanufaika na mpango huo kwa sababu hawana cha kuweka rehani.

Wakazi wa miji midogo (Wilayani na Mji Mdogo kama Sirari), hajapimwa na wananchi wana uwezo wa kujenga na wana nyumba za kuweka rehani lakini hawana hati miliki za nyumba. Wananchi hawakushirikishwa kwanza katika hatua za awali. Manufaa ya mpango huu yatanufaisha wananchi wa mjini tu na kwa wale wenye uwezo tu. Kwa hiyo ni vyema Wizara iangalie namna gani wananchi (mwananchi) wa kawaida, atawea kukopa na kitu gani mkulima ataweka rehani.

Pawepo na Shirika la Kujenga Nyumba, wananchi wataenda kukopeshwa.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Muswada huu kuletwa. Muswada huu ulenge kuondoa upungufu unaohusu taratibu za kisheria hasa katika mfumo wa Mahakama. Hivyo, mizania ya haki ya mkopaji na taasisi inayotoa mikopo izingatiwe ipasavyo.

Kesi za *Mortgage Financing* kwa nini zisikilizwe na Mahakama Kuu peke yake Kitengo cha Ardhi kwani Mahakama Kuu zipo chache nchini sio mikoa yote hivyo haki inaweza ikacheleweshwa. Nashauri kesi za *Mortgage Financing* zisikilizwe na Mahakama za Wilaya na Mkoa Kitengo cha Ardhi.

Naipongeza nia ya Muswada huu kuwezesha watu wengi kumiliki sehemu ya jengo (*condominium*). Natoa rai, nia hiyo isitumike vibaya au tofauti.

I do expect that this Unit Titles Bill will give more freedom to bodies corporate to run their developments.

The Act only states the powers and duties of the body corporate (association) in general terms. There is not enough specific help for body corporate members to understand what they should do and the minimum acceptable standard they must work to.

The Act (Bill) does not clearly define roles, responsibilities and relationships. Unit owners and tenants may not know how much about the body corporate works, and may not be sure about who is doing what, how well they are doing it and who they are responsible to.

Part II (creation and registration of units). 6 (3); The common areas of the property shall include: (a) (b) (c) (d), as agreed by co-owners, his can be swimming pool, gym, parking. 9(3) liongezwe neno Mortgage.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jambo hili ni jipya sana nchini, yapo mambo ambayo yanahitaji ufanuzi wa kutosha. Muswada unapaswa ufanue wajibu, majukumu na mahusiano (roles, responsibilities and relationships). Nani anafanya nini, jinsi gani ya kufanya na wanaowajibika kwa nani.

Mfano: Association - maamuzi yake ni yapi; Committee - maamuzi yake; Co-owners, unit – owners; Developer; Administrator; na Professional Body – Corporate Managers.

Ili mahusiano yasiwe magumu kati ya Tenants, absentee, landlords, body corporate na kadhalika, haya yatasaida maintenance and management of common property record-keeping, insurance, etc.

Mahusiano yanapaswa kuonyesha nani anawajibika kwa nani; mfano, committee to association (body corporate); can association delegate its powers to the committee. Kwa kuwa kutakuwepo na rules (kanuni); je, Landlord akiwa hayupo basi agent atawajibika wapi na Agent atapaswa kuhakikisha kuwa kanuni zinafuatwa?

Mahusiano yakiwa clear, maamuzi yanaweza kufanyika haraka na hivyo kurahisisha sana operations za Unit Titles.

Aidha Part IV S. 70; where there is no incase of dispute choice of the court will be a problem due to value; I advice agrieved party aende Mahakama ambayo ina-jurisdiction.

Muswada huu utasaida kupunguza umaskini, wapo watu ambao wana kipato fulani lakini viwanja vinapatikana nje ya miji ambako maji/umeme havipo na akianza kujenga peke yake inakuwa kazi. Lakini kama kutakuwa na wawekezaji wengi wakawekeza majengo makubwa ni rahisi huduma kama umeme, mabasi, maji, public transport kufika eneo husika na maendeleo yakaenda haraka. Pia itawezesha kuendeleza miji midogo kukua haraka sana.

Utekelezaji wa Mortgage Finance uanze mara moja, mabenki yapunguze urasimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Watumishi wote, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zangu ni kama zifuatazo:-

Jambo hili litaleta maendeleo ya haraka kwa watanzania wengi, lakini naiomba serikali uwepo utaratibu au kamati mahususi, itakayohakikisha kuwa, kwa vile wenye uwezo wa kujenga majengo makubwa hapa kwetu ni Wahindi au matajiri wenye asili nyingine, Watanzania wengi hawana uwezo.

Hofu yangu kubwa; inawezekana hawa aina moja ya kabilia (Wahindi), watawauzia flati hizo Wahindi watupu, Watanzania yaani *natives*, hawatapata fursa hiyo. Serikali ihakikishe kuwa, dhana aliyokuwa nayo Baba wa Taifa ya kufanya Miji ya Tanzania isionekane kama India; Mumbai au Delhi. Alichukua hatua ya kutaifisha majumba yote na kumpa jukumu la umiliki Msajili wa Majumba (NHC). Serikali iwalinde raia maskini nao wapate nyumba bora.

Sheria hii itaiongezea kazi Wizara yako. Sasa hivi kuna ucheleweshaji mkubwa wa kutoa hati miliki kwa kiwanja kimoja kimoja, lakini sheria hii inaleta hisia ya kuwepo viwanja vingi nya hewani, vinavyohitaji hati miliki nyingi.

Naiomba Wizara ipanue sana huduma za utoaji hati miliki kwa haya maghorofa. Upanuzi wake ndio njia bora ya kufanikisha maudhui ya sheria hizi.

Mortgage Financing ni ukombozi kwa Watanzania katika miaka ya 1960 – 1970. Kulikuweko Mortgage Financing hasa ya ujenzi wa nyumba. Watumishi wa benki ya nyumba wafanye kazi yao kwa uadilifu mkubwa. Kuna taarifa zisizo rasmi kwamba, iliyokuwa Benki ya Nyumba (*Housing Bank*) ilifilisika kabisa. Sababu yake kuu ni ukosefu wa uadilifu wa watumishi wa benki hiyo.

Tunaomba Serikali iwe makini kuvilazimisha vyombo nya fedha husika, vichunge na kufanya kazi kwa kutumia kanuni zilizowekwa na sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumpungeza Waziri, pamoja na Watendaji wake wa Wizara, kwa kutengeneza Miswada hii ambayo ni muafaka kabisa kwa nchi yetu na wananchi wetu; ambayo ni mategemeo yangu wengi tutafaidika nayo.

La kuangalia ni kwamba, sheria na kanuni zitekelezwe kama zilivyopangwa. Ihakikishwe kwamba, watendaji na watekelezaji waadilifu na hatua kali zichukuliwe kwa wale watakaokwenda kinyume. Kipaumbele kipewe kwa hao ambao tayari wamo kwenye hizo nyumba, kama watakuwa tayari kununua. Pia suala hilo la mikopo lizingatiwe vizuri sana, kutohana na uzoefu na matatizo yaliyotokea huko nyuma wakati wa Benki ya Nyumba. Bila shaka Miswada hii itakuwa ni ukombozi kwa wananchi wetu na taifa letu.

Nawatakia kila la kheri na naunga mkono hoja.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kuleta Muswada huu ambao ni muhimu sana kwa ustawi wa wananchi wetu.

Mchango wangu kuhusu *Mortgage Finance Act* ni kama ufuatao:-

- Kumekuwa na ugumu mkubwa wa ku-register title deeds kwa madhumuni ya kuweka dhamana kwa ajili ya mikopo mbalimbali.
- Naipongeza Wizara kwa kuliona hili na kupunguza mlolongo wa wahusika ili abakie Benki, Mkopaji na Msajili wa Hati na hatimaye Kamishna wa Ardhi ajulishwe tu utekelezaji wa jambo hili.
- Kuhusu ulipaji wa mikopo hasa kwa *defaulters*; pamekuwa na mtindo wa wakopaji wengi kukwamisha vyombo vya fedha na mabenki kwa kukimbilia mahakamani kwenda kuweka zuio la kuuza dhamana iliyowekwa kwa mkopo husika. Ni kutokana na tatizo hilo la *court injunction* mabenki na vyombo vya fedha vimeduwa *reluctant* kuwasaidia wananchi wengi kupata mikopo chini ya utaratibu huu.

Pamoja na kwamba sheria hii itaruhusu uuzwaji wa dhamana bila kuzihusisha mahakama, bila kuihusisha Wizara ya Katiba na Sheria ili ifanye marekebisho ya sheria inayoruhusu *court injunction* kutumika na *defaulters* kama kinga ya kuzuia kuuza dhamana ya mikopo husika.

Kama *Court Injunction Law* itaendelea kuwepo, uwezekano wa kutumia sheria hii kuuza dhamana haitatekelezeka.

Muswada wa *Unit Titles* umekuja kwa wakati na utawawezesha wananchi wengi kuweza kupata mikopo katika vyombo vya fedha kuliko ilivyo hivi sasa. Kwa sheria ya sasa, ilikuwa vigumu kutumia *flat* ya mtu moja kwa moja, kwenda benki na kusajili hati ya flat ile kama dhamana. Kwa sheria hii mpya, wananchi wengi watafaidika, kwa kuwa na *subtitle* yenye haki kamili ya umiliki. Kwa mantiki hiyo, umuhimu wa chama cha wenye *units* hizo ni muhimu sana ili kuzuia migogoro ya ardhi, ambayo huweza kujitokeza. Aidha, sheria hii izingatie adha ambazo wapangaji kutokana na utofauti wao wa hali ya maisha (*rich and poor*), (*young and old*), ili kusiwe na bugudha kama vile kelele kutokana na muziki, ibada zenyenye nyimbo na kadhalika.

Pia mazingira ya *units* hizo ziwekewe sheria ya kama nini kifungwe, kwa kuzingatia hali ya wapangaji. Kama ikiwa wapangaji wengi ni Waislamu isipokuwa mmoja na huyo mmoja wa madhehebu mengine akafuga nguruwe ni dhahiri italeta adha kwa wapangaji wengine. Kanuni za Muswada huu zizingatie hilo.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John Chiligati, Katibu Mkuu wa Wizara, Mama Sijaona, pamoja na timu yote ya Wizara hii.

Binafsi, naunga mkono hoja hasa kutokana na sababu mbalimbali zilizotolewa.

Mchango wangu hasa upo katika maeneo yaliyojengwa kiholela *especialy* Dar es Salaam. Je, serikali itajihuisha vipi katika kusimamia utwaaji wa maeneo ili kuwekeza nyumba kama za maghorofa na mwekezaji ambaye yupo tayari mfano eneo kama Manzese au Namanga, kwani naona inaweza kuwa ni ngumu *ku-negotiate* na mtu mmoja mmoja?

Kwa kuwa sheria hii imeletwa kidharura, ni vyema basi serikali/wizara itenye fedha kwa ajili ya kuwaelimisha wadau/wananchi ili fursa hiyo iweze kutumika vizuri.

Sheria ya Fidia ya Ardhi ni vyema pia ifanyiwe marekebisho, kwani fidia zilizopo zinalalamikiwa sana kuwa ni duni.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Muswada wa *Unit Titles* utaruhusu mwananchi kumilikishwa nyumba kwenye ghorofa (flats), hilo halina tatizo, lakini tuchukulie mfano Shirika la Nyumba limejenga nyumba; je, umiliki wa ardhi iliyojengwa hiyo nyumba utakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa inayotokana na kuwepo Miswada hii kwa wananchi ni kupata uwezo wa kujenga au kumiliki nyumba. Bila shaka wafanyakazi wa serikali, taasisi binafsi na mashirika ya umma, kupata mkopo wa ujenzi itatokana na kazi zao. Je, wakulima katika hilo watapataje mikopo wakati benki zetu zinasema wakulima hawakopesheki?

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja sasa kutokana na Miswada hii iliyopita kuwa sheria, basi utaratibu uwepo wa serikali kuanzisha Benki ya Nyumba ili wakulima na wao wapewe mikopo bila ya kurejea makosa yaliyofanywa na Benki ya Nyumba iliyopita na hatimaye kafilisika.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwafahamisha kuwa, kuna wananchi wanalamika mara kwa mara kuwa kuna wananchi wamekaa kwenye nyumba za NHC kwa muda mrefu sana. Serikali imewaaahidi kwa muda mrefu sana kwamba, watazinunua mpaka leo hawapati majibu, nyumba zenyewe zimechakaa sana, viwanja vyao vimefinywa wanakaa na wasiwasi sana. Sehemu zenyewe zipo Bukoba Miembeni. Zile nyingine za Kashai mbona wakazi walishazinunua wale wale waliokuwa wanakaa humo tuwape haki zao.

Je, Sheria hii inawasaidia vipi? Nitaomba msaada wako kwa majibu. Wananchi wanansumbua sana kujua hatima yao ni nini; viwanja vyao wanavigawa ofisi yako ya ardhi wanajenga.

Yangu ni hayo, Muswada mwema.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wake, kwa maandalizi mazuri ya Muswada huu. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada hii itawakombua wananchi wa kipato cha chini, ambao hawana uwezo wa kuwa na fedha za kutosha kujenga nyumba. Sheria hii ikipitishwa na kuwezesha watu kukopa, itapunguza sana vishawishi kwa watu kutafuta fedha kwa njia haramu au kutafuta fedha kwa kulazimisha rushwa kwa kutumia nafasi yake.

Sheria itasaidia vijana kuweza kukopa na kujenga nyumba wakiwa bado vijana na kuachana na vishawishi nya rushwa au fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonesha kuwa, mipango mizuri kama hii, inawasaidia zaidi watu wa mijini. Wale wa vijijini hawatafaidika kama ilivyo katika mikopo ya Mheshimiwa Rais Kikwete, kwani mabenki yatakayokopesha yapo mijini na watadai hawana watumishi wa kutosha wa kwenda vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri atanihakikishia vipi kwamba watafaidika vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu utawasaidia wananchi kama serikali itaunda Benki ya Mkopo kama ilivyokuwa Benki ya Nyumba miaka ya nyuma. Mabenki ya biashara hayatasaidia kufanikisha azma nzuri ya serikali na yanaweza kuigombanisha serikali na wananchi wake. Nasisitiza kuwepo benki maalum ya mkopo.

Nakubali wazo la kuwa na chama cha watakaomiliki ili kutatua matatizo au malumbano mionganoni mwao. Mfano mzuri ni mizozo ya wapangaji katika nyumba za mijini za vyumba sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza sheria hii itolewe elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BUJIKU PHILIP SAKILA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na serikali kwa ujumla, kwa kuleta Miswada hii nchini, inayolenga kuleta maisha bora kwa kila mtanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa Miswada yote hii miwili, ninayo maswali machache nitakayoomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha anisaidie kupata maelezo.

Je, ni Muswada upi kati ya hii miwili una manufaa ya moja kwa mwananchi wa kijiji hasa ukizingatia ukweli kuwa asilimia 70 – 80 ya wananchi wetu wapo vijijini? Je, wananchi wa vijijini watanufaika namna gani?

Je, ni kwa namna gani wafanyakazi waliopo katika taasisi zetu zilizoko vijijini na kwenye shule za sekondari, zahanati na vituo vya afya watafaidika?

Kadiri itakavyowezekana, ninaomba Shirika la Nyumba (NHC) na Vikosi vya Majeshi na Mashirika kama *NSSF* na kadhalika, washauriwe kuelekeza nguvu zao zaidi vijijini kwa kufunga mikataba na Halmashauri za Wilaya ili kupunguza upungufu wa makazi bora vijijini.

Mwisho, nazitakia kheri sheria zitakazotokana na Miswada hii ziweze kuwa endelevu kiutekelezaji kwa manufaa ya wananchi. Zitumike vyema sheria hizi bila kuongeza tofauti ya ubora wa maisha kati ya vijijini na mijini.

Sheria hizi zipitiwe mara kwa mara kujiridhisha kuwa hazongezi umaskini, kutokana na wananchi wengi kukosa kihalali uwezo wa kulipa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HARITH B. MWAPACHU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii uliyonipa kuchangia kuhusu hoja ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kuhusu Miswada ya *Mortgage Finance* na *Unit Titles*.

Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Miswada hii Bungeni na kwa kuiwasilisha vizuri. Aidha, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa uchambuzi wa kina wa Miswada hii miwili na kuiwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, imekuwa na mizuri sana, hasa maoni yaliyotolewa na Mheshimiwa Basili Mramba na Mheshimiwa Jenista Mhagama. Mimi ambalo ningependa serikali ilizingatie katika utoaji wa mikopo hii ni kwamba, tusifikirie kuwaendeleza wakazi mijini tu, fikra zetu zituelekeze jinsi ya kuboresha makazi katika *rural areas*. Hali ya makazi katika *rural areas* ni duni na inasikitisha iwapo tutataka kuboresha maisha ya Mtanzania itabidi suala la *Mortgage Finance* lazima liwekwe kwenye *larger perspective* ili kujibu uduni wa makazi vijijini. Hili suala ni changamoto kubwa kwa serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uwekezaji mijini, Miswada hii ikiwa sheria, kanuni zake ziangalie vipi mikopo na majengo hayo yatajibu masuala ya msongamano ndani ya miji yetu. Isitolewe mikopo kiholela, bila ya kuzingatia nia ya kupunguza matatizo ya wakazi wa miji; msongamano wa watu, miundombinu ya maji safi, maji taka na kadhalika. Kwa maana nyingine, dhana ya kujenga *clearer cities* inazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamekuwepo maoni kwa mfano kwamba, Jiji la Dar es Salaam limejengwa ovyo ovyo na kwamba, asilimia 75 ingefaa kujengwa upya. Je, *programme* hii ya mikopo itakuja na vigezo gani nya kuendeleza miji yetu kwa nia hii niliyoitaja?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Wizara ikatoa mwongozo kwamba, katika kutoa mikopo hii, taasisi za usalama pia zitahusishwa, kama vile Polisi, Zimamoto ili mitaa/majengo yaweze kufikiwa ili zipate huduma stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ningependa niwashukuru wale wote waliochangia katika mada hii. Kuna waliochangia kwa kusema ndani ya ukumbi huu, kuna waliochangia kwa maandishi, kuna wengine walipenda kuchangia lakini muda haukutosha, wote hawa napenda niwashukuru sana. Wote waliochangia wameunga mkono hoja, pamoja na kupewa tahadhari za hapa na pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la mikopo ya nyumba limekuwa linazungumzwa kwa muda mrefu sana, karibu miaka mitatu, katika vikao vingi sana nya wataalamu na wadau. Wakati tunazungumza miaka mitatu, Watanzania wamekuwa wanasesubiri, wanataka kujenga nyumba wameshindwa kujenga nyumba kwa sababu fedha hawana, leo jambo ambalo tumelifanya ni jambo ambalo Watanzania wamesubiri kwa muda mrefu na jambo ambalo litawasaidia sana. Nataka niwashukuru sana Wabunge, kwa jinsi mlivyopokea jambo hili kwa uharaka wake na jinsi mlivyotoa hoja ambazo zinalenga kujibu kiu na kilio cha Watanzania katika suala zima la kujenga nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ya utangulizi, naomba niwatambue kama ilivyo ada wale waliochangia. Kwanza, waliochangia kwa kauli nimtambue Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi na Mheshimiwa Joseph Mungai.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Saverina Mwijage, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Bakar Mwapachu, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Dr.

Ngasongwa, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir na Mheshimiwa Chacha Mwera Nyanguru. Narudia tena kuwashukuru sana kwa michango yao iliyotusaidia kuboresha hoja yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika kujibu hoja zenyewe, nianze na hoja zilizotolewa na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira zilizotolewa na Mheshimiwa Job Ndugai, kwa niaba ya Kamati. Kwanza, walikuwa na wasiwasi kuhusu ushirikishwaji wa wadau; wasiwasi huu vile vile ulionyeshwa na Kambi ya Upinzani. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, jambo hili limeshirikisha watu wengi kwa takriban miaka mitatu. Watu wa vyombo vya fedha, Mabenki, yameshirikishwa kwa ukamilifu kabisa. Benki Kuu ambaye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli hii amehusika katika kila hatua mpaka hapa tulipofika. Vilevile Chama cha Wapangaji Tanzania ambao wamepanga katika nyumba mbalimbali, wana chama chao na tumeshakaa nao zaidi ya mara tatu na wao vilevile wametoa maoni katika suala hili. Makampuni yanayoshughulika na ujenzi wa nyumba za binafsi na ya umma kama *National Housing, NSSF* na wengine wote ambao wanashughulika na ujenzi vilevile wameshiriki. Kwa hiyo, ucharaka wa leo haina maana kwamba, jambo hili limeanza leo leo; limeanza muda mrefu watu wengi wameshiriki ila kosa ni kwamba tumechelewa, lakini katika kulijadili wadau mbalimbali wameshiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa kwamba, nafuu inayoletwa na sheria hizi mbili zinawafikia na watu wa chini na watu wa kati ama inakwenda kuwanufaisha matajiri. Hoja hii imezungumzwa na Kamati, vilevile imerudiwa na Kambi ya Upinzani. Lengo hasa la sheria hizi mbili ni kuwasaidia watu wa kati na watu wa chini. Matajiri tayari wanajenga bila ya sheria hizi, wanazo fedha za kujenga tu. Pale Dar es Salaam utakuta maghorofa tu, kwa hiyo, sheria hii inawalenga hasa watu wa kawaida, watu wa chini wote wa mijini na vijijini ili nao waweze kujenga ama waweze kununua. Kwa kuanzia, kwa sababu mahitaji makubwa sana ya kujenga yapo mijini, tunapoanza ni kweli mijini ndio watanufaika zaidi; lakini jinsi tunavyokwenda, jinsi sheria hii itakavyozoleka na vijijini wanavyojitayarisha hatimaye vilevile itafika mpaka vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati vilevile imeeleza habari ya elimu kwa umma, wamesema sheria hii lazima umma uelimishwe ili waitumie. Nataka kulifahamisha Bunge hili kwamba, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine hasa TAMISEMI na Mashirika mbalimbali, *NGOs* na wengine wote, tutasaidiana kufikisha elimu hii kwa umma. Ndio maana katika ile sheria ya mikopo na zote hata ile ya kuuza sehemu za majengo, Wizara yangu imelazimishwa kwa mujibu wa sheria, tuitafsiri sheria hiyo kwa Kiswahili ili kuharakisha zoezi la kuelimisha umma kuhusu yaliyomo. Vilevile Kamati imetahadharisha kwamba, mpango huu wa mikopo ya nyumba umeleta matatizo kule Marekani; je na hapa nchini tumejiandaaje? Hoja hii vilevile imerudiwa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, hivi sasa soko la duniani linayumba, sehemu kubwa imetokana na hii mikopo ya nyumba. Sasa matatizo yametokea, sisi hatuwezi tukasema kwa sababu Marekani imekumbwa na tatizo hili tuache. Mikopo ya

nyumba ni jambo jema, linafanywa kila mahali duniani, sisi tumechelewa lazima tuingie. Kilichotokea kule ni ajali tu; ni kama mtu ameanguka na ndege; sasa hamuwezi kusema kwa sababu ndege ilipata ajali juzi basi hatuwezi kupanda tena; tutapanda tu umakini ndiyo unaotakuwa. Kwa hili wote wanahuksika; mabenki yanayohusika, Benki Kuu na sisi Wizara tunayohusika tutaliendesha jambo hili kwa umakini sana ili mikopo hewa isitolewe na baadae utaratibu huu upate matatizo kama ilivyotokea kule Marekani hivi sasa.

Kambi ya Upinzani, moja ya hoja kubwa waliyoitoa ilikuwa ni kwamba, kwa nini suala hili limeletwa kwa haraka, kuna nini? Kama nilivyo sema kwamba, suala hili limechelewa, Watanzania wengi hawana uwezo, leo hii takwimu zinaonyesha kwamba asilimia 70 ya Watanzania wanaishi katika nyumba duni, si kwa sababu wanapenda kuishi katika nyumba duni ni kwa sababu hawana uwezo. Sasa Sheria hizi zinawaleta uwezo, inakuja kutatua tatizo, mgonjwa huyu analetewa dawa. Sasa wenzetu wa Upinzani wanasema kwa nini dawa hii mnaharakisha harakisha? Anayesema kwa nini mnaharakisha dawa labda ni mchawi, maana mchawi peke yake ndiyo atalaumu kwa nini wewe unaharakisha dawa, lakini mtu mwenye nia njema atakusifu. Hapa tulitakiwa tusifiwe kwamba, jambo hili tulilileta haraka ili kutatua tatizo kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kilichokuwa kinatokea ni kuingiza tu siasa za ushabiki katika jambo nyeti na kubwa kama hili na hili si jambo jema. Tungependa katika kujenga utamaduni wa vyama vingi, lile jambo la msingi lenye maslahi makubwa ya wananchi, tuungane vyama vyote bila itakadi zetu. Wenzetu kote dunia nzima ndivyo wanavyofanya, kuna mengine mnabishana. Jambo lenye neema kubwa la ukombozi kwa Watanzania tunaungana wote pamoja. Sasa hili lilishindikana mpaka rafiki yangu mmoja ambaye naye alishiriki kwenye Kamati ya Uongozi analijua jambo hili, anafika ndani ya Bunge tena anaanza kuhoji imekuwaje; yaani yote hii ni ushabiki wa kisiasa. Napenda kusema kwamba, tuache ushabiki wa kisiasa katika mambo yenye maslahi makubwa ya wananchi. Tuungane kabisa, ndivyo wenzetu wanavyofanya katika nchi nyingine. Kwa hiyo, naomba tujenge utamaduni ambao leo niliona kama tulipepesuka kidogo labda ilikuwa bahati mbaya, lakini bahati mbaya katika jambo kubwa kama hili si jambo jema. Yote kwa yote hatimaye na wao wameunga mkono, kwa hilo nawasifu kwa sababu wangeacha kabisa kuunga mkono, ndiyo ningethibitisha kabisa kuwa ni wachawi. Waliunga mkono kwa sababu waliona kwamba ni jambo jema kwa Watanzania na lina maslahi kwa Watanzania. Kwa hili, Kambi ya Upinzani nawasifu kwa sababu mmeonyesha mafano mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani walionyesha tahadhari kuhusu madhara ya Sheria hii kwamba, inawezekana Watanzania wakapoteza nyumba zao, watashindwa kulipa mikopo, zitauzwa, watakuwa maskini. Nadhani tahadhari ni nzuri lakini nia ya Sheria hii vilevile tunataka kujenga utamaduni mpya wa Watanzania; kwanza wajue kwamba, maendeleo hayatakuja bila kukopa. Watanzania wanaogopa wanadhani wanaweza kupata maendeleo kwa hela zao za mfukoni, haiwezekani. Kwa sheria hii tunataka Watanzania wakope. Amezungumza vizuri sana Mheshimiwa Mhagama akasema, kama huna deni utakuwa huna msukumo kwa sababu hudaiwi na mtu basi unafanya unavyotaka. Lakini kama una deni kuna kitu kinakusukuma, hicho

kinachokusukuma ndiyo maendeleo yenewe na dunia ya sasa mtu mwenye heshima ni yule mwenye deni.

Kwamba, huyu anakopesheka, anaaminika na mtu wa maana ndiyo dunia na uchumi wa leo. Mtu ambaye hana deni siku hizi haheshimiki, hakopesheki. Kwa hiyo, Sheria hii inataka tuanze utamaduni wa kukopa na tulipe. Tukifika hapo, ule wasiwasi wa Kambi ya Upinzani kwamba nyumba za watu zitachukuliwa na Mabenki utakuwa haupo, kwa sababu umekopa, una nidhamu ya kutumia mkopo katika jambo ulilokopea, una nidhamu ya kurudisha, wasi wasi uko wapi? Wenzetu duniani kote ndivyo wanavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa vilevile kuna hoja kwamba, wapangaji wa *National Housing* watafukuzwa ili wapewe ndugu zao na baadae waje wauziwe. Sasa hili nataka niliweke vizuri, isitafsiriwe kwamba, Sheria hii maana yake kesho nyumba za *National Housing* zinaanza kuuzwa, hiyo sio tafsiri yenewe; tafsiri yake ni kwamba, tunataka *National Housing* nao wapate hii mikopo, wajenge hizo *flats* wauze kwa maana ya kuingia katika biashara ya kujenga na kuuza. Hawa waliopo sasa hivi si kwamba moja kwa moja wanauziwa *cash*. *National Housing* watatazama hali ya mwenendo wa soko, wakiona wanapata manufaa kwa kuziuza basi watazuza watawamilikisha na Sheria inaruhusu. Sasa isichukuliwe kwamba, Sheria hii maana yake nyumba zinaanza kuuzwa kesho, hapana. Watatazama waone hali ya soko itakwendaje, kama wakiuza watapata manufaa basi watauza. Sheria hii inabadilisha mwenendo mzima wa *National Housing*. *National Housing* baada ya Sheria hii kupita, hawatajenga nyumba ili wapangishe mtu uanzu kufukuzana naye kila mwisho wa mwezi kudai kodi. Huko wanaondoka wataingia katika biashara ya kujenga majumba na kuuza. Hawa waliomo sasa hivi hali ya biashara itatazamwa kama wauziwe au wasiuziwe, wakiamua kuuziwa Sheria inaruhusu na watapa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie katika hoja za Mbunge mmoja mmoja ni nyingi, mtaniwiwa radhi kama sitazimaliza maana muda wangu ni mfupi. Hoja ya kwanza ni uwezekano wa upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, mijini na vijijini na upatikanaji wa mikopo kwa watu wa chini. Hoja hii imetolewa na watu wengi akiwemo Mheshimiwa Arfi, Mheshimiwa Masolwa, Mheshimiwa Mwapachu, Mheshimiwa Missanga, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Zuleikha Yunus, Mheshimiwa Ali Khamis na wengine wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika maelezo ya mwanzo kwamba, lengo la Sheria hizi ni kuwasaidia watu wa mijini na vijijini wapate mikopo. Kwa hivi sasa mahitaji makubwa ya kujenga nyumba yapo sehemu za mijini. Kwa hiyo, kwa mwanzo mwanzo huku mikopo mingi itakwenda mijini kwa sababu ndiko yalipo mahitaji makubwa. Vilevile huko vijijini kama mtu naye anataka kukopa na nyumba yake ina dhamana, ana kiwanja chake ambacho ameshapimiwa na ana hati, anayo fursa, vilevile ipo kwa watu wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya mambo ya kuzingatia katika kuza nyumba za *National Housing* yametolewa na Mheshimiwa Maulidah Anna Komu na

Mheshimiwa Zuleikha Yunus. Kama walivyosema kwamba, Sheria hii hailengi moja kwa moja, *National Housing* wanaenda kuuza nyumba zao kesho ila Sheria hii inataka *National Housing* wakitaka kujenga na kuuza Sheria inawaruhusu, wakitaka kuuza hata nyumba zilizopo sasa hivi Sheria inawaruhusu na ni wao wenyewe wakikaa na kutazama kama wanapata faida zaidi wakiwauzia waliopo kwenye maghorofa sasa Sheria inatoa ruhusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja kuhusu kuzingatia viwango vya riba katika Mabenki ya Biashara ambayo imetolewa na Mheshimiwa Dr. Ngasongwa na Mheshimiwa Rished Abdallah. Sasa suala la riba ni kwamba, Miswada hii inalenga kujenga utamaduni wa Watanzania kupata mikopo na pia kujenga nidhamu ya kurejesha mikopo. Mswada pia unalenga kuondoa ujanja ujanja ambaa ulikuwa unatumiwa na watu kukimbilia mahakamani ili kukwepa mkopo. Riba bado zitaendelea kutazamwa na Benki Kuu. Kwa hiyo si kweli kwamba, yule ambaye anakukopesha leo kwa riba kadhaa, kesho kutwa tu anaamka peke yake anaanza kupandisha riba holela, hapana. Ni lazima Benki Kuu ndiye mdhibiti wa Benki zote na taratibu zote za fedha na itadhibiti vilevile na suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Benki zinakopesha mikopo ya biashara, ndiyo maana ni ya muda mfupi na riba ni kubwa. Tukiingia kwenye mikopo ya nyumba, watakopeshwa kwa muda mrefu, miaka kumi na kuendelea na riba itakwenda chini na Benki Kuu itaendelea kutazama mtiririko mzima wa riba sio kila Benki kijiwekea riba jinsi inavyopenda. Uanzishwaji wa Benki ya Nyumba, hili wazo limetolewa na Mheshimiwa Dr. Ngasongwa na Mheshimiwa Profesa Mtulia, Mheshimiwa Hamis Seif, Mheshimiwa Ndesamburo na Mheshimiwa Zitto Kabwe. Kwa Sheria hii, hatuna maana kwamba tunaanzisha Benki ya Mikopo ya Nyumba. Kwa Sheria hii tunafungua tu milango kwa Benki za kibiashara zilizopo, vilevile zifungue dirisha, zikopeshe mikopo ya muda mrefu. Kwa hiyo, wengi watakaokuwa wanakopesha ni Mabenki haya haya ya binafsi, yataundwa makampuni ya kutoa mikopo ya nyumba za binafsi, lakini sisi Serikali kwa sasa hivi hatuna mpango wa moja kwa moja wa kuanzisha Benki ya Nyumba. Sisi Serikali kupitia Benki Kuu, tutadhibiti mwenendo mzima wa mikopo ya nyumba. Sisi wenyewe hatutaingia moja kwa moja kwenye biashara ya mikopo ya nyumba.

Hoja nyingine ilikuwa ni elimu kwa umma kuhusu fursa zinazotolewa na Miswada hii. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Fuya Kimbita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema katika maelezo yangu ya mwanzo, ipo haja ya kutosha kabisa kueneza elimu kwa umma kuhusu jambo hili. Tutafanya Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI na *NGOs* mbalimbali ili wananchi waielewe vizuri Sheria hii, waelewe vizuri fursa hii na waitumie. Maendeleo ni jinsi unavyotumia fursa zinazokuja pamoja na fursa hii. Hoja nyingine ilikuwa namna ya watumishi wa umma wanaofanya kazi vijijini watakavyonufaika na utaratibu huu, imetolewa na Mheshimiwa Bujiku Sakila. Kama nilivyosema kwamba, Sheria hii inalenga kuwanufaisha wote wa mijini na vijijini; mtumishi wa kijijini kama ana hati yake kule ya kumiliki shamba au kumiliki *plot*, anaweza nae pia akaitumia kupata mkopo

wa nyumba. Vilevile Sheria hii inaruhusu taasisi mbalimbali kama NSSF, PPF na wengine wakope wajenge. Halmashauri zinaweza zikakopa zikajenga, zikawauzia wafanyakazi wao. Kwa hiyo hili linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ya haki ya kikatiba ya kukata rufaa iangaliwe vyema katika Sheria imetolewa na Mheshimiwa Arfi, Mheshimiwa Prof. Maghembe na Mheshimiwa Ligallama. Sheria jinsi ilivyo, haifungi milango kwa mtu aliyekopa kwenda katika Mahakama ila tu imeweka vigezo ili watu wasiende mahakamani kwa jambo ambalo halina maana kwa kuchelewesha kulipa tu. Hiyo milango ya kuchelewesha chelewesha kulipa kwenda Mahakamani kwa sababu ambayo haina msingi hiyo kweli imefungwa.

Kimsingi bado anaweza akaenda na misingi imewekwa kwa mfano, ameshamaliza kulipa deni lakini yule aliyemkopessa bado anamdaa isivyo halali, basi atatafuta haki yake Mahakamani na Mahakama ya kwenda imeonyeshwa pale ni Mahakama Kuu, Kitengo cha Ardhi. Endapo hujachukua mkopo lakini unadaiwa tu, Sheria inaonyesha mahali pa kwenda kulalamika. Kama ulikopa mkopo wa milioni 50 umeshindwa kulipa, nyumba imeuzwa kwa milioni 60, sasa zile kumi hataki kukurejeshea kwa sababu deni lake umeshamlipa hataki kukupa zile, Sheria katika mazingira haya inakuruhusu kwenda Mahakamani. Kwa hiyo, nafasi haijazibwa mia kwa mia ipo; ila imezibwa kwa wale wanaokimbilia kule kwa visingizio visivyo na mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine Sheria izingatie kudhibiti adha ambazo wamiliki wa sehemu za majengo wanaweza kuzipata. Hoja hii lilitolewa na Mheshimiwa Ligallama. Sheria inaunda umoja wa watu wanaokaa katika hilo jengo ni kwa mujibu wa Sheria na hiyo *Association* itakuwa na nguvu ya kisheria ili kusimamia adha zote ambapo mkorofii mmoja anaweza kufanya maisha yakawa magumu kwa wenzake. Kwa hiyo, Sheria imeweka huo utaratibu wa jinsi ya kuondoa adha kwa wapangaji wenzako.

Sheria ya fidia ya ardhi ifanyiwe marekebisho, kwani fidia sasa hivi ni duni. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999 inasema kwamba, pale ambapo mtu anafidiwa, lazima afidiwe kwa kadiri ya hali ya soko ya wakati ule. Kwa hiyo, kama ni nyumba atafidiwa kwa hali ya soko kwa wakati huo; je, bati sasa hivi ni shilingi ngapi, bei ya mbao, bei ya mfuko wa *cement*, kwa mujibu wa soko. Kama ni mazao ni hivyo hivyo kwa mujibu wa soko, kama ni ardhi tupu vilevile ina thamani yake lakini inazidiana. Kipande cha ardhi pale katikati ya Dar es Salaam bei yake haitafanana na ardhi ya kule kwangu Manyoni; thamani yake inatofautiana. Kwa hiyo, nadhani kupunjwa kunakodhaniwa kupo hakupo, kwa sababu kile kitu utafidiwa kwa mujibu wa hali ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali kusimamia utoaji wa ardhi kwa ajili ya kuwezesha wawekezaji kujenga maghorofa yanayojengwa kiholela. Sawa ni ushauri mzuri na lengo moja la Muswada huu ni kufanya yale maeneo ambayo yamejengwa kiholela kuweza kurekebishwa. Wenzetu wote duniani ndivyo wanavyofanya, sisi kwa sababu sheria hii hatukuwa nayo tumechelewa, lakini sasa tutafanya na tunaongeza kasi ya kupima viwanja ili wale wanaotaka kujenga majumba

wasihangaike kupata viwanja vya kujenga. Hili tutalifanya kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya, kwa sababu hawa ndiyo wenye *plot*, Wizara yangu tutasaidiana nao ili viwanja viwepo ili wanaotaka kujenga hayo majengo na kuuzia wenzao waweze kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni nyumba za *National Housing zilizopo* Bukaba, eneo la Miembeni, ziuzwe kwa wapangaji. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Mwijage. Kama nilivyosema, Sheria hii haisemi kwamba, kesho *NHC* waanze kuuza lakini Sheria hii inatoa ruhusa sasa wauze na kila mту atakayenunua kwa mujibu wa Sheria hii, atapata hati miliki ya hiyo *flat* anayoimiliki. Kwa hiyo, Sheria iliweka mazingira ili *NHC* wakiamua kufanya hivyo Sheria imeshawaruhusu, lakini hali ya biashara ndiyo itakayowafanya waamue kuuza au kutokuuza. Kwa hiyo, Sheria sasa imetoea ruhusa.

Kwa nini kesi za *mortgage financing* zinasikilizwa na Kitengo cha Mahakama Kuu na sehemu nyingine Mahakama Kuu haipo? Hili limeulizwa na Mheshimiwa Pindi Chana. Tumepeleka Mahakama Kuu kwa sababu ya kutafuta ufanisi tu ili kesi ziende haraka haraka. Hizi Mahakama nyingine za Mawilayani huku, kesi inakaa miaka mitatu, minne; sasa tunaipeleka Mahakama Kuu ili kutafuta ufanisi kesi zake ziende haraka na ni changamoto sasa kwa Mahakama Kuu, Kitengo cha Ardhi, wajisambaze wafike Mikoa yote ili kuwezesha huu uharaka unaotafutwa na hii Sheria ambayo leo tunaomba muipitishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, kuna wasi wasi kuwa Watanzania wenyе asili ya Kiafrika hawataweza kupata fursa ya kumiliki sehemu za majengo, kwa sababu wenyе uwezo wa kujenga maghorofa si wale wenyе asili ya Kiafrika. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Prof. Mtulia. Sheria hii kwa kweli haina malengo ya kuwanufaisha wasio Waafrika, kinyume chake inataka kuwanufaisha wale ambaо ni wazawa, kwa sababu sisi tulio wengi ndiyo hatuna uwezo wa kujenga. Kwa hiyo, Sheria hii inatujengea uwezo huo wa kukopa tukajenga ama tukakopa, tukanunua au nyumba nzima au sehemu ya nyumba na ndiyo hasa lengo la Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, kama sehemu zote za ghorofa zimeuzwa, umiliki wa ardhi iliyojengwa maghorofa hayo utakuwaje? Hoja hii ni ya Mhesimiwa Ali Hamis. Muswada ule wa kumiliki sehemu za majengo, unatoa utaratibu wa namna ya umilikaji wa sehemu ya nyumba. Eneo lililojengwa nyumba na huduma za pamoja kama ngazi, maji na umeme. Kama sehemu zote za nyumba zikiuzwa, ardhi ilipojengwa nyumba itakuwa inamilikiwa kwa pamoja na wote walionunua ile nyumba. Tunachozungumza hapa ni kwamba, nyumba itakuwa kwenye *plot*, wapo wapangaji 20 pale wameuziwa katika hilo ghorofa, Sheria yetu inasema kile kiwanja ambapo nyumba ile imesimama vilevile kitamilikiwa kwa pamoja na wale wanaomiliki lile jengo. Kwa sababu ukiondoa kile kiwanja kikawa cha mту mwингine, itakuwa kama ile Hadithi ya Abunuwasi. Wewe unaning'inia tu kule juu lakini huku chini haupo.

Kwa hiyo, Sheria inasema kwamba, wote ambaо mnamiliki lile jengo pale na kila mту pale atamiliki, mwингine ana chumba kimoja, mwингine viwili au sita; itaangaliwa

umemiliki asilimia ngapi ya hilo jengo. Kama unamiliki asilimia kumi kwenye jengo hilo, kwenye ile plot kule nje vilevile na wewe utamilikishwa asimilia kumi upate mahali pa ku-park gari lako na kadhalika. Kwa hiyo, utakuwa unamiliki kule juu na huku chini vilevile utakuwa na sehemu yako ambayo utaitumia na wewe kwa shughuli ambazo unataka kufanya ili usioneokane unaning'inia kule juu huku chini hupo kabisa, yaani hunu ambacho unamiliki. Ndani ya jengo hilo kuna maeneo ya pamoja, kwa mfano, zile ngazi, huwezi kumilikishwa ngazi, *corridor*; haya ni maeneo ya pamoja na mtamilikisha kwa pamoja chini ya ule umoja wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine inasema miundombinu iwekwe katika maeneo ambayo wawekezaji kwa kutumia Sheria hizi watajenga. Hii hoja imetolewa na Mheshimiwa Shellukindo ni hoja nzuri kwamba, kule tunapokwenda kuwapeleka kule kwenye kujenga hayo majengo ni vizuri miundombinu ikawepo. Sheria ndivyo inavyosema, huwezi kupeleka watu mahali jengo linajengwa barabara hakuna, maji hakuna kila kitu hakuna. Sheria inasema lazima miundombinu iwe ni sehemu ya hilo jengo ambalo linajengwa. Hii ni kwa mujibu wa Sheria.

Fursa itolewe kwa vijana kupewa mikopo ili waweze kujenga nyumba. Hili ni suala ambalo katika kuelimisha umma, tutaelimisha vijana ili wanapoanza kazi basi waweze kupata mkopo wa nyumba. Mkopo huu ni wa muda mrefu, analipa kwa miaka 20, 10 au 15. Kwa hiyo, kadiri anavyoendelea na kazi ndivyo anavyolipa na baadae anapomaliza kazi atakuwa tayari ana nyumba.

Hoja nyininge; Sheria izingatie jinsia katika masuala ya kusimamia shughuli za kila siku. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Mhagama kwamba, ile Sheria inayosimamia shughuli za lile jengo mnalomiliki kwa pamoja haisemi wanawake ni wangapi na wanaume ni wangapi. Kweli Sheria haisemi, lakini kwenye Kanuni ambazo Waziri atatunga, naahidi kwamba, suala hilo vilevile litatiliwa mikazo, isije ikawa ni Kamati ya wanaume watupu halafu maslahi ya akina mama yasizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyininge; kwa sasa kabla hata ya kupata hii Sheria ya *Unit Titles* wapo wananchi ambao wanamiliki *units* na wengine wanachangisha wenzao katika kujenga hayo majengo. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Basil Mramba na vilevile Mheshimiwa Ndessamburo. Ni kweli kuna baadhi ya watu ambao wameshaanza kuuziana visehemu vya nyumba, lakini walikuwa wanafanya kienyeji. Sheria ilikuwa haipo na ndiyo maana wale ambao wameuziwa vile vipande hata hati hawana, kwa sababu Sheria ilikuwa haitambui. Si hao tu hata watumishi wa Serikali, tulipokuwa tunauza nyumba za Serikali kwa watumishi wa Serikili baadhi ya Watumishi wa Serikali walizwi ghorofa moja lenye watumishi watatu, wanne mpaka watano. Hawa watumishi walishamaliza kulipa mikopo yao kwa Serikali, lakini mpaka leo tulikuwa hatujawapa hati miliki kwa sababu sheria hii haikuwepo. Kwa hiyo, sasa kwa Sheria hii wanaweza wakapata hati miliki kwa sababu sasa Sheria ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyininge; Halmashauri ishirikishwe katika kuhakikisha Sheria hizi zinaweza kuwanufaisha hasa huko vijijiini. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Zitto na sisi tunasema ni ushauri mzuri na Halmashauri zitapata fursa vilevile ya kukopa mikopo hii ya kujenga kwa watumishi wake na zitaiza. Nafasi ya

Benki Kuu haionekani katika Sheria; hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Zitto. Kama nilivyosema mwanzo kwamba, Benki Kuu kwanza katika kutunga Sheria zote hizi mbili, imeshiriki mwanzo mpaka mwisho. Benki Kuu ndiyo itakuwa msimamizi mkubwa na mdhibiti mkubwa katika masuala yote ya mikopo hii ya nyumba. Kwa hiyo, Benki Kuu kutokutajwa katika Sheria, tungekuwa tunasema jambo ambalo lipo tayari. Kwa sababu Benki Kuu uitaje au usiitaje, ilishawapa madaraka ya kusimamia shughuli zote za kifedha pamoja na hii mikopo ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine wakati wa kupandisha riba mkopaji na mkopeshaji wakae na kuzungumza upya. Hoja hii ni ya Mheshimiwa Keenja. Mheshimiwa Keenja, hivyo ndivyo Sheria inavyosema kwa hiyo limezingatiwa. Hoja nyingine; je, mmiliki ya kiwanja chenyе utaratibu wa *unit titles* atakuwa nani? Hoja ya Mheshimiwa Ali Hamis Seif; miliki itakuwa ya wote kama nilivyosema mwanzo, kutakuwa na uwiano wa sehemu ya jengo ambayo mtu anamiliki. Kwa hiyo, kama unamiliki asilimia 50 ya lile jengo, yaani vyumba vyako vingi kuliko wenzako, basi na huku chini vilevile kwenye ardhi utamiliki asilimia 50, kuna uwiano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, hofu juu ya wapangaji wa Shirikia la Nyumba la Taifa kuondolewa kwenye nyumba ili wapewe wapangaji wengine wauziwe. Nilishasema kwamba, Sheria hii haisemi wauziwe moja kwa moja, lakini hata watakapoamua kuuza *National Housing* kwa sababu Sheria sasa inawaruhusu, tutashangaa sana kama wataanza kuleta mikwara kwa hawa waliopo ili wawauzie wengine. Tutakuwa macho ili jambo hili lisitokee endapo *National Housing* wataamua kuwauzia wapangaji wao. Tutasimamia haki itendeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine *Unit Titles Act*, itawanufaisha viyi Watanzania waishio vijiji, hili nilishalijibu kwamba na wao wakishakuwa na kitu cha kuweka dhamana kama nyumba au kiwanja, kwa Sheria hii nao vite vite wanaweza wakanufaika. Wananchi wa kipato cha chini na cha kati watanufaika viyi wakati hawana majengo ya kuweka rehani? Ni kwamba, kuweka rehani si lazima uwe tayari una jengo na jengo hilo uweke rehani. Unaweza ukawa nalo au usiwe nalo; unaweza ukawa na kiwanja hujajenga, kwa hiyo, kiwanja hicho hicho ndicho unakiwekea dhamana na nyumba hiyo unayojenga katika kiwanja hicho ndiyo itakuwa dhamana yenyewe. Hii inawekwa hivi ili kuwasaidia wanyonge wenye kipato cha chini. Kwa hiyo, sisi kazi yetu kubwa katika Wizara yetu na Halmashauri ni kuhakikisha kwamba, Watanzania wanapata hati katika maeneo wanayomiliki.

Watanzania wanamiliki maeneo ya vijiji na mijini, lakini hawana haki. Sasa tuongeze kazi ya kupata hati ili hati hizo ziwe sehemu ya dhamana. Vilevile nyumba ambayo unataka kuinunua yule anayekuuzia ile *unit*; vilevile nayo inaweza ikawa ni dhamana kwa mujibu wa Sheria hii. Kwa hiyo, hakuna wasi wasi kwamba, wale watu wa chini hawatapata mikopo hii kwa sababu hawana nyumba. Hii sheria vilevile imezingatia maslahi ya wanyonge wale ambao hawana nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine; wanasema sheria ya kusimamia ujenzi wa nyumba (*Real Estate Development*) haipo. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Zitto

Kabwe. Kweli sasa hivi sheria ambayo inawasimamia hawa wanaojenga nyumba za kuuza (*Real Estate Developers*), haipo. Sasa hivi Wizara yangu imeanza kuandaa Muswada huo na hata kwenye hotuba yangu ya bajeti katika Miswada niliyosema kwamba, itakuja Bungeni hivi karibuni ni hii sheria ambayo itadhibiti ujenzi wa nyumba (*Real Estate Development Bill*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kutoa ahadi kwamba inakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zungu amesema, mpango wa kuboresha *squatters* Ilala Quarter ulikwama. Sasa Mheshimiwa Zungu kwa sheria hii tunayo sababu ya kuufufua, kwa sababu mkishaziondoa zile *squatters*, yule mwekezaji mliyempata akijenga yale majengo marefu na kila mtu akapata *flats* zake mle, atapata na atapata hati miliki ambayo leo hii zile *squatters* hata miliki hawana. Kwa sheria hii sasa, watapata zile *flats* na hati miliki. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zungu, tufufue na Wizara tutasaidiana na wewe kufufua. Tuanzie pale Ilala Quarter ili iwe mfano kwa *squatters* nyingine Tanzania nzima ambako zimejaa. Tutaanza kwako Mheshimiwa Zungu, tutashirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Zungu alikuwa na lingine kwamba, nyumba zitauzwa kwa bei kubwa ili watu washindwe kununua hasa wenye uwezo mdogo halafu Watanzania wenye uwezo mkubwa ndio wanunue. Tunachokusudia hapa ni kwamba, hizi nyumba ambazo zitajengwa zinamlenga yule mtu wa chini, kwa bei ambayo atawea kununua, ziwe za *National Housing* ama za watu binafsi, kwa sababu sasa akijenga, bei kubwa wananchi wanashindwa kununua, atapata hasara mwenyewe. Kwa hiyo, lengo letu ni kujenga nyumba ambazo Wazungu wanasema ni *affordable*; nyumba ambazo mtu wa chini anaweza akazimudu kununua au kuzikopa, akawa analipa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Zungu alikuwa na wazo kwamba; je, wazawa wanaweza wakaingia ubia na wawekezaji wakajenga hayo maghorofa? Jibu ni kwamba, hilo linawezekana Mheshimiwa Zungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kumchaya, hoja yake ilikuwa inasema kwamba, mabenki sasa hayana mwelekeo katika kuchangia maisha bora kwa wananchi na kwamba, yanawaogopa Watanzania, yanaogopa hasara, yanaogopa kwamba yakiwakopesha uwezekano wa kulipa ni mdogo. Mheshimiwa Kumchaya ni kweli unavyosema kwamba, kwa sasa hivi mabenki yetu yamekaa kibiashara tu. Utaratibu uliopo sasa hivi, rafiki wa Benki wa sasa, haya mabenki ya kibiashara ni mtu mwenye hela, ndio utaratibu uliopo sasa hivi na ndio maana sisi wa kawaiida ambao hatuna hela ni kweli hazitunufaishi sana. Kwa nini, kwa sababu hivi sasa mkopo ni wa muda mfupi, halafu riba ni kubwa. Kwa hiyo, sisi wadogo wadogo wameshatuweka nje.

Kwa sheria mbili hizi, sasa mikopo hii inayoletwa hapa ni ya muda mrefu; kuanzia miaka kumi na kuendelea na vile vile riba itakuwa chini. Lengo lake sasa ni kuwawezesha hawa wadogo na wao vilevile waweze kukopesheka. Si hivyo, sheria hii inasema ile nyumba unayotaka kuniuzia mimi ambaye sina nyumba, hiyo hiyo inakuwa dhamana yangu. Kwa hiyo na sisi wengi sana tutakuwa na dhamana kwa sababu nyumba

imeshajengwa, huyu anayeniuzia huyu, yeze Benki itamlipa, ile nyumba ambayo ameniuzia mimi ndio dhamana yangu, mimi nitalipa Benki kidogo kidogo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kumchakaya, utaratibu huu sasa na sisi ambao tuna uwezo mdogo utatuingiza kwenye hii boti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kumchaya vilevile ametoa tahadhari ya kitu kinachoitwa Money Laundering, yaani wale wanaopata pesa kwa njia haramu, kwa njia za kuza dawa za kulevy, kwa njia mbalimbali, sasa wanaweza wakazileta ili kuzihalalisha kwa kujenga majumba ili zionekane ni halali au kuzisafisha. Hilo linaweza kutokea, lakini mwaka jana tu Bunge hili tulipitisha Sheria ya *Anti-Money Laundering*, kukabili ana na hao ambao wanaweza wakapenyeza pesa za dawa za kulevy, pesa za ujambazi, pesa ambazo zimepatikana kwa njia haramu. Kwa hiyo, sheria inafanya kazi na vyombo vinafanya kazi. Vilevile Benki Kuu wanacho Kitengo Maalum kabisa kinachofuutilia nyendo za uingiaji wa pesa kinachoitwa *Financial Intelligence Unit*. Hiki ni kitengo cha kuangalia huyu Chiligati haya mabilioni yamekujaje, wanatazama. Hii yote inafanya ili nchi yetu isiwe kichochoro cha hizo pesa ambazo zinatokana na mambo haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mtwara watanufaika na mpango huu wa ujenzi wa majengo? Mimi sina wasi wasi; Mtwara watanufaika kwa sababu sasa hivi mnasema umeme upo, bandari inapanuliwa, kiwanja cha ndege kinapanuliwa, barabara ya lami itafika. Yote haya yanaashiria kwamba, wanaojenga nyumba kule watajenga na kuza kwa sababu mazingira yote sasa yanafanya Mtwara pawe mahali ambapo pana faida endapo mtu atajenga nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi alikuwa na wasi wasi kwamba, hawa walio kwenye nyumba sasa hivi watapewa *notice* watoke ili wengine wauziwe. Akatoa mfano wa Wakala wa Nyumba kule Musoma kwamba, ameanza kutoa *notice*. Sasa sina hakika na mfano wake, nyumba za Serikali zina utaratibu wake. Nyumba za Serikali hata kabla ya sheria hii, walishaanza kuziwa kwa wafanyakazi. Kwa hiyo, hawa *TBA* hawatahusika moja kwa moja na sheria kwa sababu wao wana utaratibu wao na sasa hivi wanawauzia watumishi wake. Kwa hiyo, hili litatazamwa kwa namna nyingine. *TBA* wapo chini ya Wizara ya Miundombinu, kwa hiyo, pengine Mheshimiwa Kawambwa atatazama nini kinachoendelea huko Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya nyumba ni jambo jema, lakini utekelezaji wake si itakuwa tu sawa sawa na ile mikopo ya JK? Mheshimiwa Manyinyi, mikopo ile ya JK huwezi kulinganisha na hili jambo, kwa sababu hii ni sheria ambayo mtu na dhamana yako unakwenda kupata mkopo. Mikopo ya JK ni mikopo ambayo haina dhamana, haifanani sana. Pengine ni mapema mno kuihukumu ile mikopo kwamba, haijaleta manufaa kwa sababu Tanzania ni kubwa, mikopo ile si mikubwa sana, haitamfikia Mtanzania kwa haraka. Watanzania walifikiri itawafikia kwa haraka sana, ile mikopo ya JK ni midogo. Hili la leo hatuzungumzii hela ndogo kama zile za JK, hili ni mabenki makubwa ya ndani ya nchi, nje ya nchi yatahusika na hili. Kwa hiyo, hili ni jambo tu sisi wenyewe tuwe na dhamana zetu, mabenki yatatoa mikopo. Hata haya tuliyonayo sasa hivi yameshasema mkishajenga mazingira haya, sisi pamoa na kutoa

mikopo ya kibiashara, tutaanzisha mikopo ya muda mrefu, hawa hawa tulionao hivi sasa. Kwa hiyo, fursa itakuwa ni pana sana kuliko ile ya mikopo ya JK.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Joseph Mungai, alikuwa na ushauri kwamba, tuendelee kukarabati sheria ya ardhi ili vile vipengele vinavyokwamisha kwamisha mambo, tuvirekebishe ili ardhi yetu sasa hivi ambayo kwa kiingereza wasema ni *dead capital*, ni kama mtaji mfu, sasa ardhi hii tuisisimue uwe ni mtaji ambao unafanya kazi, uwatahirishe Watanzania. Mheshimiwa Mungai, tumekuelewa na moja ya shughuli katika Wizara yetu sasa hivi ni kufanya ardhi ya Watanzania, ambayo sasa hivi ni mtaji ambao ni kama mtaji mfu, haiwanufaishi sana Watanzania ardhi. Tutumie kila mbinu, Watanzania watumie ardhi yao kama mtaji (*Working Capital*) na hili la leo ni moja ya hiyo na mengine tutayaibua yatakayowasaidia Watanzania wanufaike zaidi na ardhi yao. Tuna ardhi kubwa sana, lakini Serikali haipati mapato makubwa kutokana na ardhi, kwa sababu ardhi bado ipo kwenye sekta isiyo rasmi. Hatukusanyi mapato kwenye Serikali, mwananchi naye hanufaiki na ile ardhi, ndio hali ilivyo sasa hivi. Kwa hiyo, sasa hivi tutaweka taratibu ili ardhi hii sasa imnufaishe mwananchi na vilevile Serikali iweze kupata mapato kutoka kwenye ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya nchi Duniani, ardhi inaingiza mapato Serikalini namba mbili ama namba tatu, chanzo kikubwa kabisa. Sisi ardhi yetu pamoja na kwamba ni kubwa sana, inaingiza kidogo sana. Mwaka huu bajeti tuliyopitisha juzi ina shilingi trilioni 7.4, kinachopatikana kwenye kodi ya ardhi ni bilioni 18; ni *percent* ngapi? *Zero point zero*; ngapi sijui. Ardhi hii hii tukiwekea taratibu kama hizi, Serikali itapata mapato na wananchi wataitumia ardhi yao vilevile na wao kuboresha maisha yao. Mheshimiwa Mungai, ndiyo lengo hilo, tunashukuru kwa kutukumbusha hilo.

Vilevile ulituambia kwamba, mlolongo wa wawekezaji kupata ardhi ya kuwekeza umesema ni mrefu sana. Nashukuru asubuhi ulinisikiliza vizuri; ni kweli unaanzia kwenye kijiji kwa sababu ardhi ni mali ya kijiji, inakwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya, inakuja pale Wizarani (kituo cha tatu), halafu inawenda kwa Mheshimiwa Rais (kituo cha nne); ni kweli inachukua muda mrefu. Hili tumelifanya makusudi ili kulinda ardhi ya wanavijiji isije kuchukuliwa haraka haraka tukafanana na nchi ambazo leo zina watu ambao hawana ardhi. Haikuwa nia mbaya, tuliweka huu mlolongo ili kulinda ardhi ya wanavijiji isije kuporwa haraka haraka. Tutakwenda tunaboresha na uboreshaji mkubwa ambao tunataka tuufanye ni kuanzisha kitu kinachoitwa *Land Bank*. Nadhani kwenye hotuba yangu, nilieleza mkakati ambao tunataka tuwe na ardhi ya akiba, ardhi ambayo Serikali itakuwa imeipima, si ardhi ya kijiji; imepimwa kwamba ardhi hii ni kwa ajili ya viwanda, ardhi hii kwa sababu ya kilimo tena kilimo cha zao fulani na mwekezaji akija unataka ardhi kwa shughuli gani, anaikuta tayari ipo kwenye *Land Bank*.

Tukishafika hatua hiyo, basi ule mlolongo mrefu utakuwa haupo, kwa sababu hiyo ardhi sasa itakuwa imepimwa na hati ipo. Mwekezaji akienda TIC, anataka kuwekeza katika jambo fulani, *TIC* ndio itakuwa na orodha ya ile *Land Bank*, inampeleka moja kwa moja kwenye ile *plot* inayofanana na matumizi yake na anapata hati kirahisi kuliko ilivyo sasa. Kwa hiyo, huu mlolongo utakwisha pale tutakapoimarisha ile *Land Bank*. Kwa hivi sasa kwa sababu ardhi ipo mikononi mwa wanavijiji, tunailinda kwa mlolongo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mungai ameuliza wanavijiji watanufaikaje na uwekezaji huu ambao watapata ardhi? Hili ni jambo ambalo sisi Serikalini tunalizingatia sana, hatupendi wawekezaji ndio wanufaikie, wanakijiji walaliwe. Hapana! Tunataka mwekezaji apate na wananchi wetu wapate.

Katika mikataba yote ambayo watakuwa wanaingia, tumeshawaambia kwamba, Halmashauri za Wilaya, Maafisa Ardhi washirikishwe ili kuhakikisha kwamba na sisi wananchi wetu wanapata. Mwekezaji anapata maana anakuja kuwekeza, anatafuta apate na sisi vile vile wananchi wapate.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nimalizie kwa kusema kwamba, kama nilivyoeleza asubuhi nilipokuwa nawasilisha hoja yangu kwamba, kupitishwa kwa sheria hizi mbili, kutaleta mapinduzi makubwa katika sekta za ujenzi wa nyumba hapa nchini. Vilevile Bunge hili litakuwa limeweka alama (*landmark*) ya kihistoria kwamba, ndilo lililoasisi mapinduzi katika ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wameumia kwa muda mrefu kwa kujaribu kujenga nyumba wakati hawana uwezo; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameridhia jambo hili liletwe hapa Bungeni kwa njia ya haraka, nasi Wizarani mara mtakapopitisha sheria hii na Mheshimiwa Rais kuiweka saini na sisi tutafanya haraka tuanze kuitekeleza ili haya manufaa ya wananchi yawafikie kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii pamoja na kuwawezesha wananchi kujenga nyumba ama kununua nyumba au sehemu ya nyumba, lakini vilevile sekta ya ujenzi wa nyumba itapata msukumo mkubwa na itatoa ajira nyingi. Fikiria kila ghorofa ambalo linajengwa lazima litaajiri watu kadhaa. Watu hawa ghorofa moja zidisha mara hayo maelefu ya maghorofa yatakayojengwa kwa mwaka, ni ajira kubwa kabisa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hapa tutapitisha jambo ambalo vilevile lina manufaa makubwa sana. Viwanda vya vifaa vya ujenzi kama mabati, cement na kadhaliya navyo vilevile vitasisimka sana kwa jinsi ambavyo hali ya ujenzi nayo itakuwa imesisimka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na manufaa haya ambayo yamelenga kuboresha maisha ya Watanzania ana ambayo vilevile ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, kuhusu ujenzi wa nyumba bora, naliomba kwa heshima na taadhima, Bunge lako Tukufu lipitishe Miswada hii ili ziwe sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Miliki za Sehemu za Majengo wa
Mwaka 2008 (*The Unit Tittles Bill, 2008*)**

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza kifungu cha 6, sehemu ya 3 kuna (a) mpaka (c) ambayo inaelezea “*The common areas of the property shall be...*” Pale zimetajwa *common areas*. Ninapendekeza tuongeze (d) ambayo itasema; “*The common areas shall include common property as agreed by core owners.*” Kwamba, wanaweza wakaamua kujenga jengo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, umesema ni aya ya ngapi?

MHE. PINDI H. CHANA: 6(3).

MWENYEKITI: 6(3); Endelea.

MHE. PINDI H. CHANA: Ipo (a) mpaka (c). Ninapendekeza kifungu (d) kwamba, pale kuna maeneo yametajwa ambayo yatatumika kama *common properties*, kwa mfano, eneo la *parking* katika jengo, eneo la *veranda*, eneo la *balcony*, hizo ni *common properties*. Sasa, yapo maeneo mengine ambayo sheria inaweza isiyaweke, lakini wale *core owners* wakaamua kuayatumia kama *common properties*. Sasa ninaomba sheria izingatie kwa mfano, mnajenga jengo linakuwa na *swimming pool*, ile *swimming pool* mnaamua kuitumia kama *common property, common area*. Kwa kuwa ni ngumu kutaja kila eneo kwa mfano, *gym*, *swimming pool*, kwa hiyo iongezeke (d) inayosema; “*as agreed by core owners,*” yaani kutokana na wao watakavyokubaliana.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Pindi Chana nimeielewa, lakini ni dhahiri kwamba, sheria haiwezi kutaja maeneo yote kama alivyosema. Sheria imesema kwamba, ule umoja ambaao utakuwa na *bylaws* zao, wenywewe watakaa wataweka *bylaws*. Kwa hiyo, kwenye *bylaws* hizo sasa, wanaweza wakaweka na maeneo mengine yote yale ambayo hayakutajwa ndani ya sheria, lakini kwa mazingira yao wanaona kwamba ni muhimu. Kwa hiyo, wataweka katika ile *bylaw* na *bylaw* na ile *Association* yao vina nguvu ya kisheia ndani ya sheria hii.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, nadhani upo sahihi, lakini sioni alivyosema yeye kama kuna tatizo! Alivyosema yeye ni kwamba, kuna kuongeza (d) ambayo ita-*include* vitu vingine ambavyo havikutajwa; Mheshimiwa Waziri, kuna ubaya gani?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, haina ubaya.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, inasomekaje?

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza (d) isomeke; “*The common areas of the properties shall include common properties as agreed by core owners.*” Kwa sababu watakuwa na regulations zao, *common properties as agreed by core owners* na definition ya core owners tunayo kwenye interpretation vilevile definition ya *common properties* tunayo kwenye interpretation.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 7

Ibara ya 8

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 9

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina pendekezo dogo; kifungu cha 9 sehemu ya 3 inaposema “*A proprietor of a unit in respect of which part of the Register is opened under section 9 may, subject to this Act sell, transfer, lease, charge ...*”. Ombi langu, ninaomba liongezwe neno “*mortgage or otherwise deal with that Unit in the same manner.*” Sasa pale katika yale maneno *they can sell, transfer, lease, charge* ninaomba liongezeke neno “*mortgage*”.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, tupo wote? Huu Muswada tunaandika wote, siyo Pindi Chana na Waziri tu, maana naona mmemwachia Waziri na Pindi Chana.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, spirit ya *mortgage* tayari imo katika vifungu vingine. Sasa kama Mheshimiwa anataka tutaje tu kila mahali; lakini fursa yaku-*mortgage* ile *Unit* imezingatiwa katika Muswada. Sasa *unless* anataka tutaje tu kila mahali, lakini nataka nimhakikishie kwamba, fursa ya ku-*mortgage* imo, imezingatiwa katika sheria.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 20

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimeingia nimejaribu kutazama kama Waziri ametoa *schedule of amendment*, lakini sikuiona. Kwa hiyo, ataniwia radhi; kuna vitu vingine vidogo vodogo tuvishughulikie moja kwa moja.

Katika kifungu hicho cha 20, kifungu kidogo cha kwanza kile (b), kina tatizo kidogo kwa sababu huwezi kuanzisha ile sentensi. Zile sentensi zinaanza na “to”, *to use, to participate, to elect, to have*. Sasa hii (b) ningependekeza ibadilike. Ile sentensi ya pili ndiyo ingeanza, ili isomeke “*to transfer his unit to any other person by sale, lease, gift, bequest, hilo neno lingine naliacha hapo nitalizungumzia limeandikwa devise, pledge, mortgage or any other manner permitted by law without approval of the Association*”. Inakaa vizuri kwa flow yake ile.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalize yote katika hiyo?

MWENYEKITI: Sawa.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho kuna neno limetumika pale, najaribu kulitafuta nimeshindwa kuelewa maana yake nini; maana sisi ndio tunatakiwa tuelewe vizuri zaidi, hili la “*devise*”. “*Bequest*” naelewa, hizi ni *noun* zote; *lease, gift*. *Devise is a verb!* Sasa nashindwa kuelewa labda kwenye utaalam wa sheria labda hili neno lina maana yake nyiningine, kwa sababu kwa mujibu wa *Oxford Advanced Learner's Dictionary* ya mwaka 1999 ya *Oxford University Press*, inasema *devise is a verb*, maana yake ni; *to create or to invent a system or a plan and object by careful thought*. Sasa hapa nadhani tungepata hasa maana yake ni nini? Hiyo ni moja.

Katika kifungu hiki hiki kile kifungu cha pili kidogo kina vifungu (a), (b); pale ningeshauri wale wanaokamilisha wawe waangalifu sana kwa sababu, ukisoma ile “*to observe the by-laws* ... kwa sababu ile *hyphen* inakosekana, inatoa maana nyingine kabisa. Kwa hiyo, ningeomba wazingatie, kuna sehemu nyingine nimeona hizi *by-laws* zimekosa ile *hyphen*. *Hyphen* ni neno la kiingereza maana yake ni *short line joining two words*. Kwa hiyo, ikikosekana inatoa maana tofauti katika kifungu hiki. Naomba kuishia hapa. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, tuanze na (b).

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza ile nadhani sina matatizo na marekebisho ya Mheshimiwa Shellukindo, najua ni kunyoosha ile sentensi ili iwiarie na zile nyingine. Hili la...

MWENYEKITI: Neno *devise*?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: *To devise* ni kama unataka kufanya marekebisho fulani kwenye *Unit* yako pale, sasa huwezi kujifanyia tu bila kuiarifu *Association* yako na iweze kukubali. Huwezi kujiamulia wewe na mkeo, mnaanza kubadilisha mambo mle, mnagonga gonga nyundo tu, mnabadilisha mambo bila kuiarifu *Association* na kukubali.

MWENYEKITI: Hiyo *oxford* ya huko Wizarani hata ile *bylaws* kuweka zile *hyphen* lakini zile *semi-colon* pengine ziondoke kwa sababu zimepakana na *and*.

WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Sawa sawa.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 21

Ibara ya 22

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

Ibara ya 26

Ibara ya 27

Ibara ya 28

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 29

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napo ningeomba nikumbushe tena kwenye kifungu cha 29(1)(b), ile *hyphen* pale iwekwe ili isilet maana nyininge.

MWENYEKITI: Sawa na mahali pengine popote itakapoandikwa *bylaws* kwa maana hii msisahau.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 34

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napo ni kuweka sawasawa, kwa sababu sheria ikitoka sisi sote tunahusika, kama ina makosa madogo madogo hata mimi nawajibika katika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kifungu cha 34(1) kimeorodhesha mambo ambayo kimeyawakea sentensi ya kuingilia *association*, maneno yanayofuata yanakwenda vizuri sana, *to give inaendelea, to give again*. Sasa ukija kwenye (c) na (d) inaleta mparangano kidogo, *to not to.. to amend* kwa sababu tayari kuna *to kule* juu, sasa mimi nadhani hii ingerekebishwa ili isomeke kwa kufuata kule juu ambako tumeweka *to ifuatwe* na *noun* hapo kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama mmeona, maana yake haisomeki?

MWENYEKITI: Tumeiona sasa isomekaje?

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mimi nilichotaka waifanyie kazi wasiondoe hiyo *minutes* sikuwa na muda wa kuifanyia kazi, isipokuwa ukisoma, *to not to*
...

MWENYEKITI: Kwa hiyo, itagonga kwenye (c), (d), (e), (f)?

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Ndiyo, isipokuwa kwenye (e) nina pendekizo ambalo nimeliona ni kuibadilisha tu ikatangulia ile sentensi ya katikati pale inapoishia *Mortgage* sasa ile ndiyo itangulie; *to provide a copy of the current financial statement of the association upon the request of the mortgagee*. Unaibadilisha ili

iteremke vizuri na ile *to kule juu*, kwa hiyo, unaiondoa *to moja hapo*, hiyo *to provide* unaiacha halafu itaunganishwa na ile ya juu, hii ya chini nayo ifanyiwe *recasting* kwa sababu huwezi kuanzia na *to such other matters*, *hai-flow* vizuri. Mimi ningeomba niwaachie waitazame wale wanaoandika waziweke vizuri, sikuwa na muda wa kuweza kuiweka vizuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, *alternative* nyingine ni kuweka *to kule inakotakiwa* kwa *association agrees* halafu na ile *to inakwenda inakotakiwa* na pale *isipotakiwa haitafiti*, *that is the best alternative*.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri wataalamu watanyoosha vizuri hizi sentensi kama alivyoshauri Mheshimiwa Shellukindo.

MWENYEKITI: Wasiwasi wetu ni kwamba, kama haijawekwa sawa inaweza ikawa haina maana tunayoitarajia; ndiyo maana hatupendi kufanya vitu hivi lakini kwa sababu ni suala la *grammatic errors* tu.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 40

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ule ukurasa wa 24(1), kile kifungu cha mwisho kabisa kiwekewe ile *to carry out* ili ikutane vizuri zaidi na ile sentensi inayofuata juu.

MWENYEKITI: Naomba urudie tena.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema hicho kifungu cha mwisho (m); *to submit, to do*, kwa hiyo, hapa tuweke *to carry* badala ya kuiacha hivi, haikai vizuri hapa

MWENYEKITI: Kwenye (m) Mheshimiwa Waziri naona sawa.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 50

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kusisitiza tena kifungu hicho cha 50(7) ile *hyphen again*, hapo kuna maneno kama matatu yote yamekosa hizo; kwa hiyo, inakuwa ni maana nyingine kabisa.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 70

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kidogo kupata ufanuzi mzuri; kifungu cha 70 kinazungumzia juu ya mashtaka na kwa mujibu wa kifungu hiki kinasema kwamba, endapo watu wasiposulihisha katika usuluhishi wa migogoro wanapokaa wenyewe wana haki ya kwenda mahakamani na kwa mujibu wa kifungu hiki cha 70 kinasema kwamba atakwenda Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu Mahakama Kuu bado zipo chache, kuna maeneo mengine Mahakama Kuu hakuna. Kitu kingine, *Jurisdiction* ya Mahakama Kuu; ili uende Mahakama Kuu inategemeana na kiwango cha kesi, kama kesi haijafikia kiwango fulani ambacho ni kikubwa kwa kawaida tunashauri uanze na mahakama ya kawaida na baadaye unaweza kukata rufaa Mahakama Kuu, yaani kama kesi ina *less than ten million* unaenda mahakama ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani ipo haja ya kuzingatia na hivyo tuzizoeshe Mahakama zilizopo katika Wilaya na Mikoa kuweza kutatua migogoro ya ardhi kuliko tukisema tuanzie na Mahakama Kuu, pale inasema “*the agreed part may launch his case to the high court land division, or to the district housing or land tribunal where there is no high court land division; sasa naomba tusi-encourage sana High Court, lakini a person has a right to the high court because it is natural justice when the decision made by the district court is not satisfied* lakini asianzie High Court, ndiyo ombi langu na ninaomba lizingatiwe

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki alichokisema Mheshimiwa Mbunge, kinatoa fursa zote mbili, mahali ambapo *High Court* ipo jirani, asizuiliwe mwananchi kutumia na kama ipo mbali, imetoa vilevile fursa kwamba, mwananchi huyu aende kwenye Baraza la Ardhi la Wilaya. Kwa hiyo, mwananchi amepewa fursa zote mbili; *High Court* kama ipo jirani atakwenda na kwa vyovoyote kwa mazingira yetu, *High Court* zipo mbali kweli. Kwa hiyo, hapa kitakachotumika kwa sasa hivi ni kile kilicho jirani na mwananchi na ni Baraza la Ardhi la Wilaya.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 71

Ibara ya 72

Ibara ya 73

Ibara ya 74

Ibara ya 75

Ibara ya 76
Ibara ya 77
Ibara ya 78
Ibara ya 79
Ibara ya 80
Ibara ya 81
Ibara ya 82
Ibara ya 83

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Miliki za Sehemu za Majengo wa Mwaka 2008
(*The Unit Tittles Bill, 2008*)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Unit Titles Act*, ibara kwa ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa *The Unit Titles Act, 2008* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa
Mara ya Tatu na Kupitishwa*)

Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Nyumba wa Mwaka 2008
(*The Mortgage Financing (special provisions) Bill, 2008*)

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Nyumba wa Mwaka 2008 (*The Mortgage Financing (special provisions) Bill, 2008*)

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 8

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha nane kinazungumzia umuhimu wa mtu anayekopa ku-declare kwamba, ana *spouse* lakini hakielezi kwa nini afanye hivyo. Kifungu hiki kilipaswa kumalizia kwa kusema kwamba, huyu *spouse* na yeze atatoa idhini yake ili mkopaji aweze kukopa, kama hakikusema hivyo ni *useless*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kifungu hiki kilipaswa kuzungumzia *spouse with an (s)*, kwa sababu kuna watu wana *spouse* zaidi ya mmoja, kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo lizingatiwe.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, Muswada huu wa pili ni tofauti na ule wa kwanza; ule wa kwanza ulikuwa ni sheria mpya nzima, huu wa pili unarekebisha sheria ambazo tayari zipo. Kwa hiyo, kwenye ile *Principle Act* baadhi ya mambo ambayo anayasema Mheshimiwa Mbunge ndiyo atayakuta kule, kwa mfano, huyu *spouse* kwenye *Principle Act* ndipo alikoelezwa kwamba ni lazima kibali chake kipatikane. Hiyo nyumba unayoenda kuweka rehani ni lazima mwenza, ama wenza na wametafsiriwa kwenye *Principle Act* hapa ni kile kifungu kidogo tu ambacho kinarekeblishwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo nyumba inayowekewa rehani, *spouse au spouses*, kibali chao kimewekwa katika ile sheria kubwa ambayo tunairekebisha.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, katika hii sheria tunayoirekebisha inayo *spouses*?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Kwenye sheria tunayoirekebisha inayo *spouse* na *spouses* kwa sababu inazingatia mazingira yetu ya Kitanzania.

MWENYEKITI: Ndiyo alikuwa anapenda tuweke (s) *somewhere*, nadhani tukiweka (s) *in front of spouse*.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Sawa.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)
Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Nyumba wa Mwaka 2008
(*The Mortgage Financing (special provisions) Bill, 2008*)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima

imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Mortgage Financing (special provisions) Bill*, 2008, ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yote yaliyofanyika. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa *The Mortgage Financing Bill* sasa ukubalike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa
Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu pia wa *Mortgage Financing (special provisions) Act*, 2008, umepita hatua zake zote. Kwa hiyo, Miswada miwili hii, inasubiri sasa kwenda kupata *authority* ya Mheshimiwa Rais.

Waheshimiwa Wabunge, tunao muda mfupi tu uliobaki, kuna mtu kaniletea tangazo hapa linasema tunaomba ututangazie kikao cha Wabunge Wanawake wabaki. Nadhani ni Ukumbi wa Msekwa, hapa wanaanza kufunga jengo lao; kwa hiyo, Wabunge wanawake wakutane Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kwa leo hatuna kazi, kesho tunaingia Muswada wa Biashara ya Ngozi, lakini siyo biashara ya ngozi za watu. Jiandaeni mchukue hiyo Miswada muisome, muielewe na muwe nayo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuaihirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.25 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 31 Oktoba, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*